# Nipashe

Jumanne Januari 14, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580127

www.ippmedia.com

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710




## Wiki moja sarakasi Meya Jiji Dar hadi kung'olewa

UKURASA 2




UKURASA 13

# Wizi wa kutisha waibuka kanisani

**TIMU** ya RC yabaini 'upigaji mamilioni', Mchungaji adaiwa kutumia mali za shule kukopa benki...*Endelea ukurasa wa 21*




## TIKETI MABASI SASA NI KIDIJITALI

UKURASA 3

Basi la abiria la Bright Line lenye namba za usajli T 437 DFJ, linalofanya safari zake kati ya Mwanza na Dodoma, likiwa limeanguka, baada ya kugongana na gari dogo lenye namba T 173 ANW (picha ndogo), katika kijiji cha Isela, Kata ya Samuye, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga jana. **PICHA: MARCO MADUHU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store


## CCM yashtukia vikumbo uchaguzi ubunge, udiwani

UKURASA 2


**MICHEZO** HARERIMANA ATANGAZWA RASMI KOCHA MPYA KMC UK. 31

**MAONI, KATUNI UK.6**



Baadhi ya wanachuo wa Chuo Kikuu cha Ardhi, wakiwa mbele ya sanamu ya Baba wa Taifa, katika eneo la Nyerere Square, jijini Dodoma jana, kujifunza mambo mbalimbali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM yashtukia vikumbo uchaguzi ubunge, udiwani

**Na Jumbe Ismailly,**
MANYONI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewashtukia makada wake kadhaa wanaodaiwa kupigana vikumbo kujipitisha kwa wanachama kama sehemu ya maandalizi ya kugombea nafasi mbalimbali ukiwamo udiwani na ubunge mwaka huu.

Hata hivyo, hatua hiyo inakiuka maelekezo ya chama hicho tawala, ambayo yanawakataza kujihusisha kwa namna yoyote na kampeni za uchaguzi mkuu.

Viongozi wakuu wa chama hicho, hususan Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara, Philip Mangula, mara kwa mara amekuwa akitoa angalizo kwa watakaokaidi, majina yao yatakakwa kama ilivyofanyika mwaka 2015.

Wakati hali ikiwa hivyo, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida, Jumanne Makhanda, amewashtukia baadhi ya makada wanaojipitisha kwa wanachama, ikiwapo kuwapa rushwa kama njia ya kushawishi wawaunge mkono.

Kutokana na hali hiyo, Makhanda amewatahadharisha wote wanaojipitisha pitisha kwa ajili ya kuanza ushawishi, kuwa watashughulikiwa. Aidha, amesema wapo wanaotoa rushwa ya kati ya Sh. 20,000 hadi Sh. 30,000.

Mwenyekiti huyo alitoa agizo hilo kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya hiyo, kilichokutana kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa mwaka 2015-2020 iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa.

Aidha, alisema baadhi ya wanachama wanaodhamiria kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao, wanatakiwa kutoanza kampeni kabla ya wakati.

Mwenyekiti huyo alisema chama hicho hakitasita kukata majina ya wagombea watakaogundulika kuanza kampeni hizo kabla ya wakati.

Kwa mujibu wa Makhanda, wilayani humo wameanza kujitokeza baadhi ya watu wenye nia ya kugombea, kuanza kupitapita na kutoa rushwa kwa wananchi, na kwamba kuna baadhi ya viongozi wamegeuka kuwa madalali wa wagombea hao, jambo ambalo halikubaliki kikanuni.

Alisema wote wenye nia ya namna hiyo hawana nafasi, na hawatakuwa na nafasi hiyo kwa sasa kwani waliopo madarakani wanafanyakazi na ndiyo wanaotumikia ilani ya CCM.

“Na natumia nafasi hii kwenye vyombo hivi vya habari kupiga marufuku watu wote wenye nia ya kugombea nafasi ya kuanzia nafasi ya urais, ubunge na udiwani hawana nafasi. Waliopo wanafanyakazi na ndiyo wanaitumikia ilani ya chama,” alisisitiza Mwenyekiti huyo.

Alisema atakuwa mkali kwa kuhakikisha analisimamia kwa karibu jambo hilo. Kadhalika, aliwaonya baadhi ya viongozi wa chama hicho wanaojigeuza kuwa madalali wa kuwachagulia wananchi viongozi kwa kuwarubuni wananchi kwa kuwahonga fedha.

Alihoji kuwa anayetoa fedha hizo atakapochaguliwa atazirudishaje, na kuwa jambo hilo linalotia shaka. “Wewe unapotoa kati ya Sh. 20,000 au 30,000 unategemea uje upewe huo uongozi, ili kusudi ukalipe nini, hii hela utakuja kuilipaje, kwanza unaipata wapi kama siyo utapeli unaowafanyia wananchi?

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, Chama kilishaweka bayana kwamba kipindi cha kuwachagulia wananchi viongozi kimepitwa na wakati, na kwamba kiongozi yeyote wa chama ni lazima akachaguliwe na wanachama muda utakapofika.

Wakati Makhanda, akishtukia kampeni zisizo rasmi na kutoa angalizo, takribani wiki moja iliyopita CCM Mkoa wa Mara, ilitoa angalizo kama hilo, baada ya kubaini baadhi ya makada kuanza kampeni kabla ya muda.

Mwenyekiti wa chama hicho mkoani humo, Samuel Kiboye, ndiye aliyetoa angalizo hilo kwa makada wanaovunja kanuni za chama kwa kuanza kutangaza nia kabla ya wakati, na kwamba watashughulikiwa kwa kuwa wanahujumu waliopo madarakani.

## Upelelezi kesi ya Kabendera wanukia

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili mwandishi wa habari za uchunguzi, Erick Kabendera, umedai kuwa bado kuna maeneo machache wanayafanyia kazi kwa ajili ya kukamilisha upelelezi.

Madai hayo yalitolewa na Wakili wa Serikali mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega.

Hakimu Mtega aliahirisha kesi hiyo hadi Januari 27, mwaka huu itakapotajwa, na kuamuru mshtakiwa aendelee kukaa mahabusu.

Kabendera anadaiwa kupanga na kushirikiana na genge la uhalifu na shtaka la tatu ni la kukwepa kodi zaidi ya Sh. milioni 173.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa siku na mahali pasipofahamika mshtakiwa alijihusisha na genge la uhalifu. Alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Januari mwaka 2015 na Julai mwaka 2019, alitenda kosa la kutoa msaada kwa genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia maslahi. Katika shtaka la pili, Kabendera anakabiliwa na shtaka la ukwepaji kodi, zaidi ya Sh. 173,247,047.02.

Kabendera anadaiwa kuwa katika tarehe tofauti tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 19, 2019, alishindwa kulipa kodi kiasi cha Sh. 173,247,047,02.

Katika shtaka la tatu, Kabendera anadaiwa kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alitakatisha fedha kiasi cha Sh. 173,247,047.02.

# Wiki moja sarakasi Meya Jiji Dar hadi kung’olewa

**Na Gwamaka Alipipi**

HUKU mahakama ikiagiza alipe gharama za kesi, Isaya Mwita ameendelea kuwa na juma lingine la mikasa baada ya jana kushindwa kuingia Ofisi ya Meya wa Jiji la Dar es Salaam kutokana na mlango kubadilishwa nywila.

Tukio hilo limemtokea zikiwa zimepita siku tano tu tangu anyang’anywe gari alilokuwa analitumia muda mfupi baada ya kutoka kwenye kikao cha uamuzi dhidi ya hatima yake katika nafasi ya Meya wa Jiji hilo la kibiashara.

Akizungumza na Nipashe, Mwita alidai kuwa jana asubuhi, alifika kwenye ofisi yake iliyoko kwenye Jengo la Karimjee jijini ili aendelee na majukumu yake ya kikazi, lakini alikuta mlango wa ofisi yake umebadilishwa namba za siri.

“Ni kweli mlango wa ofisi yangu umebadilishwa ‘pass word’ (nywila), hivyo nilishindwa kuingia, lakini baada ya dakika kadhaa kupita, alikuja meneja na kunisaidia kunifungulia na niliingia ofisini na kutoka, na sasa niko mahakamani,” alidai.

Mbali na mikasa hiyo miwili, wiki iliyopita, kulitokea vurugu katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Jiji hilo, kilichoitishwa kwa lengo la kufanya uamuzi wa ama kumng’ao au kumbakisha katika madaraka hayo.

Vurugu hizo ziliibuka baada ya Diwani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kudai kutiwa saini kwa jina la mjumbe kutoka Chama cha Wananchi (CUF), ambaye hakuwapo ndani ya chumba cha mkutano.

Hatua hiyo ambayo diwani huyo aliitafsiri kuwa ni mbinu za kulazimisha kutimiza akidi, ilisababisha mvutano uliotulizwa na askari polisi walioingia ndani ya ukumbi.

Baraza hilo lilikuwa limekutana ili kupokea taarifa ya uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizokuwa zinamkabili Mwita baada ya timu iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda kumchunguza.

**KORTINI**

Jana, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ilikubali kuiondoa kwa gharama kesi ya madai namba 3/2020, baada ya Mwita aliyefungua, kuomba kuiondoa kwa sababu tayari walalamikiwa wa kwanza, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, walishamng’oa katika kiti hicho tangu Januari 9, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mtega baada ya mlalamikaji kuwasilisha maombi ya kuiondoa kesi hiyo na walalamikiwa kukubali ombi hilo.

Kabla ya mahakama kutoa uamuzi huo, Wakili wa Mlalamikaji, Hekima Mwasipu, alidai msingi wa kuiondoa kesi hiyo ni kwamba Januari 8, mwaka huu, waliwasilisha maombi madogo ya zuio chini ya kiapo dhidi ya mlalamikiwa wa kwanza (Jiji) na wa pili, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, wasiitishe mkutano wa kumng’oa kwenye kiti chake.

Alidai waliomba zuio hilo kwa sababu walalamikiwa wa kwanza na wa pili, walitaka kumng’oa mlalamikaji katika kiti chake cha umeya.

“Mheshimiwa Hakimu, tuliomba kwamba mahakama isipotoa zuio, mlalamikaji atakosa haki ya

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Tiketi mabasi yote sasa kiektroniki

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

CHAMA cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa), kinatarajia kuanza kukatisha tiketi kwa njia ya kielektroniki mwezi ujao kwa kampuni zote za mabasi, ili kupunguza msongamano unaojitokeza.

Vilevile, Taboa imesema inatekeleza agizo la Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Atashasta Nditiye, kuhusu kuzingatia leseni zao katika usafirishaji wa vipeto kwenye mabasi.

Katibu wa chama hicho, Enea Mruto, katika mazungumzo na Nipashe jijini Dodoma jana, alisema baada ya kikao chao na Mamlaka ya Mapato (TRA), wamekubaliana ukatishaji tiketi ufanyike kwa njia ya elektroniki kuanzia mwezi ujao kwa mabasi yote.

"Kama TRA hawatatuangusha kile tulichokubaliana nao, basi mpango huo utaanza rasmi mwezi ujao, tunahitaji kufanya kazi kwa kwenda na teknolojia mpya," alitamba.

Alisema utaratibu huo ulioanza katika baadhi ya kampuni za mabasi, utatumika kwa kampuni zote za mabasi baada ya kukamilika kwa baadhi ya mambo waliyokubaliana kisha utazinduliwa rasmi na kuwekwa agizo kwa mabasi yote.

Alisema mfumo huo utasaidia kuwarahisishia wateja kupata tiketi au kuweka maombi ya kukata tiketi kwa njia ya mtandao.

"Unajua mambo sasa hivi yanakwenda kisasa zaidi, hivyo na sisi tunahitaji kwenda kiteknolojia," alisema na kukiri kuwa tayari kuna kampuni chache za mabasi nchini zimeujaribu utaratibu huo.

Kuhusu zuio la Nditiye kwa mabasi kusafirisha baadhi ya nyaraka, Mruto alisema Taboa inatekeleza agizo kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa kwenye leseni zao za usafirishaji wa vipeto.

Alisema hata katika mkutano wao uliopita, wamiliki walisisitiza agizo hilo ili kuendana na sheria zinavyotaka.

"Taboa tunatekeleza agizo hilo, atakayekiuka atakupambana na mkono wa sheria, hivyo kila mmoja anapaswa kutekeleza sheria," alionya.

Mruto pia alisema Taboa imeweka mikakati mingi ya kuboresha huduma zake na kuhakikisha ajali za barabarani zinapungua nchini kwa kuhimiza umakini katika kampuni za mabasi, hasa kwa madereva.

Alisema chama hicho kitakuwa kinasisitiza wamiliki wa mabasi kufanya ukaguzi katika vyombo vyao vya moto mara kwa mara ili kuepusha ajali.


## BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED(BOA)** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo wa hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini,alipe deni analodaiwa.Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana(mali)yake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1 | NYAULI DRILLING COMPANY LIMITED/MICHAEL ALFRED MAUNGO | Nyumba ya makazi yenye Hati ya umiliki CT Na.464117,Kiwanja Na. 286,Kitalu "GG" Iliyopo Manispaa ya Mwanza,Eneo la Nyakato iliyopo kwa jina la MICHAEL ALFRED MAUNGO |
| 2 | KWANDIKWA MSALENGE MLEBWA | Nyumba ya makazi yenye Hati ya umiliki CT Na.28056,kiwanja na.27,Kitalu "D"Iliyopo manispaa ya Mwanza, Eneo la Nyegezi .Iliyopo kwa jina la KWANDIKWA MSALENGE MLEBWA |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**BOA Bank**
**Head Office,**
**Ohio Street/Kivukoni Front,**
**P.O. BOX 3054,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2110104**
**+255 22 2111290**



## BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na **ECO BANK TANZANIA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo wa hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini,alipe deni analodaiwa.Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana(mali)yake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1 | ZUNGU USED SPARES AND LUBRICANT/KHALID SAID SALUM. | Kiwanja chenye Hati Ct Na.85413,Kiwanja na.48, Kililopo Manispaa ya Temeke eneo la Amani Gomvu Dar es salaam,kilichopo kwa jina la KHALID SAID SALUM. |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Eco bank,**
**Head Office,**
**Kinondoni Road,**
**P.O. BOX 20500,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2137447**
**+255 22 2137446**



## JAGA AUCTION MART LIMITED.
TABATA-BIMA, PO BOX 11133, DAR ES SALAAM-TANZANIA
Tell: 0713123427, 0766121079, EMAIL: jagauction16@gmail.com

### NOTISI YA KULIPA DENI/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.

Kwa idhini tuliyopewa na **MAPAMBAZUKO SACCOS LTD** tutauza kwa **MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA MIKOPO YA WADAIWA.** Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini. Tunatoa notisi ya siku 14 toka siku ya tangazo hili.

| SN | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA | MAHALI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ROBILO MTWANGAMBATE | NYUMBA | TUANGOMA | 1/02/2020 |
| 2. | STEPHEN MICHAEL MAGEMBE | KIWANJA | TABATA KINYEREZI | 29/01/2020 |
| 3. | MAGIGE FRANK PAUL | KIWANJA | MSONGOLA YANGE YANGE | 8/02/2020 |
| 4. | LILIAN CAMILLUS MARIKI | KIWANJA | MPIGI MAJOE | 15/02/2020 |
| 5. | YVONNE MAJEVU | KIWANJA NA NYUMBA | KIPUNGUNI B" MOSHI BAR | 25/01/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itaauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi anatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo asilimia 75% yalipwe ndani ya siku (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/ mpangaji na zingine zinazo ambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**Kwa TAARIFA ZAIDI WASILIANA NA:**

**MAPAMBAZUKO SACCOS LTD**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**P.O BOX 24705,**
**DAR ES SALAAM,**
**Tel: 0783 072 460**
**Tel: 0678 022 216**

**JAGA AUCTION MARTLIMITED**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 11133,**
**DAR ESSALAAM,**
**Tel: 0713123427**
**Tel: 0766 121 079**

115582902



## TAARIFA KWA UMMA



115581702

**TIMON ENOCK**

Mtajwa hapo juu, sio mfanyakazi wa M/S Twiga Paper Product Limited P.O. Box 20192 Dar es salaam, Mtaa wa Chuma, Chang'ombe Dar es salaam, tangu tarehe 01.01.2020 na hahusiki na shughuli zozote zinazohusu Kampuni ya M/S Twiga Paper Product Limited. Hivyo basi Kampuni haitahusika na MIAMALA au shughuli zozote zitakazofanywa na mtajwa hapo juu.

**IMETOLEWA NA UONGOZI WA**
**M/S TWIGA PAPER PRODUCT LIMITED**


# Maelfu wamiminika kusajili laini za simu

**Na Salome Kitomari**

ZIKIWA zimebaki siku sita, idadi ya wanaosajili laini za simu kwa mfumo wa alama za vidole inaongezeka.

Akizungumza jana na Nipashe, Ofisa Mwandamizi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Semu Mwakyanjala, alisema hadi Januari 7, mwaka huu jumla ya laini 25,160,147 zilisajiliwa ikiwa ni asilimia 42.42.

Aidha, alisema jumla ya laini 22,796,472 hazijasajiliwa, na kuwataka wananchi kutumia vyema siku zilizosalia kukamilisha usajil wao.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, ambao hawajasajili laini zao ni asilimia 47.5.

"Mwamko wa wananchi kujisajili unazidi kukua kadri siku zinavyokwenda, ndiyo maana kunaongezeko la usajili," alisema na kuongeza:

"Usajili huu ni muhimu sana kuwalinda wananchi dhidi ya wizi, ulaghai, utapeli na uchochezi."

Kwa mujibu wa Mwakyanjala, kuna jumla ya laini 47,956,619.

Awali, mwisho wa usajili ulikuwa ni Desemba 31, mwaka jana, lakini Desemba 27, Rais John Magufuli wakati anasajili laini yake kwa alama za vidole wilayani Chato, mkoani Geita, aliongeza siku 20 hadi Januari 20, mwaka huu.

# Waziri aagiza meli iliyokamatwa uvuvi haramu itolewe bandarini

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amemtaka Mmiliki wa Meli ya Buah Naga 1, iliyokamatwa kwa makosa ya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu, kuiondoa haraka meli hiyo kwenye Bandari ya Mtwara, ili kupisha shughuli zingine za serikali.

Amesema meli hiyo inapaswa kuondolewa bandarini huko kwa kuwa tayari mahakama ilishatoa hukumu dhidi ya kesi hiyo.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo iliko meli hiyo inayomilikiwa na raia wa Malaysia, Waziri Mpina alisema jana kuwa kukamatwa kwa meli hiyo na kisha mahakama kutoa hukumu ya kifungo cha miaka 20 jela au kulipa faini ya Sh. bilioni moja, ni uthibitisho kuwa serikali ya awamu ya tano haina mzaha katika kusimamia rasilimali zake, zikiwamo za uvuvi.

Waziri huyo alisema meli hiyo ni ya pili kukamatwa na kuchukuliwa hatua na serikali, kutokana na kufanya uvuvi haramu katika Bahari Kuu ndani ya miaka 10, ya kwanza ikiwa ni Tawariq 1, iliyokamatwa mwaka 2009 na aliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dk. John Magufuli, sasa Rais wa Tanzania.

Mpina alisema baada ya Dk. Magufuli kukamata meli hiyo miaka 10, baadaye, serikali anayoiongoza imekamata tena meli nyingine na kuitangazia dunia kuwa Tanzania imekataa kuwa shamba la bibi la kila mtu kuja kufanya anachotaka.

Alisema adhabu iliyotolewa na mahakama inatoa fundisho na ujumbe kwa wamiliki wa meli na vyombo vingine vinavyotumika kufanya shughuli za uvuvi, kuzingatia sheria za nchi.

Waziri huyo alisema serikali itaendelea kufanya doria na operesheni katika ukanda wa Bahari Kuu na kudhibiti meli zote za kigeni zilizotumika kuvua katika maji ya Tanzania bila kufuata sheria.

Alisema uvuvi huo usiozingatia sheria za nchi, si endelevu kutokana na wavuvi kuvua papa na kisha kutupa miili yao baharini baada ya kuondoa mapezi.

Desemba 2018, Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Rushwa Kanda ya Mtwara, iliwahukumu watu watatu wakiwamo raia wawili wa kigeni na Mtanzania mmoja, kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja au kulipa faini ya Sh. bilioni moja baada ya kukamatwa wakifanya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu Januari mwaka huo.

Watu hao walikamatwa katika 'Operesheni NMATT', iliyokuwa inaendeshwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola.

Watu hao walikamatwa wakiwa kwenye meli ya Buah Naga 1 ya Malaysia wakiwa na kilo 90 za mapezi ya papa bila kuwa na miili yake, kinyume cha sheria.

Pia mwishoni mwa mwaka jana, Bunge la Tanzania lilipitisha Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Chakula Duniani wa kupambana na kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama, Spika Job Ndugai akitaka juhudi zaidi kufanyika kulinda rasilimali za uvuvi akisisitiza kuwa endapo hazitasimamiwa vizuri, zitatoweka.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akifunua pazia la jiwe la msingi kuzindua jengo la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi jana. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo. **PICHA: OWM**

# Ajali ya basi ilivyoua wawili

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATU wawili wamefariki dunia, huku saba wakijeruhiwa ajali ya basi lenye namba za usajili T 437 DFJ Bright Line, wakati likitokea Mwanza kwenda Dodoma kugongana uso kwa uso na gari dogo.

Ajali hiyo ilitokea jana majira ya asubuhi katika Kijiji cha Isela Kata ya Samuye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

Imeelezwa kuwa basi hilo lilipofika eneo hilo lilikutana na mwendesha bodaboda katikati ya barabara na kumkwepa, ndipo likakutana uso kwa uso na gari ndogo lenye namba za usajili T 173 ANW na kusababisha ajali.

Akisimulia, abiria aliyenusurika kwenye ajali hiyo, Matei Onyango, alisema walipofika kwenye kijiji hicho wakati basi likiwa katika mwendo wa kawaida, wakashangaa kuona linaanza kuyumba walipo angalia mbele kujua kuna nini, ndipo wakaona kofia ya mwendesha bodaboda imerushwa juu kisha wakagongana na gari ndogo.

"Mimi ni mkazi wa Rorya mkoani Mara, napeleka watoto wangu wawili shuleni Igunga, nikiwa ndani ya basi hili nikiangalia video ya wanyama, tulipofika eneo hili nikaanza kuona basi linayumba, kutizama mbele nikaona kofia ya mwendesha boda imerushwa juu, kidogo nikasikia kishindo kikubwa cha kugongana na gari dogo, ndipo tukapata ajali," alisema Onyango.

"Namshukuru Mungu mimi na watoto wangu wawili tumetoka salama licha ya kupata majeraha madogo, lakini kama dereva angekuwa kwenye mwendo kasi sidhani kama tungesalimika... ajali ni mbaya sana ukiona hata namna tulivyoanguka," aliongeza.

Kwa upande wake Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Athony Gwandu, ambaye alikuwapo eneo la tukio, aliwataja watu wawili waliofariki papo hapo kwenye ajali ni Paulina Obedi (12) ambaye ni abiria, na mwendesha bodaboda aliyefahamika kwa jina moja na Saidi, mkazi wa Kijiji cha Busongwa Shinyanga Vijijini.

Alisema majeruhi hao saba walikimbizwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, na wanapatiwa matibabu, huku abiria wengine waliosalimika waliwasafirisha kwenye basi lingine na wanaendelea na safari. Gwandu alifafanua kuwa basi hilo lilikuwa na abiria 55.

Alitaja chanzo cha ajali hiyo kuwa ni dereva wa basi hilo kujaribu kumkwepa mwendesha bodaboda, ndipo alipokutana uso kwa uso na gari jingine dogo na kugongana uso kwa uso, na kuwataka madereva wote wa vyombo vya moto wakiwamo bodaboda kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali.

## Majaliwa 'aiamsha' Takukuru uchunguzi wizi fedha korosho

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameutaka uongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ukamilishe mapema uchunguzi dhidi ya madudu yaliyoibuliwa katika mbio za Mwenge wa Uhuru 2019 na wizi uliofanywa na viongozi wa AMCOS kwa wakulima wa ufuta na korosho ikiwamo Wilaya ya Ruangwa.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua jengo la Takukuru Wilaya ya Ruangwa lililogharimu zaidi ya Sh. milioni 142. Alitoa wito kwa Takukuru kuwa imara na kutembea kifua mbele katika mapambano hayo.

Alisema pamoja na Takukuru kuendelea na utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, na ameuagiza uongozi wa taasisi hiyo ukamilishe mapema utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Rais John Magufuli aliyoyatoa kwao kwa nyakati tofauti.

Alisema ameshuhudia kazi nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya kupitia uchunguzi na ufuatiliaji wa madai ya malipo ya wakulima wa zao la ufuta na korosho.

"Kamilisheni chunguzi hizi zote kwa wakati ili hatua stahiki za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya wale wote waliopatikana na hatia."

Alisema rushwa huathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. "Kutokana na ukweli huo, serikali imetoa msukumo wa pekee katika kushughulikia vitendo vya rushwa na ufisadi. Msukumo huo, umechangia kwa kiasi kikubwa husan katika kipindi hiki, utekelezaji wa miradi mikubwa na ya kimkakati kwa ufanisi na kwa wakati."

Alisema wananchi wanatakiwa wafahamu kwamba nchi yoyote ambayo rushwa imetamalaki siyo rahisi kuwa na uwezo wa kiuchumi utakaoiwezesha nchi hiyo kumudu kulipa madeni ya ndani na ya nje. "Hata hivyo, kwa upande wa Tanzania tunashuhudia jinsi Serikali ya awamu ya tano inavyolipa madeni."

Kwa mfano, kati ya Julai na Septemba, 2019, Sh. bilioni 85.72 zimetolewa ikiwamo bilioni 50 za madai ya pensheni; bilioni 22 za madai ya watumishi wa umma ikiwamo kiinua mgongo kwa wastaafu 3,019 na malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 1,435; bilioni 10.24 zimelipa watoa huduma na zaidi ya bilioni 2 kwa ajili ya makandarasi na wahandisi washauri. Hayo ni matokeo ya jitihada za kupambana na rushwa zinazofanywa na serikali.

Alisema tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, imekuwa ikijipambanua na vita dhidi ya rushwa na ufisadi. Hivyo, kitendo hicho cha kuendelea kulipa madeni ni ishara ya mafanikio ya serikali katika jitihada zake za kuzuia na kupambana na rushwa nchini, na kuwa serikali itaendelea kudhibiti mianya yote ya rushwa katika

INAENDELEA UK. 8



Msamaria mwema (kushoto), akimsaidia mwendesha baiskeli kuinyanyua baada ya kuzidiwa na mzigo na kupinduka, katika Barabara ya Mikocheni Viwandani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mashine mpya yawatibu kansa wagonjwa 1,100

**Na Mary Geofrey**

MASHINE mpya ya kisasa ya kutibu saratani iliyosimikwa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road takribani mwaka mmoja na nusu sasa, imetumika kutibu wagonjwa 1,141, wakiwamo 208 waliokuwa wapelekwe nje ya nchi.

Idadi hiyo ya wagonjwa waliokuwa waende nje ya nchi, wametibiwa nchini kwa mafanikio makubwa na kuokoa Sh. bilioni 10.4 ambazo zingetumiwa na serikali kwa matibabu ya ughaibuni.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Julius Mwaiselage, alipozungumza na waandishi wa habar, maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, walioitembelea jijini Dar es Salaam.

Alisema ili kuimarisha huduma za uchunguzi na tiba, serikali iligharamia ununuzi na kusimika mashine mpya na za kisasa za kutibu saratani 'Linear Accelerator' mbili na CT-Simulator na kuanza kutoa huduma Septemba mwaka 2018.

Alisema tangu mashine hizo zianze kazi na kuzinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Machi 29 mwaka jana, pia zimepunguza muda wa kusubiri tiba ya mionzi kutoka wiki sita hadi kufika chini ya wiki mbili.

"Mashine hizi ni za kisasa zinazotumia teknolojia ya 3D, zinapatikana katika hospitali kubwa ya saratani duniani kama India, Ulaya na Marekani na ni za kwanza kusimikwa katika ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema.

Aliongeza kuwa mashine hizo pia zimesaidia kuongeza idadi ya wagonjwa wanaotibiwa kwa siku kwa kutumia tiba ya mionzi kutoka wagonjwa 170 hadi 190 kwa siku ilivyokuwa awali hadi zaidi ya 300 kwa sasa.

Dk. Mwaiselage alisema mashine hizo pia zimesaidia kuanzisha huduma za kupima CT-Scan katika taasisi na kufika Septemba mwaka jana, jumla ya wagonjwa 1,430 walichukuliwa kipimo hicho katika taasisi hiyo badala ya kufuata huduma hiyo katika hospitali nyingine kama ilivyokuwa siku za awali.

Alisema zimesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa kwenda kutibiwa nje ya nchi, akibainisha kwamba mwaka 2015/16, wagonjwa 164 wa saratani walipatiwa rufani ya nje ya nchi, lakini baada ya maboresho wagonjwa 14 walipatiwa rufani kwenda nje ya nchi kwa kipindi cha mwaka 2018/19. "Na wagonjwa wanaokwenda India kwa ajili ya matibabu, wengi wao hufanyiwa tiba kwa mara ya kwanza, na wanaporudi nchini huendelea na matibabu hapa kwa sababu wanashauriwa kuwa tayari Tanzania tuna mashine za kisasa za kutibu wagonjwa," alisema.

Alisema kutokana na kuimarika kwa huduma za saratani katika taasisi hiyo, wagonjwa kutoka nchi za jirani za Kenya, Comoro, Malawi, Msumbiji, Zimbabwe, Congo DRC na Burudi wameongezeka kuja nchini kupatiwa matibabu.

Sambamba na hilo alisema upatikanaji wa dawa katika taasisi hiyo ni asilimia 100 na pia mapato ya dawa yameongezeka kutoka Sh. milioni 70 kwa mwezi hadi milioni 800 hadi 900 kwa mwezi.

Alisema pia wameanzisha duka la dawa la jamii katika taasisi hiyo na kusaidia upatikanaji wa dawa kwa bei nafuu, kulikosaidia kuongeza mapato ya taasisi kutoka Sh. milioni 569.87 mwaka 2014/15 hadi Sh. bilioni 14.77 mwaka 2018/19.

Dk. Mwaiselage alisema asilimia 60 ya wagonjwa wenye dalili za awali wanaofika hospitalini hapo, wanatoka hospitali za wilaya na kwamba wana uwezekano mkubwa wa kupona tofauti na wanaofika wakiwa wamezidiwa.

Alisema kuna ongezeko la wagonjwa wa saratani kutoka 40,885 mwaka 2015/16 hadi wagonjwa 64,747 mwaka 2018/19.

Alisema moja ya sababu za ongezeko hilo ni mwitikio wa jamii kupima afya na ongezeko la ugonjwa huo duniani kote.

Alisema kwa Tanzania, saratani inayoongoza ni ya mlango wa kizazi ikifuatwa na ya matiti, mfumo wa chakula na muunganiko wa kichwa, shingo na koo na wagonjwa wengi wanatoka katika mikoa yenye wakazi wengi, ikiongozwa na Dar es Salaam.

# Kizimbani tuhuma kunajisi mtoto wake

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAHAKAMA ya Mkoa wa Wete imempandisha kizimbani mwanaume mwenye umri wa miaka 43, mkazi wa Taifu Wilaya ya Wete kwa kosa la kumnajisi mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 12.

Akisomewa shtaka lake mahakamani hapo na mwendesha mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Ali Amour Makame, ilidaiwa kuwa mtuhumiwa alitenda kosa hilo Novemba 30, mwaka 2019.

Ilidaiwa kuwa kosa hilo alimtendea mtoto wake huyo saa 3:00 usiku eneo la Taifu Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Ilidaiwa kuwa bila ya halali, alimwingilia mtoto huyo, huku akijua kuwa ni mtoto wake wa kumzaa, jambo ambalo ni kosa kisheria.

Kumwingilia maharimu ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 143 (1) (4) cha Sheria Namba 6 ya Mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

Baada ya kusomewa shtaka lake, mtuhumiwa huyo alikana kutenda kosa hilo, na kuiomba mahakama impatie dhamana, ombi ambalo lilikataliwa na mahakama.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, aliamuru mtuhumiwa huyo kupelekwa rumande hadi Januari 27, mwaka huu ambapo kesi hiyo itasikilizwa.

# Mitambo ya mabilioni yatua kwa Mkemia Mkuu serikalini

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imenunua mitambo tisa yenye thamani ya Sh. bilioni 6.5 katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli, kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa mamlaka hiyo.

Kutokana na kuwapo kwa mitambo hiyo ya kisasa, mamlaka hiyo imepunguza siku za kupima vinasaba na kutoa majibu kutoka ndani ya siku 21 ilivyokuwa awali hadi siku moja kwa sasa.

Mafanikio hayo yalielezwa jana jijini Dar es Salaam na Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, alipozungumza na waandishi wa habari na maofisa mawasiliano wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, waliotembelea mamlaka hiyo.

"Uwekezaji huu wa mitambo ya kisasa umeongeza kasi na uwezo wa GCLA kufanya uchunguzi wa sampuli mbalimbali, zikiwamo za dawa za kulevya, uchunguzi wa mazingira, vinasaba vya binadamu na wanyama na ubora wa chakula," alisifu.

Alisema kuwapo kwa mitambo hiyo ya kisasa pia kumesaidia kutoa huduma kwa wingi na kwa kasi kulinganisha na miaka ya nyuma.

Alisema mamlaka hiyo pia imefanikiwa kukarabati miundombinu ya ofisi zote za kanda nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 1.3, hivyo kusaidia kuboresha utendaji kazi.

Dk. Mafumiko alisema katika kipindi hicho, pia walifanikiwa kusajili wadau wa kemikali 2,426 na vibali 21,336 na kufanya kazi katika mipaka yote na katika bandari nchini kwa saa 24.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo Shein kupaisha maendeleo ya Zanzibar

**MAADHIMISHO** ya Miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar yamedhihirisha jinsi serikali ya awamu ya saba inayoongozwa na Rais Dk. Ali Mohamed Shein, ilivyofanya vizuri katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Kabla ya kilele cha sherehe hizo juzi, miradi mbalimbali iliyowekwa mawe ya msingi kwa ajili ya kuanza kutekelezwa na iliyofunguliwa kwa ajili ya kuanza kutekelezwa, imedhihirisha umakini wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) chini ya Dk. Shein ilivyofanya vizuri katika kuwaletea wananchi maendeleo na kukuza uchumi wa Zanzibar.

Miradi mingi mikubwa ilihusu barabara, elimu, afya, utalii na sekta nyingine kadhaa ambazo kwa namna moja au nyingine ambazo zitazalisha ajira kwa wananchi na kuongeza pato la serikali.

Katika hotuba yake juzi kwenye kilele cha maadhimisho hayo, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kutokana na kuongezeka ukusanyaji wa mapato ya serikali, watumishi wasishangae kuongezewa mshahara. Hiyo ni kauli inayoleta matumaini kwa watumishi na pia inadhihirisha kuwa serikali imejitahidi kukusanya mapato ya kutosha kwa ajili ya kujiendesha na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Rais Shein alitaja mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika kipindi cha miaka tisa ya utawala wake katika sekta ya afya, elimu, uchumi na miundombinu.

Alisema kasi ya ukuaji uchumi iliongezeka kutoka asilimia 4.3 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka 2018, pato la taifa limeongezeka kutoka Sh. bilioni 1,768 mwaka 2010 hadi kufikia Sh. bilioni 2,874 mwaka 2018. Alisema lingine ni Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar, Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2020 pamoja na Maendeleo ya Kimataifa.

Rais Shein alisema vilevile, pato la mwananchi nalo limeongezeka kutoka wastani wa Sh. 942,000 sawa na Dola za Marekani 675 mwaka 2010 hadi Sh. milioni 2,323,000 sawa na Dola za Marekani 126,000 mwaka 2018.

Alisema mfumuko wa bei nao umepungua kutoka asilimia 14.7 mwaka 2011 hadi kufikia asilimia 3.9 mwaka 2018, utekelezaji wa miradi ya maendeleo 304 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 3.42 iliyotengeneza ajira 16,866 hadi mwaka 2018.

Kwenye sekta ya elimu alisema wamefanikiwa kuainisha elimu bure, shule zimeongezeka, idadi ya wanafunzi imeongezeka, hadi mwaka 2019 shule za awali zilikuwa 382 zikiwa na wanafunzi 85,984 ikilinganishwa na mwaka 2010 kulikuwa na shule 238 na wanafunzi 29,782.


Alisema shule za msingi zimeongezeka kwamba mwaka 2010 kulikuwa na shule 299 zikiwa na idadi ya wanafunzi 226,812, mwaka 2019 zimeongezeka na kufikia shule 381 zikiwa na wanafunzi 290,510. Alisema shule za sekondari nazo zimeongezeka, kwamba mwaka 2010 kulikuwa na shule 105 zikiwa na idadi ya wanafunzi 80,208, mwaka 2019 zimefikia shule 284 zikiwa na idadi ya wanafunzi 130,713.

Rais Shein alisema bajeti ya sekta ya afya imeongezeka kutoka Sh. bilioni 10.81 mwaka 2010/11 na kufikia Sh. bilioni 104.24 mwaka 2019/20. Idadi ya kusomesha madaktari imeongezeka, ambapo kwa sasa daktari mmoja anatibu wagonjwa 6,276 kulinganisha na mwaka 2010 ambapo daktari mmoja alikuwa anatibu wagonjwa 31,838.

Alisema serikali ya Zanzibar imeongeza malipo ya wastaafu kwa mwezi kutoka Sh. 25,000 mwaka 2017 hadi kufikia Sh. 90,000 mwaka 2019.

Haya ni mafanikio makubwa na tunatarajia kuwa hadi Dk. Shein anamaliza muda wake wa uongozi mwishoni mwa mwaka huu, mipango mingi aliyoanza kuitekeleza itakamilika na kuleta manufaa kwa Wazanzibari. Yote hata yamefanyika kutokana na mazingira ya amani na utulivu aliyoyajenga katika kipindi chake na uongozi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hivi navyo ni vikwazo kwa maendeleo elimu

Na Sabato Kasika

**KUNA** mengi ambayo yamekuwa yakitajwa, kwamba ni kikwazo cha maendeleo ya elimu kwa wanafunzi, ikiwamo ukosefu wa chakula shuleni, uhaba wa madawati, vyumba vichache vya madarasa na mengine kadhaa.

Lakini yapo mengine mawili nayaona makubwa zaidi, ambayo huwa hayatajwi sana. Hii ni kwa baadhi ya wamiliki wa shule kucheza na akili za Watanzania, kwa kutengenezea watoto matokeo ili wafaulu na shule zao zipate umaarufu.

Wanafanya hivyo, ili wazazi wavutike na kuamini kwamba shule hizo zinafundisha vizuri na kupeleka watoto wao huko, lakini nyuma yake wakitengeneza mazingira ya biashara zaidi.

Ni mtindo unaoharibu wanafunzi, kwani wanapocheza na akili za Watanzania, mwisho wa siku mwanafunzi anatengenezewa mazingira ya kufaulu. Akienda sekondari anashindwa kusonga mbele.

Bahati nzuri serikali imeligundua hilo na sasa imeanza kulifanyia, kwa kuwasimamisha kazi wale wote wanaotuhumiwa kuhusika katika udanganyifu wa matokeo ya mtihani wa darasa la saba.

Mwaka juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliwataka wamiliki wa shule kuacha kucheza na akili za Watanzania kwa kutengenezea watoto matokeo.

Alisema, wanafanya hivyo watoto wafaulu ili shule zao zipate wanafunzi wengi na kwamba anajua wapo kibiashara, ila wanawaharibu wanafunzi, kwa vile wakipelekwa kidato cha kwanza wanashindwa kusonga mbele.

Alitoa onyo hilo, huku baadhi ya watendaji, maofisa elimu na walimu wakuu wakiwa wamesimamishwa kazi, kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizowakabili ili kupata ukweli wa tuhuma hizo.

Pamoja na hilo la kucheza na akili za Watanzania, lipo lingine la huduma za waganga wa kienyeji la kutangaza dawa za kuongeza akili vichwani mwa wanafunzi, ambalo ninaliona ni uhuni.

Matangazo ya aina hii, yanaweza kuchangia kuwafanya wanafunzi wanaotoka kwenye familia zinazoamini dawa hizo wasijibidiishe, katika masomo wakiamini wataongezewa akili za darasani na kumbe ni uongo.

Huduma zinazotangazwa na waganga hawa sidhani kama walipata vyeti vya usajili kutoka Baraza la Waganga wa Jadi lilipo pale katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kuratibiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kwa tafsiri ya haraka haraka ya matangazo hayo ni kwamba, mwanafunzi hana haja ya kujisomea kwa bidii, kwa vile dawa za kumuongezea akili za darasani ili afaulu mitihani. Huu ni uzushi wa hali ya juu.

Zipo baadhi ya mbinu kumfanya mwanafunzi afaulu, mojawapo ni kuweka malengo maalumu ya kusoma kila siku, kuwa na ratiba binafsi ya kujisomea nyumbani na kuifuata, ahakikishe akiwa nyumbani ana ratiba ya kujisomea sio unapokuwa shuleni tu.

Ni muhimu ajisomee, katika muda anaodhani unafaa zaidi, uwe ni wa kutosha kwa kila somo na ayapende masomo na tena uyafurahie na pia ajenge tabia ya kuyaombea masomo kila siku na kila mara.

Vilevile, katika mwendelezo huo, ajisomee kwa bidii na asipoteze muda kwa mambo yasiyo na lazima, apende kuukomboa wakati na atambue muda ukipita haurudi tena.

Mwanafunzi awe na mahali maalumu pa kusomea, ahakikishe mahali pa kusomea hapana kelele za aina yoyote na asifanye mambo mengi kwa wakati mmoja, akitimiza hayo katika masomo atafaulu tu.

Hizo ndizo mbinu zinazotajwa kumfanya mwanafunzi awe na maendeleo mazuri darasani, lakini akitegemea kuonyeshwa majibu ya mtihani au kuongezewa akili za darasani atasubiri sana na hawezi kutimiza ndoto zake.

Pia wataalamu wa afya wanasema, kuna mambo, ambayo ubongo wa binadamu unatakiwa kuyafanya kwa ufanisi, ili mtu aonekane kuwa ana akili ambayo ni timamu.

Miongoni mwake ni uwezo wa kujifunza na kuelewa haraka, kutunza kumbukumbu na kuwa na uwezo wa kutumia tena taarifa zilizotunzwa katika ubongo, ili kuzichanganua, kulingana na hali halisi ya mazingira yanayomkabili.

Wanasema, mtu anaweza kuutazama ubongo kama kompyuta ilivyo na mfumo tata wa kuchakata taarifa, ambayo utendaji wake hutegemea uwezo wa mtumiaji, kwamba hivyo ndivyo ilivyo akili ya binadamu.

## Mabwawa SGR yatishia afya wanakijiji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAKAZI zaidi ya 100,000 wa Kijiji cha Parakuyo Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro wameiomba serikali kuingilia kati kutokana na afya zao kuwa hatarini kufuatia makandarasi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) kuchimba mabwawa 10 ya kumwaga maji taka pembezoni mwa makazi ya watu.

Akizungumza na timu ya wanahabari waliotembelea kijiji hicho, Mwenyekiti wa kitongoji cha Ngoisani, ambacho ni sehemu ya kijiji hicho ambako mabwawa hayo yamechimbwa, Kokan Stert, alisema maji hayo yenye kemikali zenye yanayodhaniwa kuwa na sumu yameanza kuleta madhara kwa binadamu na mifugo.

Alisema madhara wanayopata binadamu ni kutoa harufu mbaya, inzi na wadudu kutoka katika mabwawa hayo na kuzagaa katika makazi ya watu, huku mifugo ikiungua midomo inapokwenda kunywa maji ya Mto Mkata ambao upo jirani na mabwawa hayo.

"Haya mabwawa yamechimbwa katika kitongoji hiki cha Ngoisani yamekuwa yakihatarisha maisha ya wananchi na mifugo yao kutokana na uchafu na kemikali unaotokana na mitambo ya mashine na uchafu wa vyoo, ambao unatupwa katika mabwawa, tunaomba yafukiwe na kuhamishwa sehemu isiyo ya makazi ya watu," alisema mwenyekiti huyo.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Senta kinachounda kijiji hicho, Joseph Somei, alisema hawapingani na mradi huo kwa kuwa nao ni wanufaika, lakini mabwawa hayo yamekuwa yakihatarisha afya zao pamoja na mifugo na kuomba serikali kuangalia namna ya kulishughulikia tatizo hilo.

"Haya mabwawa yamechimbwa bila kutushirikisha sisi kama viongozi wa vitongoji vyenye makazi ya watu, yapo maeneo mengi yasiyo na makazi yangeweza kuchimbwa bila kuleta athari kwa wananchi, lakini sio hapo yalipochimbwa," alisema Somei.

Alisema, madhara ya mabwawa hayo uonekana zaidi nyakati za mvua kutokana na kujaa na kutawanyika katika makazi ya wananchi, huku yakitoa harufu kali, hali ambayo ni tishio kwa afya za wakazi wa maeneo hayo.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, alivipongeza vyombo vya habari kwenda kuibua kero hiyo, na kwamba hatua za haraka zitachukuliwa ili kuokoa afya za wananchi wa kijiji cha Parakuyo.

Ofisa Mazingira katika Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro, Venance Segere, alisema amekuwa akifanya kazi kwa pamoja SGR kuhusu masuala ya mazingira na kutatua kero mbalimbali za wananchi walio pembezoni mwa mradi huo, lakini tatizo la mabwawa hayo hajawahi kupata malalamiko, na kuahidi kuchukua hatua za haraka.

# Lindi yavuka lengo makusanyo maduhuli

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKOA wa Lindi umevuka lengo la kukusanya jumla ya Sh. 4,773, 999,943 ikiwa ni maduhuli ya kodi inayotokana na ardhi, uuzaji wa viwanja na mashamba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019.

Hayo yalielezwa na Katibu Tawala wa Mkoa huo, Rehema Madenge, alipokuwa anawasilisha taarifa ya utekelezaji kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, wakati wa ziara yake mkoani hapa.

Madenge akiwasilisha taarifa hiyo kupitia kwa Katibu Tawala (Uchumi na Uzalishaji), Majidi Myao, alisema makusanyo ya maduhuli hayo ni ya kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019, huku halmashauri tatu za Lindi Manispaa, Kilwa na Nachingwea zikivuka lengo lililowekwa.

Alisema katika kipindi hicho, Mkoa uliwekewa lengo la kukusanya Sh. 2, 870,000,000, lakini kwa kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Juni 2019, uliweza kukusanya jumla ya Sh. 4,773,999,945 sawa na asilimia 166, huku Halmashauri za Ruangwa, Liwale na Lindi/Mtama zikishindwa kuvuka lengo.

Alisema Lindi Manispaa inaongoza kwa kukusanya Sh. 2,981,632,103 sawa na asilimia 189, wakati lengo lilikuwa ikusanye Sh. 1,580,000,000, kifuatiwa na Kilwa iliyokusanya Sh. 1,479, 576,121, sawa na asilimia 148 wakati lengo ilitakiwa kukusanya Sh. 1,000,000,000.

Alisema Nachingwea lengo ilikuwa kukusanya Sh. 100,000,000, lakini ilikusanya Sh. 180,923,355 sawa na asilimia 181, Liwale Sh. 95,357,134 wakati walitakiwa wakusanye Sh. 100,000,000, huku Lindi/Mtama lengo ilikuwa ikusanye Sh. 10,000,000, lakini walichokikusanya ni Sh. 9,332,578 sawa na asilimia 93.

Kuhusu migogoro, alisema mkoa umeanzisha kamati za kusikiliza na kusuluhisha migogoro na malalamiko yanayohusu ardhi, mipaka na madai ya fidia ikiwa ni ni asilimia 100 ya lengo lililokusudiwa.

Naibu Waziri akizungumza na watumishi walio chini ya wizara anayoiongoza, alizitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha zinalipa serikali kuu kodi zinazohusu ardhi.




Katapila likikata miti katika eneo la Sinza kwa Remmy, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kupisha ujenzi unaoendelea wa upanuzi wa barabara ya Shekilango. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waathirika wa mafuriko waomba makazi ya muda

**Na Idda Mushi,** MVOMERO

WAATHIRIKA wa mafuriko yaliyotokea katika maeneo mbalimbali ya kijiji cha Kilimanjaro, Kata ya Kichangani wilayani Mvomero, Mkoa wa Morogoro, ambao nyumba zao zilibomolewa na maji, wameiomba serikali kuwatafutia makazi ya muda.

Pia wameomba msaada wa chakula wakati jitihada zikiendelea za kutafuta makazi ya kudumu, huku wanaositiriwa kwa ndugu, jamaa na marafiki, wakiishi kwa tabu katika maeneo hayo kwa kuingilia faragha za familia zingine ambazo hazikuwatarajia.

Waathirika hao wa mafuriko yaliyotokea mwishoni mwa mwaka jana, walisema hayo wakati wakizungumza na waandishi wa habari kwenye hafla ya kupokea misaada mbalimbali ya kibinadamu iliyotolewa na kampuni ya vinywaji Baridi ya Coca Cola na Mbunge wa Mvomero, Suleiman Sadiq Murad. Baadhi ya wananchi hao, Amrani Juma Bakari, Mkazi wa Kitongoji cha Mtoni alisema wanapokaa kwa sasa wananyanyasika kwa vile wengi wa waliowastiri wamepanga, na hawana makazi ya kudumu, na wamewapokea kwa dharura, hivyo ni vyema serikali ikawaangalia kwenye suala zima la makazi ya muda.

Kadhalika waliomba kuharakisha upatikanaji wa viwanja ili wahamie katika maeneo mengine.

Fadhili Ramadhani Msindugu, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mtoni, anadai bado hali yake na wananchi wake ni ngumu, baada ya mvua kunyesha milimani na kuporomosha kingo za mto, na kwamba licha ya kutoa taarifa na tahadhari, suala hilo halikupewa uzito hadi kusababisha nyumba 64 kuondoka na maji sambamba na makaburi kadhaa ya wapendwa wao.

"Binafsi nimeondokewa na nyumba, sasa hivi naishi mpakani mwa kitongoji cha Mtoni na Msikitini, nimepata hifadhi ya muda, ninachohitaji msaada wa haraka ni makazi ya kuishi, kwani maisha tunayoishi sasa ni magumu sana, tukipata hata mahema ya muda, chakula na masuala ya kiafya itatusaidia sana," alisema Msindugu.

Akabainisha mvua hizo ziliondoa hata vyoo vya wakazi, hivyo kwa sasa hali ni mbaya kutokana na watu kujisaidia ovyo, na kuhatarisha afya za wakazi kutokana na milipuko ya magonjwa.

Mwajuma Kamwendo, mkazi wa Kijiji cha Kilimanjaro, ambaye ni mwenyekiti wa waathirika, anadai nyumba anayoishi makaburi ya familia yaliondoka na maji, na walifanikiwa kunusuru makaburi 14 tu.

Mbunge wa Mvomero, Murad, alisema aliwasilisha suala hilo katika mamlaka mbalimbali sambamba na kuomba misaada kwa wadau vikiwamo viwanda takribani vitano na kupata msaada toka kiwanda cha sukari Mtibwa waliokubali pamoja na mambo mengine, kurekebisha miundombinu ya maeneo yaliyoathiriwa na kampuni ya viwaji baridi ya Coca Cola, kwa kushirikiana na yeye binafsi, wakikabidhi misaada ya kibinadamu ya thamani ya zaidi ya Sh. milioni 20 kwa ajili ya kaya 64 zilizoathiriwa.

Misaada iliyokabidhiwa ni pamoja na magodoro 200, mchele kilo 500, maharage kilo 500, sembe kilo 500, vyandarua 200, mashuka 200 na kila aliyehudhuria halfa hiyo ya ugawaji wa vifaa akipata kinywaji cha Coca Cola.

Aidha, alisema atachukua ripoti ya waathirika hao na kuipeleka kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenister Mhagama, wakati jitihada mbalimbali za ngazi za wilaya na mkoa zikiendelea kushughulikia suala hilo, na kupokea ripoti mbalimbali juu ya maafa hayo sambamba na jitihada zaidi zikiendelea kuhakikisha maafa hayo yaliyopoteza pia maisha ya baadhi ya watu, hayajirudii tena.

Meneja Mawasiliano na Mahusiano wa kampuni ya Coca Cola, Victor Aron, alisema wameguswa kuwasaidia wahitaji hao kutokana na changamoto zilizowapata kwa kuamua kurudisha sehemu ya faida yake kwa wateja wao.

Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Mohamed Utaly, aliutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kuharakisha mchakato wa kuwapa wananchi hao maeneo ili waanze ujenzi ikiwamo kuangalia mashamba pori yaliyotwaliwa umiliki wake na serikali wakati mazungumzo na viongozi wa kiwanda cha Mtibwa ukiendelea wa kuomba maeneo.

# Majaliwa ataka kasi ujenzi mahakama

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameutaka uongozi wa mahakama kukamilisha ujenzi wa majengo ya mhimili huo, ili kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu na kutumia gharama kubwa katika kutafuta haki zao.

Amesema kati ya wilaya 139 Tanzania Bara, ni 111 ndizo zenye huduma ya mahakama za wilaya na zingine 28 zinahudumiwa wilaya za jirani ambazo zimepewa mamlaka ya kisheria kuhudumia mahakama zisizo na majengo ya wilaya.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizindua jengo la Mahakama ya Wilaya ya Ruangwa.

Alisema ni vyema uongozi wa Mahakama uhakikishe yale yote waliyojipangia kwenye mpango mkakati wa miaka mitano wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mahakama 2016/17 - 2020/21 unatekelezwa kwa wakati.

Waziri Mkuu alisema kabla ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Wilaya Ruangwa mwaka 2009, wananchi wa wilaya hiyo walisafiri umbali wa kilomita 180 kufuata huduma za mahakama wilayani Lindi.

"Umbali huo mrefu ulisababisha wananchi wengi kupoteza muda mwingi ambao wangeutumia kwa uzalishaji mali. Wakati mwingine wananchi walikosa haki zao kwa kushindwa kumudu gharama za usafiri kuhudhuria mashauri yao wilayani Lindi," alisema.

Majaliwa alisema mahakama ni muhimu katika kudumisha amani na kuleta maelewano ndani ya nchi au jamii ambayo huwa kichocheo cha kiuchumi, hivyo ameipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kuamua kujenga mahakama hiyo wilayani Ruangwa na sehemu zingine nchini.

Alisema kupitia mahakama, migogoro mingi hupata usuluhishi, hivyo kuimarisha hali ya amani na utulivu.

"Kwa lugha nyingine, mahakama inapokuwa imara, taifa letu huvutia uwekezaji kwa kuwa wawekezaji wanakuwa na uhakika na usalama wao pamoja na mali zao," alisema.

Kadhalika, Waziri Mkuu alisema serikali kwa upande wake itaendelea kushirikiana na Mahakama kuhakikisha kuwa mipango yake iliyojiwekea inatekelezwa kama ilivyokusudiwa kwa kuwa bado kuna kazi kubwa mbele yao.

Wakati hu huo, Waziri Mkuu ameipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kukusanya mapato kupitia mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali (Government electronic Payment Gateway- GePG) kwa kuwa serikali ilielekeza kila taasisi itumie mfumo huo ili kupunguza mianya ya rushwa na upotevu wa fedha.

Alisema amefurahi kusikia kuwa kwa kutumia mfumo wa GePG, Mahakama iliongeza makusanyo kutoka Sh. bilioni 1.6 mwaka 2017 hadi Sh. bilioni 2.5 Desemba, mwaka jana baada ya kuanza kutumia GePG.

"Fedha hizi zitatumika kuchangia ujenzi wa mahakama na miundombinu mingine ya kiuchumi unaoendelea katika kila kona nchini.

"Ni ukweli usiofichika kwamba hata wananchi nao wanafarijika kuona kuwa kile mnachowatoza kinaenda moja kwa moja kwenye mfuko mkuu wa serikali na baadaye kiasi fulani kinarudi kwenu kujenga miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi," alisema.



Baadhi ya wajumbe wa Kikao cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Manyoni, jana, kwa ajili ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi wa mwaka 2015. **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# Wiki moja sarakasi Meya Jiji Dar hadi kung'olewa

**INATOKA UK. 2**

kusikilizwa na kesi ya msingi haitakuwa na maana kuwapo mahakamani, tunaomba kuiondoa bila gharama,"

"Januari 9, mwaka huu, mlalamikiwa wa kwanza aliitisha mkutano wa wajumbe wa Halmashauri ya Jiji kwa lengo la kumvua katika nafasi yake ya umeya na mkutano huo ulifanikiwa kumwondoa mlalamikaji katika kiti hicho," alidai.

Mwasipu alidai mlalamikaji hajapata haki ya kusikilizwa ndiyo maana anaomba kuiondoa kesi bila gharama.

Hata hivyo, Wakili wa Serikali, Rashid Mohammed alidai walalamikiwa wote, Jiji, Mkuu wa Mkoa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hawana pingamizi na maombi ya mlalamikaji.

Alidai kuwa kwa sababu mlalamikaji ameamua kuiondoa kesi hiyo, walalamikiwa wametumia gharama mbalimbali, hivyo iondolewe kwa gharama.

Hakimu Mtega alisema kwa sababu mawakili wa pande zote mbili wamekubali kesi hiyo kuondolewa, mahakama yake imekubali na inaiondoa kesi hiyo kwa gharama.

Mapema Januari 10, mwaka huu, mahakama hiyo ilitupilia mbali maombi madogo ya kuomba zuio la mlalamikiwa wa kwanza na wa pili, kufanya mkutano wa kumwondoa mlalamikaji katika kiti cha umeya.

Miongoni mwa tuhuma zilizokuwa zinamkabili Mwita hadi kufikia hatua ya kuundiwa timu ya kumchunguza, ni kutotumia Sh. bilioni 5.8 kutoka Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Fedha hizo ni asilimia 51 ya hisa zilizotolewa na kampuni ya Simon Group kama sehemu ya ununuzi wa asilimia 51 ya hisa za UDA.

Tuhuma nyingine ni kutumia vibaya gari la ofisi ambayo alipata nalo ajali, kushindwa kuongoza kikao cha baraza la madiwani na kusababisha Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, kugombana na Meya wa Temeke, Abdallah Chaurembo. Tuhuma nyingine ni kudaiwa kuwapendelea baadhi ya mameya, hasa waliotokana na vyama vya upinzani, kuingia kwenye kamati za fedha.

## Majaliwa 'aiamsha' Takukuru uchunguzi wizi fedha korosho

**INATOKA UK. 4**

utendaji mzima wa serikali.

Hata hivyo, Waziri Mkuu alisema tafiti za hivi karibuni zilizofanywa na wadau wa mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora kama vile Transparency International (TI), MO Ibrahim na Afro barometer zinaonyesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo, yaani 2016 hadi 2018 Tanzania imeendelea kufanya vyema katika mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora.

Alisema mafanikio hayo ya kujivunia ni jitihada za serikali za kusimamia kwa dhati mapambano dhidi ya rushwa kwa usimamizi wa Takukuru ambayo ndicho chombo kilichopewa dhamana kisheria.

"Tambueni kwamba uongozi mzima wa juu kabisa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu) uko pamoja nanyi katika vita dhidi ya rushwa na ufisadi," alisema. Pia ameagiza kuanzishwa kwa vilabu vya kupambana na rushwa katika shule ili wanafunzi waweze kuwa na uelewa na kuweza kutoa taarifa za rushwa.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema jengo hilo limejengwa kwa miezi saba kuanzia tarehe Juni 11, 2018 na kukamilika Januari 25, mwaka jana, na kuwa hadi kufikia hatua ya uzinduzi, limegharimu Sh. 142,857,142.86.

Kuhusu uchunguzi, alisema kwa kipindi cha mwaka 2019 Takukuru imefanya uchunguzi kwenye tuhuma kubwa ikiwamo ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Magufuli aliyoyatoa Oktoba 15, 2019 kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika wilayani Ruangwa.

"Kupitia uchunguzi ule, tumebaini kwamba zaidi ya vyama 30 vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) vya Mkoani Lindi viliwadhulumu wakulima wa ufuta kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni Sh. 1.23. Kupitia uchunguzi huo tuliwakamata na kuwahoji zaidi ya viongozi 300 wa AMCOS zilizokuwa zinahusika katika dhuluma hii. Tulifanikiwa kuokoa zaidi ya Sh. bilioni 1.042. Fedha hizi zilikuwa ni mali ya wakulima wa ufuta ambao walidhulumiwa fedha hiyo na Viongozi wa Vyama vya AMCOS."

## HABARI KITAIFA

# Bajaji watakiwa kuzingatia sheria

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

VIJANA waendesha bajaji katika Manispaa ya Iringa wametakiwa kufuata sheria za usalama barabarani ili kupunguza malalamiko yanayotolewa na wadau ya kwamba wao ndio chanzo kubwa cha ajali.

Wadau hao walisema pamoja na kwamba bajaji na na bodaboda zimeleta neema kwa vjana wengi nchini kumekuwapo na baadhi ya malalamiko kwa vijana wanaondesha vyombo hivyo vya moto kuvunja sheria za usalama barabarani pamoja na kujihusisha na vitendo vya uhalifu katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo, wadau mbalimbali mjini Iringa wamesema biashara ya bajaji imesaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana pamoja na kupunguza pia suala la uhalifu kwa sababu wanatumia mwingi kushinda na bajaji na bodaboda.

Walisema biashara ya bajaji imeajiri vijana wengi wasomi na wasio wasomi ambao wanaendesha bajaji hama kwa kuajiriwa au kwa kumiliki wenyewe na kujipatia kipato.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jumson Group, Juma Nchakwi, alisema kuwa biashara ya bajaji imeleta mapinduzi makubwa kwa vijana ambapo wengi wao wameajiriwa na kujiajiri, na kuwa awali walikuwa hawana shughuli za kufanya zaidi ya kukaa vijiweni na kushirikia vitendo vya uhalifu.

Alisema kuwa vijana wengi walikuwa wanajishughulisha na mambo ya uhalifu kama kukaba watu na kupora vitu watu, lakini kwa sasa waendesha bajaji.

Alisema wengi wanaendesha bajaji na bodaboda wakiwamo vijana wanaomaliza vyuo nao wanaendesha bajaji hama za kwao au za watu kwa wameajiriwa.

Nchakwi ambaye anajishughulisha na uuzaji wa bajaji mjini Iringa, alisema kuwa uwapo wa bajaji na bodaboda pia umeongeza ushirika na ulinzi shirikishi katika jamii, na kunapotokea uhalifu vijana wao wa bajaji wanapigiana simu na kufanyikisha kumdhibiti mhalifu kabla vyombo vya usalama hawajafika tayari wao wanakuwa wamefika.

Changamoto kubwa ya tasnia ya bajaji ni kwamba bei ni kubwa ambapo bajaji mmoja huuzwa kati ya Sh. milioni saba na Sh. milioni nane, wakati vijana wengi hawana mitaji mikubwa kununua bajaji.

Alisema kuwa vijana wanaomaliza vyuo wamekuwa wanajihusisha na shughuli za kuendesha bajaji na bodaboda, lakini wakiwa katika vikundi wanaweza kununua bajaji au bodaboda kwa kuunganisha nguvu.

Alisema mabenki mengi hayakopeshi vijana kwa vile hawana mtaji, lakini kama watajiunga katika vikundi na vikasajiliwa wanaweza kukopa bajaji kupitia kwenye vikundi vyao.

Naye Mwenyekiti Umoja waendesha bajaji mjini Iringa, Nobert Sunka, alisema kuwa umoja huo unasaidia vijana wengi kukopa bajaij na mpka sasa vijana zaidi ya 1,000 wapo kwenye ajira ya bajaji.

Alisema kuwa pia uwapo wa bajaji umepunguza uhalifu kwa asilimia 90 kwa Manispaa ya Iringa kwa vile vijana wengi zaid wameajiriwa kwenye sekta ya bajaji.

# Wahitimu darasa la nne, la saba kufundishwa ufundi

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

ASASI ya kiraia ya Tanzania Development Forum (TADEFO) inatarajia kuwakusanya vijana waliohitimu darasa la saba na kidato cha nne ambao hawakuendelea na masomo ili kupatiwa elimu ya stadi za kazi.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki Mjini Kibaha na Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Mohamed Lacha, alipokuwa akizungunza na Nipashe.

Lacha alisema wanatarajia kufanya hivyo ili kuwezesha kundi hiyo kujiajiri, na kuachana na kukaa mtaani bila kazi.

"Lengo letu ni kuisaidia serikali katika mapambano ya kupndokana na adui umaskini ambaye anadumaza maendeleo kwenye maeneo mbalimbali, mkakati wetu huu utawawezesha vijana kujiajiri kwa kufanya shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato na kuondokana na utegemezi kwa wazazi na ndugu," alisema Lacha.

Aidha, alisema baada ya kupewa mafunzo, pia watatakiwa kuunda makundi ambayo yatawapa fursa ya kupata mikopo kwenye halmashauri na taasisi nyingine za kifedha.

Vijana hao pia wataunganisha na Vyuo vya Mamlaka ya Ufundi Stadi (VETA) ili kupata ujuzi zaidi wa kiufundi, ili ukidhi vigezo vya kuajiriwa na kampunii.

"Vijana hawa pia watanufaika na elimu za usimamizi wa miradi ili kila anayekuwa na mradi wake ukawe endelevu na kuwa na namna ya utunzaji wa fedha wazitumie kwa malengo waliyokusudia," aliongeza Lacha.

Tadefo ni Asasi isiyo ya Kiserikali ambayo ilianzishwa mwaka 2019, ikilenga kujishughulisha na shughuli za kijamii.



Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Malamba Mawili, Kata ya Msigani, jijini Dar es Salaam, Idd Mgweno, akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara, alioitisha kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali ikiwamo kuanzisha ulinzi shirikishi ili kukabiliana na vitendo vya uhalifu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Sababu wakulima kupata mavuno kidogo zatajwa

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

WAKULIMA wamebainisha sababu za kupata mavuno kidogo, wakisema hali hiyo inatokana na idadi kubwa ya wakulima kutokuwa na uelewa wa kilimo chenye tija.

Imeelezwa kuwa badala yake wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea, hali ambayo inasababisha mazao kushindwa kunawili vizuri na kutoa mazao mengi.

Hayo yameelewa na baadhi ya wakulima katika Kijiji cha Busoka Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, na kwamba wakulima wengi hasa waishio vijiji wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea chenye kutegemea mvua pasipo kutumia mahitaji mengine ikiwamo mbegu bora na mbolea.

Walisema kilimo hicho kimekuwa kikiwafanya wavune mazao kidogo ukilinganishwa na wakulima wanaolima kilimo chenye tija, na kwamba hawana elimu ya kilimo chenye tija kutoka kwa wataalamu wa masuala ya kilimo.

Charles Jumanne, alisema kuwa katika shamba lake la hekari moja analolilima mahindi, amekuwa akivuna magunia yasiyozidi manne kwa kuwa hana uwezo wa kutumia njia za kitaalamu kulima kilimo chenye tija.

Naye Juma Lucas alisema ingawa ana zizi la ng'ombe, mwaka huu hajatumia mbolea ya samadi kutokana na kukosa muda wa kutoa mbolea hiyo kwenye zizi, na kwamba anatamani mahindi yake kuyafyeka ili alime mazao mengine kwa kuwa hana uhakika wa kuvuna hata gunia moja.

Mmoja ya wakulima anayelima kilimo chenye tija katika kijiji hicho, Laurent Nkwabi, alisema katika shamba lake la mahindi la hekari moja amekuwa akivuna magunia zaidi ya 20 kila mwaka kutokana na kuzingatia misingi ya kilimo bora, huku akiwataka wakulima kuondokana na kilimo cha mazoea.

"Katika shamba langu mwaka jana nilipata gunia 20 za mahindi na hata mwaka huu naamini nitapa zaidi ya hayo kwa namna nilivyoweka," alisema na kuongeza:

"Watu wengi hawana maandalizi ya kilimo unaweza ukakuta mtu ana zizi ila halitumii, cha msingi tu maofisa ugani wajaribu kuhitisha mikutano kwenye vijiji na vitongoji ili wawape elimu wakulima."

Ofisa kilimo, umwagiliaji na ushirika wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Samson Sumuni, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitoa elimu kwa wakulima kuhusiana na namna ya kulima kilimo chenye tija, huku akiwataka wakulima kuwatumia maofisa ugani waliopo katika kila kijiji kwa ajili ya kuwapa ushauri.

# Kampeni kujiunga vifurushi vya NHIF

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umezindua kampeni ya uhamasishaji wa wananchi kujiunga na vifurushi vya bima ya afya ili iwe rahisi kwa Watanzania kupata matibabu bila kulazimika kutumia fedha taslimu.

Wananchi wanahimizwa kujiunga na bima kwa kuwa licha ya kuimarisha afya, pia inaimarisha uchumi.

Akizungumza wakati akizindua kampeni hiyo jijini hapa Mwenyekiti wa Bodi ya NHIF, Anne Makinda, alisema hospitali zipo ila wanashindwa kwenda kutibiwa kwa vile hawana bima kwani Tanzania mpya ni pamoja na wananchi wake kuwa na bima na duniani pote bima ni lazima.

"Ukiugua unatibiwa haraka na unakuwa na uhakika wa kupata matibabu, mambo ya kuugua hayachagui muda na hayana tarehe wakati mwingine unaugua una hela, bima itakuwa na mtindo na utaratibu wa maisha yako na kufanyakazi kwa uhakika," alisema na kuendelea: "Hivyo wito wangu ni kwamba Watanzania mtafute bima ya afya."

Pia aliwaagiza watumishi wa Mfuko huo kupita nyumba kwa nyumba, mtaani na sehemu za biashara kuelimisha watu kuhusu bima ili watambue umuhimu wa kujiunga na vifurushi hivyo, huku watoa huduma za afya ngazi zote kuwa na ubinadamu kwa wagonjwa wakati wakuwapatia huduma za matibabu.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema asilimia 34 ya Watanzania ndio wapo katika mfumo wa bima ya afya, na kwamba lengo la mfuko huo ni kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya matibabu kupitia mfumo huo, hivyo wamejikita katika kutoa taarifa na hamasa ili wanachama wapate huduma bora za matibabu na zenye unafuu na zinazopatikana kwa haraka kupitia vituo hivyo vilivyosajiliwa na mfuko huo.

"Kwa kuwa dhamira kubwa ya mfuko ni kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa ndani ya huduma za NHIF, tumekuwa tukiweka mipango mbalimbali ili kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na fursa ya kujiunga na huduma, makundi ambayo yamefikiwa mpaka sasa na huduma ni watumishi wa umma, sekta binafsi, wanafunzi, watoto chini ya umriwa miaka 18, wajasiriamali na wakulima kupitia mpango wa ushirika afya," alisema Konga.

Alisema mfuko umefanyia kazi na kubuni taratibu ambazo zitawezesha wananchi kujiunga kulingana na mahitaji yao ikiwamo kuwezesha mtu mmoja mmoja kujiunga, hivyo kupitia mpango huo kila mwananchi atakuwa na fursa yakuangalia ni huduma gani anataka na atajiunga nazo na kuwa na uhakika wa kupata matibabu wakati wote.

# Waomba kukopeshwa vifaa kisasa vya kuchimbia madini

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WACHIMBAJI wadogo wa mgodi wa Pamoja Mining Gold Rush uliopo kijiji cha Wisolele, Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala Mkoa wa Shinyanga, wameioma serikali kuangalia namna ya kuwakopesha vifaa vya kisasa vya uchimbaji wa madini.

Pia wameomba serikali kuharakisha ugawaji wa leseni za uchimbaji ili waweze kumilikishwa maeneo yao ya uchimbaji wa madini kabla hawajajitokeza watu wengine na kuanza kudai kuwa ni maeneo yao.

Aidha, walisema kuwa kupatikana kwa leseni kutawawezesha kuwa wawekezaji wa kati kama ilivyo kwa kampuni nyingine za uwekazaji na kufanya shughuli zao kwa uhuru bila kubungudhiwa.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa mgodi huo, Hamisi Mabubu, wakati akizungumza na wanahabari, huku akisema wachimbaji wadogo wanaweza kuwa wawekezaji wakubwa iwapo serikali itawasaidia zana za kisasa za uchimbaji.

Alisema wachimbaji wadogo wamekuwa wakitumia nguvu nyingi katika shughuli za uchimbaji wa madini, na wamekuwa wakipata madini kidogo kulinganisha na nguvu waliyotumia, na ni kwa sababu ya kukosekana kwa zana za kisasa za uchimbaji.

"Sisi wachimbaji tumekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunatekeleza suala la ulipaji kodi ya serikali licha ya kwamba hatuna vifaa vya kisasa vya uchimbaji...kwa kidogo tunachokipata tunahakikisha tunatekeleza suala la maendeleo kwa wananchi wanaotuzunguka hasa kwenye sekta ya afya, maji na barabara," alisema.

Elivis Jonas, mhitimu wa chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), aliwataka vijana waliohitimu elimu ya juu kuachana na dhana potofu ya kuendelea kusubiri ajira kutoka serikalini, badala yake wajiajiri katika shughuli za uchimbaji wa madini.

Pia alisema wanatakiwa kutumia fursa ya uwapo wa migodi midogo kufanyakazi kwa kujituma ili kunyanyua uchumi wao, huku akisisitiza serikali kutoa leseni kwa wachimbaji wadogo ili kuepuka kuvamiwa na wawekezaji wenye mitaji mikubwa.



Ofisa wa Jeshi la Polisi nchini, ASP Fatuma Mtalimbo, akitoa mada kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa wafanyakazi wa kiwanda cha TBL Ilala, wakati wa semina iliyoandaliwa na kampuni na kufanyika kiwandani hapo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sikonge kutumia 40% ya mapato miradi ya maendeleo

**Na Tiganya Vincent, TABORA**

BARAZA la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora wamepitisha mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya zaidi ya Sh. bilioni 22 kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha, kuhusu likisema lengo ni kutumia asilimia 40 katika miradi ya maendeleo.

Hatua hiyo imefikiwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani la Sikonge la kujadili na kupitia mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21.

Akiwasilisha mapendekezo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Martha Luleka, alisema makusanyo na matumizi ya mwaka ujao wa fedha yatatokana na ruzuku ya Serikali Kuu Sh. bilioni 19, mapato ya halmashauri Sh. bilioni 2 na asasi isiyo ya kiserikali Sh. milioni 542.

Luleka alisema pamoja na makisio ya makusanyo na matumizi katika mwaka ujao wa fedha, halmashauri hiyo imepanga kuhakikisha asilimia 40 ya mapato yake ya ndani yanaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na kuanzisha ukanda wa biashara katika eneo la Tulu (Sikonge Business Park).

Alisema vipaumbele vingine katika bajeti ijayo ni kuimarisha usimamizi wa karibu wa miradi ya maendeleo na kuhakikisha asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani yanaenda kwenye vikundi vya wanawake, vijana na walemavu.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Peter Nzalalila, aliwapongeza watendaji kwa maandalizi mazuri ya mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21.

Aliomba serikali kuhakikisha inasaidia fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili waweze kukamilisha iliyobaki kwa ajili ya kuwawekea wananchi mazingira mazuri nao kujiletea maendeleo.

Baraza hilo kwa kauli moja walipitisha mapendekezo ya makisio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21.

# Mbunge akunwa mgogoro kumalizwa

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

MBUNGE wa Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya, amewashukuru wakazi wa vijiji vya Sukuro na Kitiangare, waliomaliza mgogoro kati yao uliodumu zaidi ya miaka 20 wakigombea Kitongoji cha Katikati.

Mgogoro huo ulishasababisha mtafaruku mkubwa kati ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Henry Shekifu na aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Christopher Ole Sendeka mwaka 2010.

Ole Millya akizungumza jana na wakazi wa Kijiji cha Sukuro aliwapongeza wananchi wa vijiji hivyo viwili, kwa kuridhia kwa pamoja na kuachana na mgogoro usiokuwa na tija kwao.

Alisema katika mgogoro huo yeye alikaa pembeni bila kupendelea kijiji chochote, kwani vyote ni vya kwake, hivyo hakupaswa kupendelea kimojawapo na aliwaachia wataalamu wagawe vitongoji kama sheria inavyoelekeza.

"Nawapongeza sana wananchi wa vijiji vya Kitiangare na Sukuro, kwani hali ya amani haikuwapo, lakini sasa mmemaliza mgogoro wenu na kuridhia kwa pamoja kuishi kama ndugu, kwani mlikuwa kijiji kimoja kabla ya kugawanywa," alisema Ole Millya.

Alisema hali ya amani na upendo imerejea kati ya vijiji hivyo kama awali, na wananchi wanasalimiana kwa furaha, wanaelewana na kunywa maji pamoja.

Alisema kupitia mfuko wa jimbo alitoa Sh. milioni sita kwa vikundi vya wanawake wa vijiji vyote viwili na Sh. milioni nne kwa mradi wa maji kijiji cha Sukuro na darasa la shule ya kijiji cha Kitiangare.

Mkazi wa Kijiji cha Sukuro, Lengai Ole Makoo, alipongeza hatua ya kumalizika kwa mgogoro huo usiokuwa na tija uliosababishwa na baadhi ya wanasiasa wa wilaya hiyo.

Ole Makoo alisema Kijiji cha Sukuro kimebakiwa na vitongoji vyake vitano na Kijiji cha Kitiangare kimebaki na vitongoji vyake viwili kama ambavyo kanuni, taratibu na sheria zilivyofuatwa wakati kijiji mama cha Sukuro kilipogawanywa.

"Kijiji cha Sukuro kimebaki na vitongoji vya Katikati, Lembutwa, Lenjani, Mouwara na Lasepa na Kitiangare imebaki na vitongoji vya Loongung na Kitiangare," alisema.

# Shule kinara ufaulu darasa la nne yafagiliwa

**Na Cynthia Mwilolezi, SIMANJIRO**

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula, amewapongeza wanafunzi, walimu, wazazi na walezi wa shule ya awali na msingi ya Glisten katika Mji Mdogo wa Mirerani, kwa kuongoza Mkoa wa Manyara kwa ufaulu wa matokeo ya darasa la nne.

Mhandisi Chaula alisema serikali inatoa pongezi kubwa kwa shule hiyo kuongoza mkoa mzima na kuitangaza Simanjiro kielimu.

Alisema kutokana na ufaulu huo, serikali itampatia zawadi ya cheti cha kutambua mafanikio hayo mmiliki na mkurugenzi wa shule hiyo, Justin Nyari.

Alisema anatambua mafanikio ya shule hiyo kushika nafasi ya kwanza kwa ufaulu mkoani Manyara, zimetokana na jitihada na ushirikiano mkubwa kati ya wanafunzi, walimu na wazazi.

"Hivyo ndiyo vitu vya msingi sana ushirikiano wa wanafunzi, walimu na wazazi au walezi, walikuwa pamoja na kusababisha shule hiyo kushika nafasi ya kwanza kiwilaya na kimkoa," alisema Mhandisi Chaula.

Mmiliki wa shule hiyo, Nyari alisema imeshika nafasi ya kwanza kiwilaya kati ya shule 25, ya kwanza kimkoa kati ya shule 102 na ya 39 kitaifa kati ya shule 3,244 zilizopo nchini.

Alisema wamepanga hivi karibuni kuwafanyia tafrija walimu na wanafunzi wa shule hiyo, ili kuwapa moyo wa kuendelea kupiga hatua kielimu.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Silvanus Tairo, alisema ufaulu wa shule hiyo na wanafunzi wengine umesababisha kiwango cha ufaulu kwa wilaya hiyo kifikie asilimia 89.12.Tairo alipongeza shule hiyo na shule nyingine za wilaya hiyo ambazo kwa namna moja au nyingine zimechangia kiwango cha ufaulu kupanda, lakini alionya wasibweteke badala yake waongeze juhudi zaidi.



Meneja wa Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Arusha, Nina Nchimbi (kulia), akipata maelezo kuhusu teknolojia ya EM.1, ambayo inatumika kwenye kilimo, mifugo na uboreshaji wa mazingira, kwa njia ya asili bila kutumia kemikali, kutoka kwa Meneja Masoko wa Teknolojia hiyo, Janeth Swai, katika mkutano wa wadau wa mimea inayozalisha mbolea kwa njia ya asili jijini Arusha jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Washauriwa kuwahi kliniki kujifungua

**Na Cynthia Mwilolezi, BABATI**

WANAWAKE wilayani Babati mkoani Manyara, wametakiwa kuhudhuria kliniki mapema pindi wanapogundua kuwa ni wajawazito ili kujifungua salama, na kupata watoto wenye afya bora.

Mdau wa Maendeleo, Dk. Juma Muna, aliyasema hayo juzi kwenye Kata ya Magara, katika mwendelezo wa utoaji wa elimu ya afya kwa wananchi bila malipo na upimaji wa baadhi ya magonjwa hasa kisukari, shinikizo la damu na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (HIV).

Dk. Muna alisema wanawake wanapaswa kuhudhuria kliniki mapema ndani ya miezi mitatu ya kwanza ili kujua hali na maendeleo ya ujauzito wake.

Alisema anatakiwa kuhudhuria kliniki angalau mara nne hadi kujifungua kwake na ushauri wa jinsi ya kuutunza ujauzito wake na kufikia kujifungua mtoto salama, lakini kujua dalili za hatari zote juu ya ujauzito alionao.

Alisema faida za mwanamke mjamzito kuhudhuria kliniki ya ujauzito kituo cha afya au zahanati ni kuanza kufanya utambuzi wa ujauzito na hali zao.

"Kufanya uchunguzi wa maradhi mbalimbali yanayoathiri ukuaji wa ujauzito kama ugonjwa wa malaria, kisukari, shinikizo la damu, upungufu wa damu, magonjwa ya zinaa, maambukizi ya HIV na mengine na kuanza tiba mara moja ili kutokuathiri ukuaji wa ujauzito na kuzuia mimba hizo kuharibika," alisema.

Alisema faida nyingine ni mjamzito kupata elimu ya afya hasa mabadiliko ya kimwili kipindi cha ujauzito, kujadili na wenza wao kuhusu muda, mahali na njia ya kujifungua.

Alitoa elimu kwa wanawake wajawazito waliofika Kituo cha Afya Magara juu ya madhara ya kutumia pombe wakati wa ujauzito ambapo moja ya madhara hayo ni kujifungua watoto wenye uzito mdogo.

Madhara mengine ni watoto wenye vichwa vikubwa na watoto wenye mgongo wazi, pamoja na shida mbalimbali zinazowapata wanawake wanaotumia vilevi wakati wa ujauzito wao.

Aliwashauri wanawake wote hasa wajawazito kujikinga na matumizi ya tumbaku na kujikinga na magonjwa ya zinaa kama maambukizi ya VVU ili wawe salama na afya zao na watoto.

Baadhi ya wanawake hao walimshukuru Dk. Muna kwa kufanikisha shughuli hiyo bila malipo na kutoa maombi ya kufanyika mara kwa mara kwani wengi wao wana kipato duni.

Mmoja kati ya wanawake hao, Zaituni Mohamed, alisema Dk. Muna ni mfano wa kuigwa, na kuomba kurudiwa kwa tukio hilo mara nyingi ili wapate elimu ya afya.





# Waziri akunwa ujenzi madarasa

**Na Godfrey Mushi, SIHA**

KASI ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa katika Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, ambavyo vinatarajiwa kumaliza tatizo la wanafunzi wa kidato cha kwanza kuchelewa kuanza masomo 'imemkuna' Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara.

Waitara alieleza kuridhishwa kwake na ujenzi huo, baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Esinyari iliyoko Kata ya Orkolili.

"Niseme tu kwamba nimeridhishwa na ujenzi wa shule hii ya Kata ya Orkolili, kujenga mapema madarasa ya ziada katika Shule ya Sekondari ya Esinyari, kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao (2021) kutasaidia sana kuepuka mahangaiko yanayoweza kujitokeza baada ya mitihani ya darasa la saba mwaka huu.

"Ndiyo kwanza tunaanza mwaka wa 2020, lakini nyinyi mmefikiria mbali kwa kujipanga kwa udahili wa kidato cha kwanza mwaka wa 2021, hii inaonyesha ni kiasi gani mmpejipanga kushirikiana na serikali kuu katika kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu ya juu, baada ya ile ya msingi."

Kutokana na jitihada hizo, Naibu Waziri huyo aliahidi kuwa serikali itafanikisha ujenzi wa madarasa manne kwa ajili ya shule hiyo.

Awali, Mkuu wa Shule hiyo, Siporah alimweleza Naibu Waziri Waitara kuwa uongozi wa shule hiyo ulipokea jumla ya Sh. milioni 46.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili na matundu sita ya vyuo, kupitia mradi wa mpango wa fedha za motisha kutokana na matokeo (EP4R).

"Nguvu za wananchi zilisaidia kupunguza gharama za ujenzi ambapo fedha zilizobakia pamoja na posho ya mwalimu mkuu aliyojitolea zilisaidia katika kumalizia darasa lingine lililokuwa katika hatua ya lenta," alisema na kuongeza nguvu za wananchi zilijumuisha pamoja na michango mingine madawati kwa ajili ya madarasa hayo mapya.

Aidha, Siporah alielezea changamoto ambazo zinaikabili shule hiyo ya msingi ya Mkombozi kuwa ni pamoja na upungufu wa matundu 13 ya vyoo pamoja na ukosefu wa vyuo vya walimu, pamoja upungufu wa madarasa tano.

# Ukosefu dawa wakwamisha chanjo homa ya ini KCMC

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya KCMC, imesitisha chanjo ya homa ya ini kwa muda usiojulikana, huku kukiwa na mahitaji makubwa kwa watu wanaojitokeza kufanyiwa vipimo kabla ya kupatiwa chanjo.

Taarifa za kusitishwa kwake ilithibitishwa jana na Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya KCMC, Gabriel Chisseo.

Katika milango ya kuingilia hospitalini hapo, tangazo hilo linaeleza kuwa: "Lile zoezi la chanjo ya homa ya ini lililokuwa linafanyika GOPD Clinic ya KCMC limesitishwa kwa muda kuanzia Januari 10, mwaka huu, hadi litakapotangazwa tena.

"Ila kwa wale waliokuwa wafike tarehe 12 Januari 2020 kwa ajili ya chanjo, zoezi hilo litafanyika tarehe nyingine watakayotaarifiwa na hakuna madhara ya kiafya yatakayotokana na kuchelewa kwa zoezi hilo."

Juzi, zaidi ya watu 50 waliofika katika hospitali hiyo kuendelea na chanjo hiyo walikwama kupata huduma, baada ya kukutana na tangazo hilo kwenye milango ya kuingilia wagonjwa na watu mbalimbali wanaofika hospitalini hapo.

Akitoa ufafanuzi wa sababu zilizosababisha kusitishwa kwa chanjo hiyo, Chisseo alisema: "Kilichotokea ni kwamba huwa tunapokea dawa za chanjo kutoka kwa wenzetu wenye dhamana ya kupata dawa (Bohari Kuu ya Dawa -MSD), kwa kipindi fulani tumekosa hiyo chanjo.

"Kwa hiyo unapokosa madhara yanakuwa kwa yule mtu ambaye anakuja na yule ambaye ameandikiwa. Kwa mfano waliokosa leo (jana) kuchanjwa ni watu ambao wamekuja baada ya miezi sita. Wamechanja mara ya kwanza, mara ya pili na baada ya miezi sita ndio hao ambao hawajapata chanjo hiyo na ndio imekuwa changamoto."

Alifafanua kuwa: "Lakini ndani ya wiki moja kwa wenzetu ambao wanatupa hizi dawa wametuambia watakuwa wametupatia. Kwa hiyo tumewaambia wagonjwa wetu na wateja wetu kwamba baada ya wiki moja, chanjo hii itatolewa kama kawaida. Bahati nzuri madaktari wetu bingwa wa magonjwa ya ndani, wamesema haina madhara yeyote kukosa kwa wiki moja hii chanjo kwa mtu aliyekuwa ameshachanjwa chanjo mbili."

Kabla ya uongozi wa hospitali hiyo kutoa ufafanuzi huo, baadhi ya watu waliokuwa wakiendelea na chanjo hiyo walilalamikia kukosa huduma wakati tayari wengine walikuwa wameshasafiri kutokea mikoa mbalimbali ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Singida kupata chanjo.

Mkazi wa Mkoa wa Arusha, Abdalah Noah, alieleza masikitiko yake kuhusu kusitishwa kwa huduma hiyo akisema: "Leo (jana) asubuhi nimesafiri kwa gari langu na familia yangu kutoka Mto wa Mbu, Arusha mpaka hapa KCMC kwa ajili ya chanjo ya tatu ya homa ya ini. Nilikuja hapa siku ya homa ya ini duniani nikapata semina na nikapima, Mungu alinisaidia nikakutwa sina maambukizi, lakini nikatakiwa nianze chanjo tukiwa na wenzangu wengi zaidi ya 200.

"Sasa kilichotokea ni kwamba nimepata chanjo mbili na leo tarehe ambayo niliandikiwa (Januari 12) ndiyo siku ya kupata chanjo ya mwisho na nimesubiri kwa miezi minne, lakini baaada ya kufika asubuhi hapa tukakutana na tangazo. Tayari tumeshapata chanjo mbili, umeniwekea vitu ndani ya mwili wangu nasubiri chanjo ya tatu halafu uje useme imeahirishwa, tumetoka mbali hamna mawasiliano, kidogo hicho kitu kimetukwaza."

Naye Anna Mwasha, mkazi wa Masama Mudio, Wilaya ya Hai alisema alifika hospitalini hapo kulingana na tarehe aliyoandikiwa na amefika na kukuta hakuna kinachoendelea.

"Kwa kweli tumekwazika sana, amekuja Mkurugenzi Mtendaji wa KCMC (Dk. Gilleard Massenga) ametoa ufafanuzi na amesema atatupa tarehe nyingine kwa hiyo ndio tunangojea, baada ya kuchukua sasa mawasiliano yetu," alisema Mwasha.

Julai 27 na 28, mwaka jana, wakati wa upimaji wa homa ya ini bure, walijitokeza watu 2,550 na kati ya hao watu 56 waligundulika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo.




Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Gabriel Chisseo (katikati aliyeshika simu na funguo mkononi), akitetea jambo na baadhi ya wananchi hospitalini hapo, mjini Moshi jana, baada ya kufika kuendelea na chanjo ya homa ya ini, lakini wakakwama kutokana na sababu za kiufundi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Watanzania ughaibuni wachangia maendeleo

**Na Godfrey Mushi, SAME**

JUMUIYA ya Watanzania waoishi nje ya nchi (Diaspora), imeanzisha kampeni maalum ya kuisaidia Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro kujenga zahanati za kisasa, shule na kusukuma miradi ya ujenzi wa maji vijijini.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Rosemary Senyamule, maeneo ambayo yameanza kunufaika na mkakati huo ni Hedaru (Hedaru Family), Kihurio (Vumwe vwa Kihurio), Mtii na Makanya.

"Ni kweli hao Diaspora wameshaanza kushiriki kikamilifu kampeni ya Kijiji Changu, Fahari Yangu kupitia vikundi na mtu mmoja mmoja, kama wilaya kampeni hiyo inategemea kuzinduliwa rasmi mwaka huu.

"Nimezungumza nao na wanasema kijiji kikiwa na zahanati nzuri, shule nzuri, maji, uchumi mzuri hata wao itawafanya kila mtu ajivunie. Tayari kampeni hii kwa kila kijiji/kata inaendelea," alisema Senyamule.

Kampeni hiyo ya kuwatumia Watanzania waishio nje ya nchi kushiriki kuchangia maendeleo ya maeneo ya asili walipozaliwa ilianza Desemba 12, 2018.

Alisema wananchi wa Same wanafanya misaragambo (kazi za mikono) kwa bidii, lakini inapohitajika vifaa vya madukani kama saruji, mabati, misumari, ujira wa fundi nakadhalika, ndipo inahitaji ushiriki wa watu hao.

Mmoja wa Watanzania hao kutoka Wilaya ya Same anayeishi Uingereza, Dk. Meleck Mmbaga, akizungumzia mchango wao, alisema: "Sisi kama serikali ikifanya na sisi tukifanya, hakika maendeleo yataenda haraka zaidi. Huduma zikiwa nzuri wadogo zetu, shangazi zetu, wazazi, babu na ndugu zetu watafaidika nazo.

"Tanzania Diaspora wanapenda kuiomba serikali itunge mkono ili kuchangia zaidi utaalamu na fedha. Pia tunaishukuru serikali kwa kukamilisha sera yetu ni matumaini yetu tutazidi kushirikiana ili kufungua fursa zaidi kwa Diaspora kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo na ujuzi walioupata nje," alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 14, 2020
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 18
## Nitumie mbinu ipi kufanikiwa shuleni?

Ukurasa 15



**Aina shule zifanyazo vizuri kidato cha nne bado utata**



## BURIANI
Ukurasa 19
Profesa Kezilahabi: Mkongwe wa Kiswahili aliyeiaga dunia



BUNGE LA WANAFUNZI
# Lazaa mapinduzi ya elimu Mafia kutoka kuchukia, hadi kuipenda

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# SIKU TOFAUTI ZA IGP SIRRO



Alipokabidhiwa jukumu.




Akiwa kazini.




Alipokabidhiwa kuongoza Polisi Afrika Mashariki. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**




Alipokutana na wanafunzi wa kigeni wa upolisi.

## JIELIMISHE

# Nani yuko nyuma ya udanganyaji mitihani?

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya wanafunzi 333, wamefutiwa matokeo ya mitihani ya kujipima ya darasa la nne, kidato cha pili na cha nne ya mwaka jana, baada ya kubainika kufanya udanganyifu kwenye mitihani hiyo.

Miaka yote, hilo hutokea kwa namna tofauti, ingawa ukweli unaangukia mahali hapo.

Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) ndilo lililosema hayo wiki iliyopita, wakati likitangaza matokeo ya kidato cha pili na cha nne na kuelezea udhaifu huo unaofanywa na baadhi ya wanafunzi.

Necta imefuta matokeo huku ikibainisha kuwa 142 kati ya watahiniwa hao ni wa darasa la nne, 29 kidato cha pili na 162 wa kidato cha nne, wanaoumba jumla 333.

Tatizo la udanganyifu kwenye mitihani nchini ni la muda mrefu na limekuwa likijirudia kila mara, licha ya kuwapo kwa njia mbalimbali za kukabuliana nao, lakini limeendelea kujitokeza.

Kwa mfano, mwanzoni mwa mwaka jana Katibu Mtendaji wa Necta, Dk. Charles Msonde, alitoa onyo kwa shule zote na wanafunzi wa kidato cha sita kutojihusisha na udanganyifu katika mtihani wa taifa, uliotarajia kufanyika Mei mwaka huo.

Ni pale alipowatembelea wanafunzi zaidi ya 1000 wa kidato cha sita mkoani Simiyu, waliokuwa kwenye kambi ya kitaaluma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa.

Pamoja hayo, kwa nyakati tofauti matokeo ya watahiniwa wa ngazi mbalimbali yamekuwa yakifutwa baada ya Necta kubaini kuwapo udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wanafunzi katika mitihani.

Wadau wa elimu wakiwamo Haki Elimu, wanasema, hatua zinazochukuliwa na serikali za kufuta matokeo ya wanafunzi wanaobanika kufanya udanganyifu, ni sahihi, wakizingatia Sheria na Kanuni za Mtihani za Mwaka 1984.

Ujumbe wao ni kwamba, sheria hiyo iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2006, inazuia namna yoyote ya udanganyifu katika mitihani na inaagiza kuchukuliwa hatua kama hiyo, kukiwapo ushahidi wa kutosha.

Pamoja na hayo, wanasema kuna haja ya kujiuliza kwamba, watoto hao ndiyo pekee wanastahili kuadhibiwa? Umri wa watoto hawa ni kati ya miaka 12 na 15. Je, wenye umri mdogo kama huu wanaweza kufanya udanganyifu?

Kuna mtazamo unaoibuka kwa umma wadau hao wanaamini kuwa ingawa inawezekana baadhi yao walifanya udanganyifu, lakini wengi wao wanaweza kuwa wameshawishiwa au kusaidiwa kufanya udanganyifu huo.

Katika mazingira hayo, inawezekana jamii inayowazunguka, kuanzia kwa wazazi, walezi na walimu wakawa wanahusika kwenye mchezo huo ambao ni hatari kwa maendeleo yao kielimu.

Hatari yake ni kwamba, udanganyifu huo unaporomosha elimu nchini, kwa vile mwanafunzi anaweza kuchaguliwa kwenda kwenye shule za vipaji na kujikuta ufaulu wake uko chini, kumbe amefika huko kwa udanganyifu.

Kimsingi, siyo vyema kuwapo udanganyifu katika mitihani, kwani ni mtindo unaoporomosha elimu na katika mazingira hayo, wanaandaliwa wasomi wasio na sifa.

Dk. Msonde, anakemea wizi wa mitihani sio sifa njema kwa taifa na umekuwa ukiliporomosha Taifa kielimu. Hivyo, kuwapo wazazi, walezi na walimu wanaojihusisha na vitendo hivyo, watambue wanachangia kuporomosha elimu, la msingi wabadilike.

Hapo kuna wasimamizi wakuu, walimu wakuu, wakuu wa shule na wasaidizi wao wanatakiwa kusimamia kanuni na weledi kwenye masuala ya mitihani, ili kuunga mkono juhudi za serikali kutoa elimu bora kwa jamii na kuinua viwango vya ufaulu kwa wanafunzi.

Ikumbukwe Tanzania inaelekea dunia ya viwanda, hivyo ni muhimu kuandaa wasomi wa kuendesha viwanda hivyo, wanaofaulu kwa njia halali siyo udanganyifu wa aina yoyote.

Jambo kuu, ni wanafunzi waachwe wafanye mtihani, wafaulu kwa akili zao na siyo kutegemea udanganyifu, ambao mwisho wa siku mbele ya safari wanakwama.




Dk. Charles Msonde, Katibu Mtendaji wa Necta, alipozungumza na wanahabari (hawapo pichani). **PICHA: MTANDAO.**

MJADALA

# Aina shule zifanyazo vizuri kidato cha nne bado utata

## • Hakuna lisilowezekana kanuni muhimu

Na Michael Eneza

MATOKEO ya mitihani ya kumaliza sekondari ngazi ya kwanza yametoka juzi na katika nafasi 10 za kwanza, wasichana waliendelea kuongoza, hali ambayo imekuwa labda sasa inakuwa ya kawaida kwa miaka ya karibuni.

Baadhi ya shule zilizofanya vizuri, zilibaki katika nafasi zao. Hapo zinatajwa kuna vinara Marian Girls ya Bagamoyo au Feza Boys, ya Dar es Salaam.

Lakini, jumla kila mwaka kunakuwa na shule mpya zinajitokeza katika 10 bora, angalau moja au mbili. Uwezekano wa baadhi ya shule zilizofanya vizuri miaka iliyopita kurudi baadaye, pia upo.

Bado siyo rahisi kusema ni vigezo gani au viashiria vinavyoweza kuonyesha shule inayoweza kufikia nafasi ya juu katika mitihani, kwani hakuna kianzio cha moja kwa moja au kinachoonekana kila wakati, mtu kuwa mbunifu, ni shule gani zitaongoza.

Kuna wakati, ilidhaniwa seminari ndiyo hasa zina uwezo wa kufaulisha wanafunzi, lakini haitokei hivyo kila mwaka, licha ya kuwa hazikosekani, kwani ziko nyingi na kwa jumla zina viwango vya kuridhisha.

Wakati fulani, hisia zikaelekezwa kwenye shule za binafsi kutokana na wanafunzi wao kupitia mitaala bora ya Kiingereza kuanzia shule ya msingi.

Hiyo nayo ikapita na kukosekana kwa vigezo vya shule kurudia ubora mwaka mmoja hadi mwingine, au kundi fulani la shule kuendelea kushika nafasi za juu katika kumi bora imekuwa kawaida, hali inayoweza kuelezwa kwa njia tofauti kadhaa.



Aina ya madhila ya darasani, yanayozaa hatima kwenye chumba cha mitihani.

### UFAULU UNAPATIKANAJE?

Mojawapo ni ufaulu ambao baadhi ya wachunguzi wanaona ni wa juu kupita kiasi, hali inayoashiria kuwa mitihani inakuwa rahisi kiasi fulani, kuondoa tatizo la kuhojiwa 'kwanini wanafunzi wamefeli mitihani.'

Ufaulu wa shule za sekondari unaendana kwa kiasi fulani na shule za msingi, kwani msingi unaingia katika wastani wa zaidi ya asilimia 95, wakati sekondari unaanzia asilimia 85 kwa wastani. Ni kioja mwanafunzi asifaulu hapo?

Katika mtiririko huo wa ufaulu, kinachoweza kutokea ambacho kimsingi hakitabiriki, ni ulegevu maalum kwa wasomaji au upenyo wa aina fulani katika kutunga, kusimamia au usahihishaji mitihani. Kwa kuwa upande wa pili ni siri, mtazamo unasimama dhidi ya fumbo.

Hapo inaweza ikaangaliwa kimantiki kwamba, vimelea vya bahati vinaweza kujitokeza kwa namna tofauti, lakini bado vipenyo vya bahati vinahitaji wanafunzi wenye vipaji, wanaopata ufundishaji bora huku mitihani yenyewe inakuwa katika kiwango wanachomudu.

Ndipo panatokea mwanafunzi mwenye kumbukumbu ya ziada, hivyo kunakuwapo mikakati inayowezesha shule kufaulu au kufaulisha vizuri wanafunzi wake, pale walimu wanapojituma na hawana malalamiko kwa uongozi wa shule, hata serikali kimaslahi.

Bado kuna mjadala kuhusu aina gani ya misukosuko ya maslahi inayoweza kukwamisha shule kufanya vizuri, ambayo bado haijahimitishwa.

Hapo inagusa maana ya hitilafu za uongozi na mizozo katika shule au inayogusa walimu kwa jumla wasifanye kazi yao vizuri. Kimantiki, itakuwa inagusa shule, kwani itaonekana kupitia ubora wa jumla wa elimu kitaifa, viwango vya kufundisha na mitaala inayooana na uwezo, au ari ya walimu.

### MZIZI MATATIZO

Upande mwingine, matatizo ya jumla hasa ya uongozi, utamaduni, mila na miundombinu katika maeneo tofauti, yanaweza kutoa picha ya wilaya ya zinazofelisha wanafunzi zaidi.

Kuna wakati serikali ilianza kuchukua hatua kuhusu shule zinazoshika mkia, lakini suala hilo likaachwa kwani hakuna sheria inayotaka shule isiwe ya mwisho.

Inakuwa rahisi kutoa majibu ya haraka kuhusu shule kuwa ya mwisho, ila mtu akipewa orodha ya matatizo ya kurekebishwa kufaulisha.

### KUTOKA VIONGOZI

Kuna wakati, aliyekuwa Mkuu wa Wilaya mojawapo mikoani Kagera, aliyegeuka mkali kidogo katika elimu wakati mmoja wilaya yake iliposhika mkia katika mtihani wa darasa la saba kitaifa na kuchukua hatua kali, iliyomletea tatizo kikazi.

Kisa na mkasa wa yote, ilikuwa mtihani na maswali yake 'inakuwaje hili na lile inakuwa vile?'

Ni hivi karibuni mtawala mwenzake, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila 'aliwatakia' vijana walionyang'anywa simu, halafu inadaiwa wakalipiza kisasi kwa kuchoma mabweni. Nako alitandaza viboko 'vya uhakika' kwa vijana hao kumtia aibu.

Hakuna takwimu ya nini kilitokea baada ya hapo, lakini inawezekana mbinu za 'mitulinga' kama hizo kuna maeneo zikawa na tija angalau.

Kinachotokea katika miaka ya karibuni, kuongeza ufaulu au hasa viwango vya elimu katika shule za msingi na sekondari, ni kurunzi ya kumulika vyeti feki na ajira za kusaidiana, au kuwepo wafanyakazi hewa katika sekta hiyo.

Ni mazingira yanayoongeza mzigo wa mishahara inayodakwa na watu wachache wanaochukua mishahara ya ziada na hivyo kukwamisha ununuzi wa vifaa, ujenzi wa shule, uharaka wa kulipa mahitaji au madai ya walimu. Inawaongezea walimu ari ya kusoma na kufaulu. Bado hata hivyo, inaonekana uongozi wa shule katika ngazi au kundi lolote, ndiyo sababu kubwa zaidi ya kufanya vyema, kwani mazingira ya kufundisha yanapokaa sawa uwezekano unaongezeka wa kuvitambua au kuvijenga vipaji vilivyopo shuleni.

Lengo la msingi ni kufaulu hapo shuleni na mara nyingine bila kutazamia, vipaji hivyo vinawika katika mitihani ya kitaifa unakuta shule moja inatoa wanafunzi wawili au zaidi nafasi 10 za juu.

Siyo jambo linaloweza kupangwa katika ngazi yoyote ile au hata kutazamiwa, lakini yakiwapo mazingira ya kujituma katika kufundisha na ari ya wanafunzi ya kusoma wakiamini, wanaweza na wanasaidiwa ipasavyo na walimu wao, 'hakuna lisilowezekana.'

Profesa Joyce Ndalichako, ni mtaalmu wa mitaala, aliyewahi kuwa Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA), ni uwanja wake na timu yake kutafakari ulingo wa maboresho wa eneo lake kikazi na kitaaluma.



Wanafunzi wakiwa katika chumba cha mtihani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

ELIMU

## BUNGE LA WANAFUNZI

# Lazaa mapinduzi ya elimu Mafia kutoka kuchukia, hadi kuipenda

- Mabinti 'wa kuolewa' hadi 'wa kufaulu'
- Wawa wanaharakati kufika hadi kwa DC
- Wafunguka 'madudu' yaliyojiri nyumbani
- Shule yaweka rekodi ya wote wamefaulu



Mratibu wa Mradi kutoka shirika lisilo la kiserikali la ActionAid Tanzania, Samwel Mesiak, akiwapongeza wanafunzi wa Shule ya Msingi Kilindoni, kwa kuleta mabadiliko chanya kitaaluma na kuwasaidia wazazi.

**Na Beatrice Philemon**

UNAPOZUNGUMZIA Bunge la Wanafunzi Shuleni, si wanafunzi au walimu wote katika shule za msingi nchini wanafahamu nini maana yake?

Kimsingi, ni chombo kilichoanzishwa na wanafunzi kwa kushirikiana na Shirika lisilokuwa la kiserikali la ActionAid Tanzania, lengo ni kuwasilisha kero wanazokutana nazo shuleni au katika jamii wanayotoka.

Imegeuka kuwa chombo pekee kisiwani Mafia, hususan katika Shule ya Msingi Kilindoni, ambako ujumbe unaokusudiwa umeifikia jamii bila kikwazo chochote sasa.

**MWALIMU MKUU**

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilindoni, Steven Mlobi, anasema limewasaidia kuibua vitendo viovu wanavyofanyiwa majumbani, mfano kubakwa, kulawitiwa ndoa za utotoni, kunyimwa mahitaji muhimu ya shule na mabinti kufanyishwa kazi nyingi.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kilindoni, ambayo ni kioo cha mageuzi ya mafanikio Mafia.

Pia imesaidia kuwaibua watoto wenzao wanaotazwa kwenda shule, ili kubaki katika shughuli ndogo.

Mwalimu Mlobi, anasema imesaidia kuamsha na kubaini upungufu katika ufundishaji shuleni, akiwekewa sanduku la maoni shuleni huku wakiwa na nafasi ya kujadiliana kuhusu taaluma, pia wanapatikana viongozi kukutana na uongozi wa shule kueleza kero katika masomo au ufundishaji wa walimu.

"Kupitia mkutano wao pamoja na uongozi wa shule, inakuwa rahisi hata kuwabadilishia mwalimu wa somo ambaye wanafunzi hawamwelewi wakati akifundisha," anasema.

Pia anasema ni bunge linalosaidia vijana kuwa wabunifu zaidi na kuwajengea uwezo kuendelea kujiamini katika kujieleza, hivyo hata kwenye mitihani wanapata uwezo mzuri kujieleza masomoni.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mlobi, inasaidia kuongeza ari ya wanafunzi kujifunza na kuwafanya waendelee kuhudhuria shule kila siku (utoro unatoweka), lila mwanafunzi anatamani kuingia bungeni sasa.

**MATOKEO CHANYA**

Katika mafanikio yake Shule ya Msingi Kilindoni, mkoani Pwani, Mwalimu Mlobi, anasema limeleta mabadiliko makubwa kwa wanafunzi na wazazi.

Anasema, kwa sasa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kiko juu, jamii imehamasika na wazazi wameanza kuhudhuria vikao vya wazazi shuleni, jambo ambalo huko nyuma walifika hatua mahudhurio 'sifuri' mkutano wa wazazi.

Kingine, Mwalimu Mlobi anataja kwamba watoto wamejua haki zao na jinsi ya kuzipata tofauti na miaka ya nyuma, huku idadi ya ufaulu imeongezeka baada ya wazazi kuanza kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto na maendeleo yao shuleni.

Anarejea zamani, wazazi hawakutaka kushiriki vikao shuleni, lakini kupitia matamasha yaliyoandaliwa na wadau ikiwamo serikali na wanafunzi kupata fursa ya kuelimisha, jamii imebadilika kuhusu dhana ya unyanyasaji ulikuwapo.

Mwalimu Mlobi, anatoa mfano kuna wakati hata walipoitisha kikao mauhudhuria ni kati ya 40 na 70 katika kundi la wazazi 400 shuleni, idadi ambayo ni ndogo sana.

"Sisi kama uongozi wa shule tunashukuru Shirika la ActionAid Tanzania kuanzisha mabunge ya wanafunzi katika Wilaya ya Mafia ikiwamo shule yangu, kwa sababu limetusaidia katika suala zima la taaluma, ukianza na watoto wenyewe.

"Zamani walikuwa hawafanyi vizuri kabisa katika masomo yao lakini kupitia mabunge haya, hivi sasa watoto wanafaulu vizuri katika masomo yao, wengi wamejua haki zao za msingi na pia kuzidai," anasema.

**WATOTO WAFUNGUKA**

Inaelezwa, baadhi ya watoto walipoona wazazi hawaeleweki, waliamua kwenda kwa Mkuu wa Wilaya na Ofisa Maendeleo kuwashtaki kwa kunyimwa ya msingi nyumbani na baadaye vongozi hao walichukua hatua stahili na haki zinapatikana sasa shuleni na nyumbani.

"Kabla ya kuanzisha Bunge la Wanafunzi shuleni kwetu, kuna wazazi walikuwa hawanunui hata 'unifomu' kwa ajili ya watoto wao.

"Walikuwa wanasoma katika mazingira magumu sana, tunashukuru mabunge haya yameleta mwamko mzuri," anasema Mwalimu Mlobi.

Kupitia bunge la wanafunzi, watoto wanaibua changamoto zinazowakabili nyumbani na na kisha yanawekwa kwenye sanduku la maoni shuleni na kuzipatia suluhisho.

**TAALUMA KILINDONI**

Mwalimu Mlobi anataja takwimu za maendeleo ya taaluma katika Shule ya Msingi Kilindoni, kwamba mwaka jana, jumla ya wanafunzi 52 walifanya Mtihani wa Taifa wa darasa la saba, kati ya wanafunzi 52 sawa na asilimia 100 walifaulu, wavulana na wasichana 27.

Akitaja mwaka 2018, wanafunzi 54, kati ya hao, 53 sawa na asilimia 98 walichaguliwa kujiunga na sekondari (wasichana 26, wavulana 27).

Mwalimu Mlobi anasema, kiwilaya ilishika nafasi ya kwanza kati ya shule 34 zilizofanya mtihani darasa la saba, huku katika mkoa Pwani Kilindoni kilishika nafasi ya 11 kati ya shule 251 zilizofanya mtihani kitaifa.

Anasema, mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 52 pia walifanya mtihani wa darasa la saba, kati ya hao, wanafunzi 51 sawa na asilimia 98 walichaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari (wavulana 21 na wasichana 30).

Anasema mwaka 2016, wanafunzi 50 walifanya mtihani wa darasa la saba na 37 sawa na asilimia 74 walichaguliwa kujiunga na sekondari (wavulana 19 na wasichana 18) na katika ngazi ya wilaya ilishika nafasi ya pili kati ya shule 34

Mwalimu Mkuu anataja mwaka 2015, wanafunzi 42 walifanya na kati yao 41 walichaguliwa kujiunga na sekondari, wasichana walikuwa 18.

**HAKI ZA JINSIA**

Mwalimu MlobI anasema, hivi sasa hali ya unyanyasaji kijinsia imepungua kwa asilimia 95, watoto wa kike wanasoma na wanapata muda kujsomea, tofauti na nyuma walitakiwa kufanya kazi za nyumbani na kusubiri kuolewa.

"Hapo awali siku za wikiendi watoto wa kike walikuwa hawaruhusiwi kuja shuleni kusoma, lakini siku hizi wanakuja, mwamko mkubwa zaidi na pia hivi sasa wazazi wanafuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni." Anasema.

Miaka ya nyuma hakuna mzazi aliyekuwa anakuja shuleni kufuatilia maendeleo ya mtoto wake, mtoto asome, asisome hawana mpango kabisa.

"Kupitia mabunge haya tumeweza kujua changamoto zetu, kuboresha elimu yetu na pia maendeleo ya shule kwa ujumla kutokana na ushirikiano wa wazazi tulioanza kupata," anasema.

**MWANAFUNZI**

Mwanafunzi kutoka Shule ya Msingi Kilindoni, Sada Khatibu, anakiri Bunge la Wanafunzi limewasaidia kujua mambo mbalimbali yahusuyo haki zao na, utafutaji wake.

**Inaendelea Uk. 19**




Sada Hatibu, mwanafunzi wa darasa sita katika Shule ya Msingi Kilindoni, akielezea jinsi Bunge la Wanafunzi lilivyowasaidia nyumbani na shuleni. **PICHA ZOTE: BEATRICE PHILEMON.**

---

HAKI UWAJIBIKAJI NA VITA YA RUSHWA

# TUKATAE KUTAPELIWA 2020



Simu nyenzo ya matapeli. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

Suala la utapeli wa kimtandao unaendelea kukua kwa kasi ya ajabu.

Cha kujiuliza ni je inakuwaje wengi wetu tunaamini watu tusiowafahamu kiasi kwamba tunaishia kutapeliwa ?

Naomba nitoe mfano ambao wengi ikiwemo baadhi yenu wasomaji mtakuwa mmekumbana nalo. Kuna genge la wahalifu ambao hupiga simu kwa wanaolenga kuwatapeli na kuwaaminisha kwamba wameshinda tuzo fulani la donge nono.

Matapeli hawa wanajiamini kiasi kwamba wanafanya utafiti wao vizuri. Waliponipigia walitoa taarifa ndefu ya jinsi tunavyofahamiana, pamoja na kutaja majina ya rafiki zangu waliodai kwamba wanawafahamu.

Utaratibu wao waliojiwekea ni kumuaminisha wanayemlenga kwamba ni watu wa karibu ambao hamjaona na au mmepoteza na kwa muda mrefu. Ole wako unapoendelea kuwasikiliza ndipo wanapotumia fursa hiyo kushindilia msumari la uaminifu ili kukuondoa kwenyesha kwa lolote na kukuamninisha ni watu wema.

Siri hiyo uambatana na hulka ya mlengwa mwenyewe. Mfano mimi niliambiwa jinsi mzungu anahitaji bidhaa hizo Dar es Salaam na kwamba lengo lilikuwa wafanikishe kuyatoa kigoma , mi ni yalipie na kisa binafsi nilipe dola 25,000 yatakapopokelewa na mzungu.

Waliandaa mazingira ya mzungu kunipigia na kusema binfasi hawaamini wale jamaa ila ametaarifiwa taasisi nililokuwa nafanyia kazi (analitaja) na akaona kwamba binafsi siwezi kuwatapeli nikiwa muajiriwa wa taasisi ile.

Baadhi ya tahadhari unayohitaji ni kutazama ni jinsi matapeli hawa hutumia namba nyingi tofauti kuwasiliana na wanayemlenga.

Hili nalo ni jambo jema kwamba laini za simu ambazo hazijasajiliwa zitafungiwa suku chache zijazo kuanzia leo maana matapeli hawa wametumia mwanya huu wa laini zisijosajiliwa kutapeli.

Jambo lingine la msingi ni kwamba matapeli nao wamesoma na hutumia muda mwingi kusoma saikolojia ya yeyote Yule wanayelenga kumtapeli. Manaeno yanayotumika ni ya kutia moyo. Wanataja hela kubwa ambayo wengi hushindwa kuzuia mapigo ya moyo.

Ukweli usiopingika ni kwamba usemi wa lugha ya kingereza unahusu 'When the deal is too good think twice' tafsiri yake isiyo rasmi, ukiona ofa unayopewa ni nzuri kuliko maelezo, tafakari. Mara nyingi tunashindwa kuuliza maswali ya kawaida tu.Inakuwaje ni mechaguliwa mimi? Wakati mwingine shindano lenyewe linalodaiwau meshinda wala hujashiriki. Swali la msingi je nitakuwaje mshindi wa milioni 200 za mtandao fulani wa simu wakati hujashirikiwa kujiunga na shindano lenyewe.

Kinachosababisha kukithiri na kufanikiwa kwa utapeli ni tamaa. Tamaa za kupata hela kwa njia isiyo rasmi na isiyokuwa na utoaji jasho ndiyo husababishawa tu kutapeliwa .Kwa hali ya kawaida uzalishaji wa hela unategemea kazi na jasho. Hiki kinachotokana na kuaminishwa kuna fedha za haraka ndio utapeli wenyewe.

Wengine wameibuka na mfumo wa kupeleka meseji zinazosema tuma zile hela kwenye namba hii, namba yangu ya kawaida ina matatizo. Hili nalo ajabu wameweza kutapeli nalo watu. Ni ajabu kwa sababu iweje yeyote yule aibuke na kutuma hela kwenye namba yoyote fedha ambazo umezifanyia kazi na kuzitolea jasho?

Mwaka 2020 tukatae kutapeliwa. Hatua ya kwanza kukataa kutapeliwa ni kutoendekeza tamaa ya hela rahisi. Hicho kitu hakipo kwamba kuna namna ya kutajirika kwa fedha za haraka. Ukikataa kuendekeza ya fedha za haraka zisizokuwa na utoaji jasho, umeshachukua hatua ya kukataa utapeli na hivyo basi umewajibika.

- **Kwa maoni: baruapepesamawatiarts@yahoo.com**

JE, WAJUA?



Mwanafunzi akijisomea. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Nitumie mbinu ipi kufanikiwa shuleni?

MTU unaposoma na umenaswa katika msitu mkubwa na hujui njia ya kutokea, mwangaza wa jua hauonekani kwa sababu ya wingi wa miti. Ili kutoka humo, ni lazima ajitengenezee njia kukata vichaka hivyo kwa upanga.

Huenda wengine wakalinganisha maisha yao shuleni na hali inayotajwa juu. Unakuwa kama mfungwa darasani mchana kutwa, na usiku una migawo mingi ya shule hivi kwamba huna wakati wa kufanya mambo mengine. Je, ndivyo unavyohisi? Katika nafasi iliyo hapa chini andika somo unaloliona kuwa gumu zaidi.

Huenda wazazi na walimu wako wamekusihi uongeze bidii katika somo hilo. Ikiwa ndivyo, si kwamba wanataka uwe na maisha magumu, bali wanataka ufanikiwe maishani. Hivyo, tengeneza njia itakayokuwezesha kutoka katika msitu huo. Ni vifaa gani hivyo?

●Si rahisi kufanya vizuri shuleni ikiwa una maoni mabaya kuhusu masomo. Jaribu kuelewa mambo yote yanayohusika. Mtu anayelima anapaswa kulima akiwa na tumaini.

Kama ilivyo kazi ya kulima, mwanzoni usione faida ya masomo fulani, kwa sababu huenda mambo fulani mnayosoma yasionekane kuwa yenye faida kwa sasa. Hata hivyo, kujifunza masomo mengi kutapanua maarifa yako katika dunia vyovyote vile, utaboresha uwezo wako kufikiri, ustadi utakusaidia siku za baadaye.

●Maoni yanayofaa kuhusu uwezo wako; shule inaweza kufunua vipaji vyako. Hata kipawa anacho Mungu, kinahitaji kuhusishwa ili kisipotee bure. Shule inaweza kukusaidia kugundua na kukuza vipawa ambavyo hukujua unavyo.

Usikate tamaa eti kwa sababu unadhani kwamba huwezi kufanya vyema shuleni. Unapoanza kuwa na maoni yasiyofaa kuhusu uwezo wako, badili mtazamo wako na kujitahidi kuwa na maoni yanayofaa.

Una vipawa gani? Ikiwa unadhani hujui, kwa nini usimuulize mtu unayemtumainia? Rafiki kama huyo anaweza kukusaidia kutambua vipawa vyako na kuvitumia kwa njia bora.


●Mazoea mazuri kusoma njia ya mkato ya kupata mafanikio shuleni, upende usipende, lazima usome. Huenda hata hupendi kusikia neno hilo, hata hivyo ukweli masomo yana faida. Ukitia bidii hata kidogo tu, unaweza kufurahia masomo yako.

Ili uwe na mazoea mazuri ya kusoma, unahitaji kupanga wakati wako. Kumbuka kwamba kusudi la kwenda shuleni ni kusoma. Kwa hiyo, kama vijana wengi, huenda ungependa kutenga wakati fulani kwa ajili ya tafrija.

- Msaada wa kutimiza majukumu shuleni; Namna gani ukilemewa na majukumu shule?
- Ondoa Vizuizi; Fikiria mfano uliotolewa mwanzoni mwa sura hii. Ukijikuta katikati ya msitu mkubwa na hujui njia ya kutokea, unahitaji kifaa kinachofaa, kama vile, upanga wa kufyeka njia.

Ndivyo ilivyo pia kuhusu shule. Badala ya kuhisi kwamba umeelemewa na wazazi na walimu wako, tumia vifaa vitatu vilivyozungumziwa katika sura hii ili ufanikiwe shuleni. Kadiri unavyofanya maendeleo, utafurahi kwamba ulitumia vifaa hivyo.

***Kwa mujibu wa taarifa za mtandao***



Mwanafunzi akiwa maktaba ya shule.

# AL SHABAB WAUA WALIMU 3 KENYA

- Wamteka mmoja
- Wakata mtandao



Shule na jengo jingine lililoathiriwa . **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Garissa, KENYA**

NI shambulio la kigaidi liliyoishia walimu watatu kuuawa, baada ya wanaoshukiwa kuwa wanamgambo wa Al Shabab kuvamia mji wa Garissa, Kaskazini mwa Kenya katika mpaka wa nchi hiyo na Somalia.

Walimu hao watatu wakazi wa eneo hilo walipigwa risasi hadi kufa, huku kituo cha polisi kikichomwa moto na mfumo wa mawasiliano kuharibiwa katika eneo la Kamuthe, asubuhi ya jana.

Taarifa zinasema, baada ya shambulizi hilo, wanamgambo hao waliondoka na mwalimu na shirika la habari la redio linasema:"Muuguzi wa kike alinusurika shambulio hilo, kwa sababu ya jinsia yake kabla wavamizi hawajakwenda kuharibu mnara wa mawasiliano."

Washambuliaji hao, pia wameharibu mnara wa mawasiliano uliopo mahali hapo, kabla ya kutoweka na maofisa wa polisi wanafuatilia wavamizi huo, huku kukiwepo ripoti za kiusalama zinazoonyesha kwamba wavamizi wameweka milipuko ardhini katika barabara za eneo hilo.

Ni aina ya shambulizi, linaloifanya Kenya kuwa katika tahadhari baada ya kupata taarifa za kijasusi kwamba kundi la Al Shabab linapanga kufanya mashambulio zaidi.

Wiki iliyopita, Uingereza imetoa onyo kwa raia wake wanaotaka kusafiri nchini humo dhidi ya kutembelea Kaunti ya Garissa na katika eneo la ndani ya kilomita 60 katika mpaka wa Kenya na Somalia.

Hadi sasa imeshafika shambulizi la 11 kutekelezwa na kundi la Al Shabab nchini Kenya katika kipindi cha wiki sita. Mashambulizi manne yalitekelezwa kaunti za Garissa, matatu katika eneo la Wajir, Mandera na Lamu mashambulizi mawili kila moja.



# LAZAA MAPINDUZI YA ELIMU MAFIA KUTOKA KUCHUKIA, HADI KUIPENDA

Inatoka Uk. 17

Anafafanua: “Pia watoto kutosikilizwa. Watoto wa kike hawasikilizwi, kwa mfano tukienda nyumbani unakuta wa kike anapigwa, tukienda kusema hasikilizwi.”

“Awali mzazi mwingine alikuwa anamwambia mtoto wake wa kike akifika darasa la saba ajifelishe ili aende kuolewa na wazazi wengine walikuwa wanaambia watoto wao waende kwenye boti kuombao au kuchukua mshipi waende kuvua samaki kwa ajili ya matumizi ya nyumbani,” anasema.

Anataja changamoto nyingine, wanafunzi wanaotoka sehemu za mbali kusikokuwepo usafiri, baadhi walikosa vipindi darasani au kukutana na watu wanaowarubuni kuingia katika ngono.

Khalfan Khatibu, anasema kuhusu mimba za utotoni wazazi wengi hawazijui haki za mtoto, akimpeleka katika biashara hadi usiku, weakikutana na vishawishi vya mimba.

**ILIKOTOKEA SHULE MFANO**

Anasema, Shule ya Kilindoni, anasema kuwa shule ilianzishwa mwaka 1967, mpaka sasa ina wanafunzi 478, kati yao 242 wavulana na 236 wasichana na jumla ya walimu 13; wanaume sita na wanawake saba.

Mwalimu Mlobi anasema, mpaka sasa shule ina jumla ya tundu nane za vyoo, nyumba nne za walimu ambazo ni chakavu na madawati 155.

“Hivi sasa bado tunahitaji tundu nneza vyoo, walimu wawili wa somo la kingereza na sayansi, madawati 70 ikiwamo nyumba 15 za walimu kwa sababu nyumba nne zilizojengwa mwaka 1975 hazitoshi na zimechakaa sana.

“Pia tunahitaji vitabu vya Kiswahili darasa la tatu, hisabati kwa sababu vitabu tunavyopata kutoka wizarani havitoshelezi,” anasema Mwalimu Mkuu Mlobi.

BURIANI

# Profesa Kezilahabi: Mkongwe wa Kiswahili aliyeiaga dunia

• Mtunzi Rosa Mistika, Dunia Uwanja Fujo...

**Na Michael Eneza**

BINGWA wa Kiswahili aliyegeuka kiongozi wa kisiasa, Profesa Euphrase Kezilahabi hayupo nasi tena, akiaga dunia miezi mitatu kabla ya kufikisha umri wa miaka 77 hapo Aprili 13.

Kwa wanaojua, wana tarehe inayofanana na ya kuzaliwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, tofauti yao ni miaka ya vifo.

Akiwa anatofautiana na wenzake wengi katika klabu ya waandishi wa riwaya au hadithi, Hayati Kezilahabi alikuwa msomi aliyefundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kwingineko.

Kote alikokuwa kati ya wale wenye mvuto wa kipekee zaidi kati ya waandishi wa riwaya. Alichangia sana katika kutoa tafsiri na tathmini za fasihi barani Afrika na akeanda mbali katika uchangiaji ujenzi wa fasihi kwa riwaya, kazi zake zikisomwa hapa nchini na kwingineko.

Kuingia kwake katika siasa hapakuwapo kishindo sana kuhimili cha taaluma. Zaidi, atakumbukwa kuwa mmoja wa wabunge wa upinzani walioiona kazi nzuri anayoifanya Rais Dk. John Magufuli na kuunga mkono angalau kwa hisia ya maendeleo kutokuwa na vyama.

Anakiri hivyo, akimkaribisha au kutoa salamu, wakati Rais Dk. Magufuli alipotembelea jimbo lake katika mojawapo ya ziara zake mikoani mwaka jana.

Ni kwa njia hiyo, pia alifahamika hasa katika kipindi cha ujana wake Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakati huo ikiwa inafukuta kwa mikondo tofauti ya kiharakati na kiitikadi, lakini alifahamika kwa utunzi, siyo harakati.



Marehemu Profesa Euphrase Kezilahabi. **PICHA: MAKTABA**

**SAFARI YAKE**

Maisha ya Prof. Kezilahabi, yanaelezwa alizaliwa Aprili 13, mwaka 1944, huko wilayani na katika taaluma alipasishwa kuwa Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Botswana, Idara ya Lugha za Kiafrika.

Historia yake inagusa kwamba aliandika kazi zake kitalauma kwa Kiswahili na ameshatoa machapisho ya kitaaluma katika fani ya fasihi, iwe ni kwa kazi za Kiswahili au nyinginezo barani Afrika.

Mojawapo, inatajwa kuwa ni ‘Mkanganyiko wa Maudhui katika Kiswahili cha Kisasa’ (Aesthetic Ambivalence in Modern Swahili) na “Dhana ya Shujaa katika Riwaya za Kiafrika” (The Concept of Hero in African Literature).

Ni kazi aliyoungana na mhakiki fasihi mwingine ambaye si mwandishi sana wa riwaya za Kiswahili, Profesa Fikeni Senkoro katika uchambuzi wa ‘Kahaba katika Fasihi ya Kiafrika.’

Kazi moja iliyofahamika sana ni ‘Dunia Uwanja wa Fujo’ iliyochapishwa mwaka 1985 na mshangao wa baadhi ya wakongwe, kazi ya ujana wake iitwayo ‘Rosa Mistika’ ambayo katika chapisho la awali ilipigwa marufuku.

Baadhi yetu awali katika miaka ya 1970 mwanzoni, tulikuta imepigwa marufuku, baadhi yetu tunakumbuka wakati tunaingia shule za sekondari tulikuta tangazo ubaoni ikisomwa: “Rosa Mistika ni marufuku shuleni.”

Ina maana kazi hiyo ilipata ahueni wakati wa chapisho, hata ikaanza kusomwa tena kwa mapana, zama utandawazi ulipoingia, awamu ya pili. Hiyo ilikuwa mwishoni mwa 1988.

Ina maana kuwa mwandishi huyo mkongwe alikuwa na utundu katika sanaa ya uandishi. Kimsingi, jamii zinapokuwa katika mawasiliano na uchumi, zinakuwa huru zaidi na kutupilia mbali mazingira ya kiimla yenye lengo la kuhakikisha utamaduni na maadili, vinalindwa.

> Mojawapo, inatajwa kuwa ni ‘Mkanganyiko wa Maudhui katika Kiswahili cha Kisasa’ (Aesthetic Ambivalence in Modern Swahili) na “Dhana ya Shujaa katika Riwaya za Kiafrika” (The Concept of Hero in African Literature).

Kuna wadadisi wa fasihi ya Afrika nchi za nje waliokusanya kazi zake na kuchagua baadhi ya mashairi yake kutoa kitabu wakilishi wa mtiririko wa hisia zake kama mshairi.

**UMAHIRI KAZINI**

Mwaka 2015 kuna andiko liliitwa ‘Stray Truths’ yaani kweli zilizoko nje ya mstari, ambazo kuzitaja inahitaji utundu au uthubutu kwa kiwango fulani.

Ziko tungo kadhaa za Hayati Kezilahabi zilichapishwa katika miaka ya 1980 na ile ya 1990, kwa mfano ‘Karibu Ndani’ (1988); ‘Nagona’ (1990); na ‘Mzingile’ (1991).

Chapisho la baadhi ya mashairi yake kuwa kitabu wakilishi cha kazi zake lilitolewa na taasisi ya kutafsiri mashairi ya tamaduni tofauti, yenye wachangiaji kutoka nchi kadhaa za Ulaya kama Uingereza na Ufaransa.

Kuna maeneo ambako kazi za Hayati Kezilahabi zilihusishwa katika chapisho la kitabu mtandaoni. Hakuna uhakika kama mjadala ni wa hapa nchini au Bara Afrika, ambako inawezekana wanaofundisha fasihi na hasa lugha za Kiafrika, wanapata tabu kuziainisha.

Kazi moja ya fasihi na zile za lugha au fasihi kongwe kama Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu, licha ya kuwa Kiarabu kimegawanyika vipande kadhaa.

Hata hivyo, unaweza kupata picha sahihi zaidi ya mjadala huo ukitoka katika fasihi ya Kiswahili ambayo ina mapana ya kutosha kuwa fasihi, kulinganisha na lugha nyingine za Kiafrika, mfano Kisomali, Kiganda, Kizulu, Kikikuyu ambacho anakiandikia mkongwe Profesa Ngugi wa Thiong’o.





# WADAU SABATO KASIKA

## Uandikishaji wa watoto wa darasa la kwanza kwa mwaka huu, ulikumbwa na changamoto kufuatia baadhi yao kuandikishwa, kwa kukosa vyeti vya kuzaliwa. Wadau wanasemaje?



**JOSEPH JANDWA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

UANDIKISHAJI wa watoto kuanza darasa la kwanza ni zoezi la kila mwaka, kwa maana hiyo siyo geni, hivyo tusiwaadhibu watoto kwa kuwazuia kuanza shule kwa sababu kucheleweshwa kwa vyeti, si makosa yao bali ya wazazi na watendaji wa serikali. Suala la vyeti vya kuzaliwa lina utata mkubwa, katika baadhi ya maeneo hasa ya vijiji na baadhi ya maeneo ya mijini. Vijijini kinamama wengi hujifungulia kwa wakunga wa jadi au kwa zahanati na vituo vya afya vya karibu yao. Wanachoambulia ama ni karatasi (tangazo) la kuzaliwa kwa mtoto. Kimbembe huja pale kinapohitajika cheti cha kuzaliwa. Hiki cheti hiki hutolewa na msajili wa Vizazi na Vifo (RITA), ambaye kwa maeneo mengi ya nchi ofisi zake ziko ndani ya ofisi za wakuu wa wilaya. Kuna maeneo mtu kufika wilayani huhitaji kusafiri saa au kilomita kadhaa kuifikia ofisi husika. Linapo kuja suala la nauli za kwenda huko wilayani hasa kwa sisi wa vijijini jumlisha gharama nyingine za kuwapo huko mjini, husababisha kuona ni adhabu kufuatilia cheti cha kuzaliwa. Kwa hiyo watendaji wa vijiji au maofisa maendeleo ya jamii, katika kata au vijiji wapewe mamlaka ya kutoa vyeti hivyo kwa watu wa maeneo kama hayo niliyotolea mfano. Hiyo itapunguza kwa kiasi kikubwa urasimu wa kusafiria vyeti mijini. Jambo lingine, Rita wasiishie kutoa vyeti tu, watoe na elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuwa na cheti cha kuzaliwa na namna ya kukipata. Tena hiyo elimu inapashwa kutolewa hasa wakati ule kinamama wajawazito wanapokuwa wanaenda kwenye kliniki. Na ikiwezekana cheti kitolewe siku hiyo hiyo aliyozaliwa mtoto badala ya kuwa na tangazo kwanza. Vinginevyo hatuwatendei haki watoto wetu kwa kutowaandikisha shule kisa eti hana cheti cha kuzaliwa.




**STEPHEN KOROKONI (MCHUNGAJI WA ANGLIKAN, MUGUMU)**

NI kweli kuandikisha watoto wadogo kuingia darasa la saba kumekuwa na changamoto za vyeti vya kuzaliwa, mimi nafikiri elimu itolewe kwa jamii kuwaelemisha wazazi, wajue umuhimu wa vyeti vya kuzaliwa ili muda unapofika wa kuandikisha watoto kusiwepo na usumbufu wowote, pia ifanywe sensa kila mtaa, ili kubaini watoto, ambao hawana vyeti vya kuzaliwa wapewe na unapofika muda wa kuandikishwa kusiwapo na usumbufu. Kwa kweli mimi ningependa sana kuwajengea watoto uzalendo kutoka mwanzo kuliko walipokuwa wanaenda kidato cha tano na sita, kwa hali hii mtoto akitoka shule ya msingi amekamilika na cheti cha kuzaliwa tangu darasa la kwanza, madarasa ya juu hakuna usumbufu, hivyo mimi kama kiongozi wa dini, ninaona hatua ya kila mtoto kuwa na cheti cha kuzaliwa kuanzia darasa la kwanza ni nzuri sana. Lakini changamoto hizi zilizojitokeza zitafutiwe ufumbuzi. Pia kukipata cheti lazima mzazi awe na kadi ya kliniki. Lakini ukiangalia, wapo wazazi wanaozalia nje na vituo vya afya kupata kadi ya kliniki huwa kazi kubwa, hivyo serikali iweke mkazo katika kuhimiza wazazi kwenda vituo vya afya kujifungua, ili kupata kadi za kliniki ambazo kimsingi zinasaidia kupata kiurahisi cheti cha kuzaliwa. Hatua hii itapunguza changamoto katika zoezi la kuandikisha watoto kwa kutumia vyeti vya kuzaliwa. Lakini ikumbukwe kuwa suala hili la kutumia vyeti vya kuzaliwa shuleni ni jema na linajenga uzalendo kwa watoto. Pamoja na hayo, walimu wawe wanatoa taarifa mapema kuhusu vitu vinavyohitajika wakati wa uandikishaji wa watoto, ili kuondoa usumbufu kama huo uliojitokeza.



**MAGESA NATHANAEL (MWANASHERIA, MKAZI WA BAGAMOYO)**

VYETI vya kuzaliwa ni muhimu kwa kila mtoto, ili kuwa na kumbukumbu zake sahihi, na huondoa udanganyifu shuleni ambao umekuwa ukijitokeza hasa kuhusu umri, kwani katika mazingira hayo husababisha iwe rahisi kwa baadhi ya watoto wanaoacha shule majina yao kuchukuliwa na wengine wanaorudia shule. Na mrudiaji akishafaulu na kuendelea mbele inamlazimu awe na cheti cha kuzaliwa chenye jina husika. Kwa upande mwingine utoaji wa vyeti vya kuzaliwa bado haujawekewa utaratibu mzuri kuwawezesha wazazi vijijini kuweza kupata vyeti kwa urahisi mara mtoto anapozaliwa, bali anatakiwa kufuatilia katika ofisi za Rita zilizopo Bomani, na elimu kwa wazazi na jamii kuhusu umuhimu wa cheti cha kuzaliwa bado ilikuwa haijatolewa hasa vijijini. Kwa ujumla elimu inatakiwa kutolewa na utaratibu mzuri kuwekwa angalau maofisa wa Rita wawe wanashuka kwenye ngazi za kata hata kwa ratiba maalum, ili kuhamasisha wazazi na jamii. Lakini niipongeze serikali kwa uamuzi wake wa kupiga marufuku mwanafunzi kuzuiliwa kuandikishwa darasa la kwanza kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa. Muda uliowekwa na serikali kwa wazazi kuendelea na mchakato wa kuwatafutia watoto wao vyeti uendelee wakati wakiwa shuleni. Uamuzi huo ni mzuri unalenga kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wanapata elimu. Jambo la msingi ni kila mzazi kutambua kuwa cheti ya kuzaliwa ni cha muhimu sana kwa kila mtoto. Hivyo kila mmoja afuatilie na kuhakikisha anakipata.



**MAUA KINGAZI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

HAPA nyumbani kwetu nasi tumekumbana na tatizo hilo ambalo kwa kweli lilituchanganya. Kuna mtoto wa marehemu kaka yangu alikataliwa kuandikishwa darasa la kwanza kwa sababu ya kukosa cheti cha kuzaliwa. Hii inatokana na kwamba mama yake alipoteza tangazo, hivyo ikawa vigumu kukipata. Lakini pamoja nayo mbona miaka ya nyuma watoto walikuwa wakiandikishwa kwa kutumia kadi za kliniki? Utaratibu huo ulikuwa hauna usumbufu kama ambao umejitokeza kwa watoto walioandikishwa ili kuanza darasa la kwanza mwaka huu. Ila uamuzi uliofanywa na Waziri Jafo ni mzuri na umesaidia wengi ambao walikuwa wamekwama kupeleka watoto wao, kwa sababu ya kukosa vyeti wakati kadi za kliniki za watoto zipo. Ushauri wangu kwenye suala hili ni kwamba uandaliwe utaratibu, ambao hautakuwa na usumbufu katika kupata vyeti ili Watanzania waweze kuvipata kirahisi. Ninasema hivyo kwa sababu inawezekana miezi, ambayo Waziri Jafo ameweka inaweza kutumia, huku baadhi ya wazazi wakiwa bado hawajavipata kutokana na mlolongo mrefu uliopo. Pamoja na hayo, watu wa vijijini wasogezewe huduma hiyo kwenye maeneo yao, kwani wengi wa watu, ambao hawana vyeti vya kuzaliwa kutokana na hali halisi kwamba huduma hiyo haipo hadi mtu aisafirie umbali mrefu na kama hana uwezo kifedha, basi anajikuta akikaa bila mtoto wake kuwa na cheti cha kuzaliwa. Siyo vibaya huduma hiyo vya vyeti vya kuzaliwa ikapatikana hata katika ngazi ya kata kuliko ilivyo sasa.



**SWALEHE ATIK (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NIONAVYO ni kwamba suala hili la ukosefu wa vyeti kwa baadhi ya watoto, limechangiwa na mambo mawili. Kwanza upatikanaji wa vyeti ulivyo mgumu kwa sababu ya mizunguko mingi ya kupitia hadi kuvipata na pia uzembe wetu Watanzania wa kutozingatia mambo yakiwamo ya muhimu kama vyeti vya kuzaliwa. Kila upande ukitimiza wajibu wake inavyotakiwa, hakutakuwa na tatizo la baadhi ya watoto kutokuwa na vyeti. Uzembe unasababisha baadhi ya wazazi kutoona umuhimu wa mtoto kuwa ma cheti, eti kwa sababu tu yeye kama mzazi hana na anaendelea kufanya shughuli zake bila usumbufu, lakini ukweli unabaki palepale kuwa cheti cha kuzaliwa ni cha muhimu kwa kila Mtanzania. Ili kuondoa tatizo hili kwa mwaka ujao, ni vyema huduma za kupata vyeti zirahisishwe zaidi na kupatikana zaidi maeneo ya vijijini ambako ninaamini kuna tatizo kubwa la kuvipata. Kwanza wapo wasioona umuhimu wake, wengine kwa uzembe wao tu hawavifuatilii na pia wapo ambao wanakwama kusafiri umbali mrefu kufuatilia vyeti kwa sababu za kiuchumi. Hebu hayo yote yatazamwe kwa kina na kuyapatia ufumbuzi na ikiwezekana, elimu pia itolewe kwa wale wasioona umuhimu wa watoto wao kuwa na vyeti vya kuzaliwa ili watambue umuhimu huo kwamba kila mtoto wa Kitanzania anatakiwa awe na cheti cha kuzaliwa na akipate bila usumbufu kama ilivyo sasa, ambapo inawezekana wengine wamevikosa kwa sababu ya usumbufu au uzembe wao wenyewe wa kutozingatia mambo ya muhimu kama hayo.





## Wachangamkia kilimo cha alizeti

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wakulima wa alizeti katika Mkoa wa Mbeya, wameanza kuchangamkia fursa ya kuzalisha zao hilo kwa madai kuwa gharama zake za uzalishaji ni ndogo kuliko kipato kinachopatikana.

Wakizungumza na Nipashe juzi katika Bonde la Songwe wilayani Mbeya, wakulima hao walisema awali walikuwa hawalipi kipaombele zao hilo kutokana na kwamba hawakujua tija yake.

Mmoja wa wakulima hao, George Simchinga, alisema alikuwa analima zao hilo kwa kuzungusha kwenye mashamba ya mahindi, lakini kwa sasa ameanza kulima zao hilo kwa kulitenganisha na mazao mengine.

Alisema baadhi ya taasisi za serikali na zisizo za serikali zimekuwa zikiwatembelea na kuwapatia elimu ya kilimo bora cha zao hilo na hivyo wamehamasika kuanza kuzalisha zao hilo ili kujiongezea kipato.

"Kampuni zinazozalisha na kuzalisha mbegu za alizeti zimekuwa zikitutembelea na kutupatia elimu ya kilimo bora cha zao hili, lakini kuna taasisi zimekuwa zikutukusanya kwenye vikundi na kutuhamasisha wakiwamo Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV)," alisema Simchinga.

Alisema kwa sasa amelima ekari nne kwa mara ya kwanza katika historia ya maisha yake, na kwamba ameambiwa na wataalamu kuwa akifuata vizuri masharti atapata kipato ambacho kitamfanya aachane na mazao mengine.

**"Kampuni zinazozalisha na kuzalisha mbegu za alizeti zimekuwa zikitutembelea na kutupatia elimu ya kilimo bora cha zao hili, lakini kuna taasisi zimekuwa zikutukusanya kwenye vikundi na kutuhamasisha wakiwamo Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV)," alisema Simchinga.**

# Chanzo mgogoro wa kanisa chafichuliwa

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TIMU iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuchunguza mgogoro uliokuwa unafukuta ndani ya Kanisa la Uwinjilisti mkoani humo na kuhatarisha amani, imebaini kuwa chanzo ni ufisadi wa fedha uliofanywa na viongozi wa juu wa kanisa.

Chalamila aliunda timu hiyo mwishoni mwa Desemba mwaka jana baada ya baadhi ya viongozi wa kanisa hilo kudaiwa kutaka kutwangana makonde kwa sababu ya kutuhumiana kwa matumizi mabaya ya madaraka na kuibua tatizo la ubaguzi wa rangi kati ya Waafrika na wazungu.

Mkurugenzi wa miradi wa kanisa hilo, Tito Nduka na Mwenyekiti Lazaro Halinga, walikuwa wanatuhumiwa na Mshauri wa Kanisa, Markus Lehner (mzungu), ambaye ndiye mwanzilishi wa kanisa hilo kuwa wanatumia vibaya fedha za kanisa, huku na wao wakimtaka aondoke kwa madai kuwa hawataki kuongozwa na mzungu.

Akiwasilisha ripoti ya timu hiyo kwenye Mkutano wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanisa hilo, Mwenyekiti wa Tume hiyo, Hasan Mkwawa, alisema fedha ambazo hazijulikani matumizi yake ni zaidi ya Sh. milioni 689.

Mkwawa ambaye ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, alisema fedha hizo zilikuwa zinachukuliwa na Mwenyekiti, Halinga na Mkurugenzi wa Miradi Nduka kwa njia mbalimbali ikiwamo kutumiwa na wahasibu kwa njia ya simu na kusaini hundi, lakini hakuna vielelezo vinavyoonyesha matumizi yake.

Alisema miradi ambayo ya fedha viongozi hao wamefisadi fedha ni katika Shule ya Sun Rise, chuo cha wahudumu wa afya, kwenye karakana na nyumba za kupangisha ambazo zinamilikiwa na kanisa hilo.

"Tume imebaini kuwa chanzo cha ugomvi wa viongozi hawa sio ubaguzi wa rangi kama ilivyokuwa inadaiwa, bali ni matumizi mabaya ya fedha za kanisa ambao ulikuwa unafanywa na mkurugenzi na mwenyekiti, tumefuatilia baadhi ya maeneo na kujiridhisha," alisema Mkwawa na kuongeza.

"Kwenye miradi michache ambayo tumepitia tumebaini fedha hizo zaidi ya milioni 689 hazina vielelezo vya matumizi, lakini ukifanyika ukaguzi kina fedha hizo zinaweza kufika hata zaidi ya bilioni moja, tulimhoji mwasibu baada ya kuona miamala ya simu akasema alikuwa anaambiwa atume lakini hakuambiwa matumizi," aliongeza.

Aliongeza kuwa tume hiyo ilibaini kuwa viongozi hao hawakupeleka zaidi ya Sh. milioni 88 za watumishi kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) licha ya kukata fedha hizo kwenye mishahara ya watumishi hao.

Hata hivyo alisema tume hiyo ilibaini kuwa viongozi hao waliuza gari la kanisa bila kufuata utaratibu, na kwamba kwa sasa liche ya gari hilo kumilikiwa na mtu binafsi, lakini bado kwenye mifumo linaonekana kama ni mali ya kanisa.

Vilevile Mkwawa alisema tume hiyo ilibaini kuwa Mkurugenzi wa Miradi, Nduka alichukua mkopo binafsi benki lakini dhamana ya mkopo huo, aliweka majengo ya Shule ya Sun Rise ambayo ni mali ya kanisa na kwamba kanisa hilo ndilo linalipa mkopo huo.

Baada ya tume hiyo kuwasilisha taarifa hiyo, Chalamila aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Jeshi la Polisi kuendelea na taratibu zingine ikiwemo kuchunguza mali za viongozi hao pamoja na kuwachukua hatua.

Alisema serikali ina mamlaka ya kusimamia mali za kanisa lolote na kwamba ndio maana Hospitali ya Ifisi ambayo inamilikiwa na kanisa hilo la uwinjilisti inatumika kama Hospitali ya Wilaya ya Mbeya na hivyo akasisitiza kuwa hatua lazima zichukuliwe.

"Tume imeshauri viongozi hawa wachunguzwe zaidi, sasa hili ni la kwenu Takukuru na Jeshi la Polisi, matumizi hayo mabaya ya fedha yanaonyesha kuwa viongozi hawa wanataka kuua miradi ya kanisa na serikali haiko tayari kushuhudia kitu hicho," alisema Chalamila.

Awali Mshauri wa Kanisa hilo, Lehner alieleza kuwa viongozi hao walikata miti ya kanisa hilo iliyokuwa katika Wilaya za Mbozi mkoani Songwe na Wilaya ya Mbeya lakini kanisa halikuambulia chochote.



Wananchi wa Kata ya Utengule - Usongwe katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, wakishirikiana kusomba mchanga wakati wa ujenzi wa vyumba vya madarasa tisa katika Shule ya Sekondari Usongwe, wikiendi, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa vyumba hivyo uliosababisha wanafunzi 400 wa kidato cha kwanza wakose nafasi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mpango waja udhibiti ukuaji makazi holela

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa utaratibu wa kushirikiana na halmashauri za miji, majiji yote nchini kudhibiti ukuaji holela wa makazi katika maeneo hayo kwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Hayo yalisemwa jijini Mbeya mwishoni mwa wiki na mtaalamu wa Mipango Miji kutoka katika wizara hiyo, Paulo Kitosi, wakati wa mkutano wa kupitia rasimu ya kwanza ya mpango kabambe wa jiji la Mbeya.

Alisema serikali imeamua kuanzisha utaratibu huo baada ya kubaini kuwa miji mingi nchini inakuwa bila kuwa na mpangilio mzuri wa makazi ya pamoja na shughuli mbalimbali za kijamii.

Kitosi alisema mbali na wizara hiyo kushirikiana na halmashauri, pia itashirikiana na wadau wengine wa maendeleo ambao nao watakuwa wanatoa maoni yao juu ya mpangilio wa miji hiyo.

"Utaratibu huo utakuwa unaainisha maeneo ya makazi ya wananchi, sehemu za huduma za jamii kama shule vituo vya kutolea huduma za afya na sehemu za kufanyia biashara, hii itasaidia miji yetu kukua vizuri," alisema Kitosi.

Alisisitiza kuwa utaratibu huo pia utasaidia kupunguza migogoro ya ardhi inayoibuka mara kwa mara kwenye miji hiyo kutokana na makazi ya wananchi kuingiliana na shughuli zingine za kijamii ikiwamo kuvamia maeneo ya wazi.

Akiwasilisha rasimu ya kwanza ya mpango kabambe wa Jiji la Mbeya, mwakilishi wa Kampuni ya Urban Solution lTD ambayo ndiyo imepewa kandarasi ya kuandaa mpango huo, Willy Kitorika, aliitaka serikali kukaa na wananchi na kuwaelimisha umuhimu wa kuendeleza ardhi yao.

Alisema moja kati ya vitu ambavyo wananchi wanatakiwa kuelimishwa wanapotaka kuendeleza maeneo yao ni kufuata sheria za nchi ikiwemo kuwa na hati miliki ya maeneo wanayotaka kuyaendeleza pamoja na kupata vibali vya kuendeleza kutoka serikalini.

"Serikali lazima iwaelimishe wananchi utaratibu wa kuendeleza ardhi yao, waendeleze kulingana na mipango ya serikali sio kila mtu anajikatia viwanja vyake jinsi anavyotaka yeye, ni kweli ardhi ni ya kwao lakini lazima wafuate mipango ya serikali," alisema Kitorika.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Gerard Luzika, alisema utekelezaji wa mpango huo kabambe utakwenda sambamba na mipango mingine iliyopo kwa mujibu wa sheria.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema kwenda kinyume na mpango huo kabambe ni kuendelea kuharibu taswira ya Jiji na akawataka wanasiasa wa Jiji la Mbeya kuwa mstari wa mbele kulinda mpango huo.





# Mahenge awapa kibarua wahandisi wa Dodoma

**Renatha Msungu, DODOMA**

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewaagiza wahandisi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutafuta ufumbuzi wa mfumo wa majitaka ili kuondokana na tatizo la baadhi ya nyumba kuzingirwa na maji wakati wa msimu wa mvua.

Alitoa agizo hilo jana baada ya wakazi wa eneo la Mnyakongo, Kata ya Nkuhungu kuomba msaada wa kutengenezewa makaravati, ili kuondoa kero ya kujaa maji katika baadhi ya nyumba kipindi hiki cha mvua.

Dk. Mahenge alisema ifikapo Februari mwaka huu, wahandisi hao wanapaswa kuwa wameimarisha mifumo hiyo jijini hapa.

"Wananchi wanaishi kwa wasiwasi hasa katika msimu huu wa mvua inayoendelea kunyesha, nawaomba wahandisi mnaohusika na suala hili, lifanyieni kazi haraka iwezekanavyo ili wakazi wa maeneo haya waishi kwa amani," aliagiza.

Awali, wananchi hao walimweleza Mkuu wa Mkoa huyo kuwa wanahitaji msaada wa kuwekewa makaravati yatakayopitisha maji kwa kuwa nyumba zao zinazingirwa na maji.

Fidelis Tarimo, mkazi wa eneo hilo, alisema maji hayo yamekuwa yakizingira nyumba na kuingia ndani kutokana na kukosekana kwa mifereji ya kupitishia maji kwenye barabara za mitaa.

"Hili tatizo limekuwa kubwa kwa sababu ya ujenzi wa barabara kubwa ya Singida unasababisha maji kukosa uelekeo na kuelekea kwenye makazi yetu, hili ni tatizo linatusumbua sana, tunaishi bila amani na kwa tahadhari pale mvua inapoanza kunyesha," alilalamika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mnyakongo, Hekta Matonya, alisema kero hiyo inasababisha wananchi kuchelewa kwenda kwenye majukumu yao ya kujiingizia kipato.

Akizungumzia hali hiyo, Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Dodoma, Lusako Kilembe, alisema tatizo hilo linasababishwa na baadhi ya njia za maji kuzibwa na baadhi ya nyumba zinazojengwa maeneo hayo.

Alisema watalazimika kuvunja baadhi ya miundombinu ili kunusuru watu wasiathirike na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

## Wataka vituo maalum usajili laini kwa vidole

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

ZIKIWA zimebaki siku sita kabla ya kufungwa kwa usajili wa laini za simu kwa alama za vidole, watoa huduma za simu za mkononi wameomba kuanzishwa kwa vituo maalum kwa ajili ya kutoa vitambulisho vya taifa na kusajili laini za simu, ili kuwapunguzia usumbufu wananchi ambao bado hawajasajili.

Meneja wa Vodacom Tanzania Kanda ya Kati, Andrew Temu, alitoa rai hiyo alipokutana na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi mwisho wa wiki katika ofisi za kanda hiyo kuangalia hali ya usajili huo.

Alishauri kutengwa kwa eneo moja la kutolea huduma za vitambulisho na watoa huduma wengine ili kuwapunguzia wananchi usumbufu wanaofika kupata huduma hiyo.

"Kwa sasa, mkuu utakuta mwananchi anachukua fomu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), anapeleka kwa mtendaji, akitoka huko anapeleka Uhamiaji na mwisho anarudia tena Nida, hii inasababisha wengi kukata tamaa na mizunguko hiyo," alilalamika.

Alisema uwapo wa kituo kimoja utawasaidia wananchi kupata huduma zote eneo moja ili kukimbizana na muda uliobakia wa kusajili laini za simu kwa njia hiyo.

Alisema katika eneo hilo inatakiwa ziwapo kampuni zote zinazotoa huduma za simu ili kumrahisishia mwananchi huyo akipata namba ya Nida, anasajili laini zake hapo hapo.

"Pia, wanatakiwa wawapo watu wa Uhamiaji na Nida ili kupunguza mzunguko wa kutafuta huduma hizi kwa kuwafuata ofisini kwao," alishauri.

Alidai baadhi ya wanafunzi vyuo vikuu wameshindwa kukamilisha taarifa zao kutokana na wengi kutokea mikoani, akimaanisha si wakazi wa Mkoa wa Dodoma.

"Tuna vituo vyetu saba pale Udom, lakini tatizo kubwa ni hilo, wengi hawana vitambulisho vya Nida na wakienda Nida, wanadaiwa taarifa za mahali walipotoka na hivyo mpaka sasa, hawajasajili laini zao," alilalamika.

Kutokana na maelezo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma (Katambi), aliahidi kuwasiliana na mamlaka husika ili kuanzisha kituo hicho kabla ya kufungwa kwa usajili huo Januari 20 mwaka huu.

"Ni wazo zuri, ndiyo maana mimi nipo hapa kupata maoni ya jinsi ya kuwasaidia wananchi wetu kupata huduma, ikiwezekana tutaifanya ndani ya wiki hii," aliahidi.

Alisema siku zilizobakia ni chache na uongozi wa wilaya unatafuta namna ya kuwasaidia wananchi ambao bado hawajasajili laini zao za simu kwa alama za vidole.

"Tunaangalia eneo nzuri ikiwezekana pale Nyerere Square, tutaandaa miundombinu rafiki kwa watoa huduma ili wananchi wapunguze mizunguko ya kupata vitambulisho na namba za Nida," aliahidi.

Alisema mizunguko hiyo imekuwa ikiwapa shida wananchi hasa wanaotoka maeneo ya vijijini kwenda mjini kupata huduma ya vitambulisho na wakati mwingine kuangukia kwa matapeli kutokana na kutoyajua vyema baadhi ya maeneo ya kutolea huduma ya vitambulisho.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiandika maandishi ya kuzuia ujenzi wa nyumba iliyokuwa ikijengwa bila kibali eneo la Ndachi, Kata ya Mnadani, jijini Dodoma, juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## Wakulima wa zabibu walilia soko

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKULIMA wa zao la zabibu mkoani Dodoma wamesema ukosefu wa soko la uhakika ni tatizo linalochangia kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Wakizungumza na Nipashe jana, wakulima hao walidai wanalazimika kuuza zabibu kwa hasara huku zingine zikioza shambani.

Mohamed Mwiru, mmoja wa wakulima hao, alidai kukosekana kwa viwanda vya kutosha vya kusindika zabibu, kumechangia wakulima kukosa soko la kuuza zabibu zao.


"Wakulima wana mwamko mkubwa wa kulima zabibu, lakini viwanda vya kutosha havipo, vilivyopo vinachukua zabibu kidogo kulingana na mahitaji yao na zinazobaki tunajikuta tunauza kwa hasara, zingine zinaozea shambani," alilalamika.

Alishauri serikali kushawishi wawekezaji wengi kuwekeza kwenye viwanda vya juisi ya zabibu, akiamini ni njia ya kusaidia kutatua tatizo la uhaba wa masoko.

"Hii itasaidia kujua wapi tupeleke, kuna wanunuzi wanatengeneza pombe, hivyo wawekezaji pia wa juisi wanahitajika," alisema.

Sista Bether Mafimbo alidai: "Hakuna soko kamili la wapi tuuze zabibu pale zinapoiva, zabibu si sawa na machungwa au mahindi, kwa kuwa zabibu zinapoiva ndani ya wiki mbili, wiki ya tatu zitaanza kukauka kama hakuna mvua."

Mmoja wa wafanyabiashara wadogo wa zao hilo, Merian Kisoma, alisema kwa sasa biashara si nzuri kutokana na kukosa wanunuzi.



# Z'bar yanyooshea kidole wahisani wasio wema

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidhi, amesema serikali haipo tayari kupokea misaada ya wafadhili na wahisani wasiokuwa na nia njema na Zanzibar.

Kiongozi huyo aliyasema hayo hivi karibuni alipotembelea Shule ya Mkombozi iliyopo Welezo Mjini Unguja.

Alisema malengo ya Mapinduzi ya mwaka 1964 ni kuwaletea maendeleo wananchi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo elimu.

Hafidhi alisema baadhi ya wahisani na wafadhili wanaosaidia maendeleo hayo wanaingiza maslahi yao binafsi jambo ambalo ni kinyume na Mapinduzi hayo.

Alieleza kuwa serikali inathamini juhudi zinazochukuliwa na wadau wa maendeleo, lakini hakuna budi kuzingatia misingi na masharti yaliowekwa kwa faida ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa waziri huyo, katika kunyanyua sekta ya elimu katika Jimbo la Welezo viongozi wanatarajia kujenga shule ya ghorofa katika shehia ya Mtofaani ambapo tayari wameanza harakati za kutafuta wafadhili wa ujenzi.

Kwa upande wake, Msaidizi Katibu Mkuu wa Taasisi ya Rafiki Elimu, Saidi Shaame Khamis, alisema wamebaini katika Wilaya ya Magharibi A na B Unguja kuna idadi kubwa ya wanafunzi jambo ambalo limepelekea kusaidia kujenga madarasa katika baadhi ya shule na kupunguza msongamano.

Aidha, alisema hatua hiyo ni kuunga mkono serikali katika maendeleo ya elimu ili kuwa na matokeo mazuri ya wanafunzi katika mitihani ya taifa.

Waziri huyo aliwataka wazazi kuwa na ushirikiano wa karibu na walimu ili kufuatilia mwenendo wa masomo wa watoto wao kwa maendeleo endelevu kitaaluma.

"Wapo baadhi ya wanafunzi wanatoka majumbani kwao wanakwenda shule lakini shule huwa hawafiki na wazazi wala hawana taarifa yoyote na hawafuatilii," alisema.



Waziri asiye na Wizara Maalum, Juma Ali Khatib (kulia), akimkabidhi cheti cha shukrani aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Abdalla Mwinyi, ambaye alitoa eneo la kiwanja chake kuruhusu ujenzi wa hospitali ya kujifungulia Kiboje Mkwajuni Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wanaume 17 wayakimbia makazi yao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KITENDO cha MKUU wa Wilaya ya Micheweni Kisiwani Pemba kuwataja hadharani wanaume 17 wanaowafanyia vitendo vya udhalilishaji watoto wameyahama makazi yao katika wilaya hiyo.

Mkuu wa wilaya huyo, Salama Mabarouk, aliwataja wanaume hao baada ya kukithiri kwa vitendo hivyo wilayani humo, jambo ambalo lilifurahiwa na wananchi wengi.

Wakizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni baadhi ya wananchi walisema kuwa wanaunga mkono juhudi za mkuu wa wilaya huyo kuwataja hadharani watuhumiwa hao.

"Tunaiomba serikali ichukuwe hatua kali kwa wale wote wenye viashiria vya matendo ya udhalilishaji kwa sababu wanavitia doa wilaya yetu," alisema Ali Mabrouk.

Aidha, aliishauri serikali kutoa adhabu kali kwa washtakiwa wa matendo hayo ili kuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia hiyo kuweza kuacha.

"Tunapendekeza adhabu kwa wabakaji ianzie miaka 50 jela badala ya kufungwa miaka mitano au saba kwa kuwa haichukui muda wanarejea mtaani," alisema. Naye Sheha wa Shehia ya Shumba Viamboni wilayani humo, Time Said Omar, alisema baada ya DC huyo kutangaza kuwa kuna matukio hayo bado haijajulikana hatua inayofuata kwa wanaofanya vitendo hivyo.

## Mwinyi ataka bidhaa zenye ubora viwango

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, amewataka wafanyabiashara kuzalisha bidhaa zenye ubora na kuziuza nje ya nchi.

Akizungumza juzi wakati akitembelea maonyesho ya biashara katika viwanja vya Maisara Mjini Unguja, alisema kila mfanyabiashara anawajibu wa kuzalisha bidhaa zenye viwango na ubora unaotakiwa ili waweze kupata soko kwa urahisi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupata fedha za kigeni na kuinua uchumi wa nchi, lakini kuimarika wao wenyewe kutokana na bidhaa zao.

Aidha, aliwataka Wazanzibari hasa vijana kujikita katika kilimo cha mazao ya biashara ambayo ndio njia pekee itakayoweza kuwasaidia katika kujiongezea kipato.

"Mimi hapa licha ya kuwa naonekana nimezeeka, lakini nathamiini sana kilimo na ninalima kwa sababu kilimo ni muhimu kwa maisha ya binadamu," alisema.

Aidha, alieleza kuwa kilimo ndio uti wa mgongo hivyo ni vyema vijana wakajiajiri badala ya kukaa na kutegemea ajira pekee kutoka serikalini.

Rais Mwinyi pia aliwataka Watanzania kuthamini bidhaa zinazozalishwa nchini badala ya kupenda zaidi za kutoka nje ya nchi.

Mwinyi aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuweka utaratibu wa kila mwaka kufanya maonyesho ya biashara kila mwaka katika kipindi cha sherehe za Mapinduzi ambayo yamewakutanisha wafabiashara mbalimbali kutoka Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa upande wao baadhi ya wafanyabiashara katika maonyesho hayo, walisema changamoto kubwa iliyopo ni hali ya hewa ya jua kali katika maeneo hayo hali ambayo inawapa usumbufu mkubwa. Maonyesho hayo yameanza Janaури 2, na yataendelea hadi Januari 15, mwaka huu.

**"Mimi hapa licha ya kuwa naonekana nimezeeka, lakini nathamiini sana kilimo na ninalima kwa sababu kilimo ni muhimu kwa maisha ya binadamu," alisema.**

# Waomba kuongezwa muda usajili simu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WAKAZI wa Mkoa wa Shinyanga, wameomba serikali kuongeza muda wa usajili wa vitambulisho vya Taifa na usajili wa laini za simu mpaka Rais John Magufuli atakapomaliza muda wake wa kipindi cha kwanza Oktoba, mwaka huu.

Ombi hilo lilitolewa jana wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti wakiwa kwenye ofisi za Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) wilayani Kahama, na kusema wapo baadhi ya wananchi walijiandikisha tangu mwaka 2017, lakini mpaka sasa hawajapata namba wa kitambulisho.

Lucas Shija, mmoja wa wananchi hao, alisema kuwa wanaiomba serikali kuongeza muda wa usajili wa vitambulisho vya Taifa na laini za simu mpaka Rais Magufuli atakapomaliza muda wake wa uongozi wa kipindi cha kwanza cha miaka mitano Oktoba mwaka huu, na kudai kuwa muda uliioongezwa wa siku 20 ni mdogo kilinganisha na idadi ya watu.

Alisema wapo waliojiandikisha kupata vitambulisho hivyo tangu mwaka 2017 na kutolewa picha kwenye ofisi za kata, lakini wanapofuatilia namba zao wanaambiwa wakajisajili upya, na hao ndio wengi kulinganisha na wanaomba kwa mara ya kwanza.

Naye Sofia Paulo, alidai ndoa zao zimeanza kuteteleka kutokana na kushinda kwenye ofisi za Nida kwa muda mrefu bila mafanikio ya kupata namba na kusababisha kwenye ndoa kutokuwa na imani hasa mmoja anaporudi usiku kwa kisingizio kuwa alikuwa Nida.

"Wakati tunajaza fomu za Nida pia tunajaza na namba zetu za simu, kwanini wasitutumie namba zetu za Nida kwenye simu zetu, ili tukasajili laini zetu za simu, na kuwaachia nafasi wengine ambao ndio kwanza wanaanza harakati za kujaza fomu na kupata namba?" Alihoji Sofia.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema kuanzia mwaka 2016 hadi Januari Mosi mwaka huu, zaidi ya wananchi 3,013,303 wa Halmashauri za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini wameshasajiliwa katika uandikishaji huo.

Alisema kuwa wapo ambao walikuwa na upungufu katika fomu zao, hivyo zilirudishwa kwa watendaji wa vijiji, kata na mitaa ili kufanyiwa marekebisho, na baadaye zirudishe katika ofisi za Nida kwa ajili ya kuendelea kupatiwa huduma.

"Serikali ilitoa muda wa kutosha kwa wananchi kujiandikisha na kupata vitambulisho vya Taifa, na wengine tuliwafuata hadi kwenye kata zao, lakini kwa kupuuza zoezi hili hawakujitokeza kwa wingi na zimebaki siku chache ndio wanajitokeza na kujazana kwenye ofisi za Nida," alisema Ndanya.



Lami ikiwa imebanduliwa bila ya kufanyiwa ukarabati katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam na kusababisha usumbufu kwa mabasi yanayotumia kituo hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Barabara kuwapa fursa wananchi

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati Zanzibar, Salama Aboud Talib, amewataka makandarasi wa ujenzi wa barabara ya Gombani-Pagali kuikamilisha kwa kiwango cha lami kwa muda uliopangwa, ili wananchi waweze kuitumia.

Amesema hatua hiyo itasaidia kuwarahisishia katika shughuli zao mbalimbali zikiwamo za kiuchumi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kuwafikishia huduma mbalimbali wananchi wake bila ubaguzi ikiwamo huduma ya barabara kwa lengo la kuimarisha uchumi mjini na vijijini kwa kuwa ndio lengo la Mapinduzi ya Zanzibar.

Akiweka jiwe la msingi kwenye barabara ya Gombani-Pagali, Waziri huyo alisema maendeleo hayakufanywa kwa ajili ya watu fulani bali ni kwa ajili ya wananchi wote na ndio dhamira ya mapinduzi ya mwaka 1964.

"Katika kuhakikisha huduma ya barabara zinaimarishwa mjini na vijijini, Serikali kupitia Rais Dk. Ali Mohamed Shein, ilinunua vifaa vya ujenzi va barabara vyenye thamani ya Sh. bilioni 14," alieleza waziri huyo.

Aliipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutekeleza kwa vitendo ilani ya CCM, ambapo huduma mbali mbali zimewafikia wananchi, ikiwamo miundombinu ya barabara, hivyo kuna kila sababu ya kujivunia matunda ya Mapinduzi.

Aidha, aliwataka makandarasi wanaotengeneza barabara hiyo kuwa waaminifu na kujenga kwa kiwango kinachohitajika ili idumu kwa muda mrefu sambamba na kuwataka kuvitumia vizuri vifaa vya kutengenezea barabara, ili vitumike kwa muda mrefu.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Rashid Hadid Rashid, alisema wamefurahia sana kuona barabara hiyo imewekewa jiwe la msingi, na kusema kuwa ushauri waliopewa na waziri wataufanyia kazi katika kuhakikisha wanafanikisha, ili maendeleo yazidi kukua.

Alimpongeza Dk. Shein kwa hatua anazozichukua za kujenga barabara zenye kiwango cha lami katika wilaya hiyo, hatua ambayo inawapa faraja.

"Kabla ya Mapinduzi tulikuwa na barabara mbili tu, ya Chake-Mkoani na Chake-Wete, lakini kwa sasa mpaka vijijini kuna barabara, tunashkuru sana na tunajivunia matunda ya Mapinduzi," alisema.

Katibu Mkuu, Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Juma Nyasa Juma, alisema ujenzi wa barabara hiyo ni mradi unaolenga kuleta maendeleo kiuchumi.

Alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 1.8 upana na urefu mita saba itagharimu Sh. 2,171,874,075, ambapo mkandarasi wa ujenzi huo ameshalipwa Sh. 325,781,011.

Wakazi wa Gombani walisema uwapo wa barabara hiyo utawarahisishia katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.

# Mil. 800/- kujenga machinjio Kibaha

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha, mkoani Pwani, inajenga machinjio ya kisasa kwa gharama ya Sh. 804,309,600 ambayo itakuwa na uwezo wa kuchinja zaidi ya ng'ombe 100 kwa siku.

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 halmashauri hiyo, ilitenga kiasi cha Sh. 945,059,000 kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa awamu ya kwanza.

Hayo yamebainishwa jana mjini hapa na Ofisa Uhusiano wa Halmashauri hiyo, Innocent Byarugaba, alipozungumza na Nipashe.

Byarugaba alisema kati ya fedha hizo Sh. 140,750,000 ni kwa ajili ya usimamizi na ushauri na Sh. 804,309,600 ni kwa ajili ya machinjio hiyo katika eneo la Mtakuja Kata ya Pangani.

Machinjio hiyo ambayo inajengwa na mkandarasi M/S Petra Construction. co.L.td, ujenzi wake ulianza Aprili 2019 na alitarajiwa kukamilisha kazi Novemba 2019.

Byarugaba alisema kuwa kwa awamu ya kwanza kazi za miradi huo zimefikia asilimia 90, na malipo yaliyofanyika hadi sasa ni Sh. 459,279,586.47.

Alisema, katika utekelezaji wa mradi huo zipo changamoto ambazo zimesababisha mkandarasi kushindwa kukamilisha kwa wakati, ikiwamo mvua zilizonyesha katika kipindi cha mkataba zilizosababisha kasi ya ujenzi kupungua.

Changamoto nyingine ilielezwa ni kubadilika kwa eneo la ujenzi wa machinjio na mipaka kati ya msitu wa hifadhi ya Ruvu na Halmashauri ya Mji Kibaha.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuimarisha mapato ya halmashauri, kupitia uuzaji wa ngozi, damu na ushuru wa kuchinjia.

HABARI KIMATAIFA

## Waziri Mkuu kuwatetea wafiwa ajali ya ndege

**OTTAWA, Canada**

WAZIRI Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, amesema atawapigania ndugu wa abiria waliofariki katika ajali ya ndege ya Ukraine iliyodunguliwa na Iran wapate haki zao.

Trudeau alisema hayo mjini Edmonton, katika mkesha wa kuwakumbuka raia 57 wa Canada waliouawa katika tukio hilo wakati akizungumza na idadi ya wananchi 2,300 katika ukumbi wa mazoezi katika chuo kikuu.

Waziri Mkuu aliahidi kupata majibu kutoka kwa Iran, ambayo imekiri majeshi yake ilidungua kimakosa ndege hiyo, na kuua abiria wote 176 waliokuwa ndani ya ndege hiyo.

Awali Iran ilikuwa imekana madai kwamba inastahili kulaumiwa kutokana na ajali hiyo.

"Mkasa huu usingetokea kabisa, nataka kuwahakikishia kwamba nitashirikiana na nyinyi kikamilifu wakati huu mgumu ... mnatupa sababu ya kufuatilia suala hili ili haki ipatikane na kuwawajibisha waliohusika, Hatutapumzika hadi tupate majibu," alisema Trudeau.

Trudeau alikuwa akihudhuria ibada ya kuwakumbuka walioathiriwa, huku maandamano dhidi ya viongozi wa serikali yakiingia siku ya pili nchini Iran.

Iran ilikubali kudungua ndege hiyo baada ya kukanusha kufanya hivyo hapo awali, na kusababisha wasiwasi zaidi kati ya nchi hiyo na Marekani. Ndege hiyo iliyokuwa ikielekea mji mkuu wa Kyiv, ilidunguliwa karibu na mji wa Tehran Jumatano iliyopita, muda mfupi baada ya Iran kurusha makombora dhidi ya kambi mbili za kijeshi za Marekani nchini Iraq.

Mashambulizi hayo yalikuwa ni hatua ya kujibu mauaji ya ofisa mkuu wa Iran, Komanda Qasem Soleimani aliyeuawa kwenye shambulizi la ndege inayojiendesha yenyewe mjini Baghdad Januari 3, mwaka huu.

**BBC**

# Marekani yaionya Iran kushambulia raia wake

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameionya Iran dhidi ya kuwaua raia wake wanaoandamana kuipinga serikali baada ya kukiri iliidungua ndege ya abiria ya Ukraine.

Haya yamejiri wakati Waziri wa Ulinzi wa Marekani, Mark Esper, akisema milango iko wazi kwa Iran kufanya mazungumzo na Marekani bila masharti yoyote.

Ujumbe huo wa Trump umekuja wakati ambapo uongozi wa Jamhuri hiyo ya Kiislamu unakabiliwa na changamoto kutoka kwa waandamanaji walio na hasira baada ya nchi yao nusra iingie kwenye vita na Marekani baada ya mashambulizi ya kulipiziana kisasi.

Katika ujumbe aliouandika kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter, Rais Trump alieleza kuwa ulimwengu na hasa Marekani inatazama yanayoendelea nchini humo kwa sasa.

Lakini licha ya onyo la rais huyo wa Marekani, video zilizowekwa kwenye mitandao ya kijamii zinaonyesha polisi ya Iran na majeshi yakifyatua risasi za moto na mabomu ya kutoa machozi ili kuwatawanya waandamanaji karibu na eneo la Azadi huku baadhi ya waandamanaji wakionekana wakitoka damu.

Lakini mkuu wa polisi mjini Tehran, Hossein Rahimi alikanusha huku akisema kuwa maofisa wake walipewa masharti ya kutowakabili waandamanaji.

Mashirika ya kimataifa ya kutetea haki za binadamu nayo yamejitokeza na kuitaka Jamhuri hiyo ya Kiislamu kuwaacha raia kuandamana kwa amani kama inavyoruhusu katiba ya nchi hiyo.

Kufariki kwa abiria wote 176 waliokuwa kwenye ndege iliyodunguliwa wiki iliyopita na kukiri kwa Iran baadaye kwamba kikosi chake kililenga ndege hiyo kimakosa kwa kufikiri kuwa lilikuwa ni kombora ndiyo chanzo kilichosababisha maandamano kote nchini humo.

Canada ambayo ilikuwa na idadi kubwa ya wahanga katika tukio hilo inaendelea kuomboleza huku Waziri mkuu, Justin Trudeau akiahidi haki kwa familia zilizowapoteza wapendwa wao.

"Nataka kuzihakikishia familia zote na Wacanada wote, hatutapumzika hadi tutakapopata majibu, hatutopumzika hadi kutakapokuwa na haki na uwajibikaji," alisema Waziri Mkuu Trudeau.

Wakati huohuo, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza wametoa wito kwa Iran kuendelea kutekeleza mkataba wa mwaka 2015 ambao unadhibiti mpango wa nyuklia wa nchi hiyo.

***DW***



Rais wa Marekani, Donald Trump (Katikati) akiongea na vyombo vya habari wakati akiionya Iran kuacha kuwashambulia raia wa Marekani wanaoishi nchini humo. **PICHA: AFP**

# Ramaphosa ajawa hofu kuhusu Libya

**JOHANNESBURG, Afrika Kusini**

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ameelezea wasiwasi wake kuhusu mgogoro wa Libya, wakati akijiandaa kumrithi Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sissi kwenye uongozi wa Umoja wa Afrika (AU).

Rais Ramaphosa aliyasema hayo alipokuwa akimpokea Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed ambaye alikuwa kwenye ziara ya kiserikali nchini humo mwishoni mwa wiki hii.

Wawili hao walijadili kuhusu uhusiano kati ya nchi zao mbili, lakini walijadili masuala mbalimbali kuhusu Bara la Afrika.

Rais Ramaphosa anajiandaa kuchukuwa mikoba ya Rais wa Misri, Abdel Fattah al-Sissi kama Rais wa Umoja wa Afrika wakati wa mkutano wa kilele mwezi Februari.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Ethiopia alithibitisha kwamba Uchaguzi Mkuu utafanyika nchini mwake mwezi Mei au Juni mwaka huu.

Atakapochukuwa uongozi wa Umoja wa Afrika, Cyril Ramaphosa anatarajia kutafuta suluhu mgogoro wa Libya, ambao unaendelea kuiathiri nchi hiyo.

"Umoja wa Afrika umedhamiria kukomeza vita katika nchi mbalimbali za bara hili, na Libya ni nchi ambayo ni muhimu sana barani Afrika kwa mpango wetu. Tunakaribisha tangazo la kusitisha mapigano, ambalo linatupa fursa ya kujenga suluhisho la amani. Tunapaswa tupate suluhisho kutoka nchi za Afrika kwa matatizo yanayozikabili nchi za Afrika," alisema Ramaphosa.

Waziri Mkuu Ahmed anatarajia kwamba Rais Ramaphosa pia ataweza kuchangia katika mazungumzo katika mzozo kuhusu bwawa la Renaissance.

"Kama rafiki wa Ethiopia na Misri, kama ndugu, anaweza naweza kusimamia mazungumzo kati ya wadau tofauti ili kusuluhisha tatizo hilo kwa amani," alisema Ahmed.

Lakini Afrika Kusini haina picha nzuri kwenye Bara la Afrika, baada ya wimbi la ghasia dhidi ya wageni waishio nchini humo zilizotokea Septemba mwaka jana.

Hata hivyo, Ramaphosa amehakikisha kuwa serikali ya Afrika Kusini iko wazi kabisa kwa suala hilo.

"Wale wote ambao wapo Afrika Kusini wanakaribishwa, na kamwe hawapaswi kushambuliwa na mtu yeyote," alisema Ramaphosa.

Ramaphosa pia anatarajia kutumia mamlaka yake kwenye uongozi wa Umoja wa Afrika kuwezesha biashara kwa kukamilisha uanzishwaji wa eneo la biashara huria.

***RFI***

# Adaiwa kujiua kwa sumu kisa wivu wa mapenzi

**Na Stevie Chindiye, NAMTUMBO**

MKAZI wa kijiji cha Magazini wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma, Njawala Ally (37), amefariki dunia kwa madai ya kunywa sumu.

Inadaiwa alichukua hatua hiyo kutokana na wivu wa mapenzi kwa mkewe.

Taarifa zilizopatikana zinaeleza kuwa aliamua kujiua kwa kunywa dawa pamoja na pombe kali.

Shemeji wa marehemu, Daudi Goliama, alisema kuwa alikuwa anasumbuliwa na kisukari kwa muda mrefu akiwa anatumia dawa pamoja na sindano, na kwamba madaktari wa Hospitali ya Misioni ya Peramiho walimzuia kunywa pombe wakati akiwa anakunywa dawa hizo.

Alisema baada ya kunywa dawa nyingi za kisukari na pombe kali alizidiwa, huku akitamka sababu ya kifo chake.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Magazini, Ally Manoni, alithibitisha kifo cha mtu huyo na kudai kuwa kimesababishwa na kunywa dawa nyingi za homa ya kisukari pamoja na pombe kali.



Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Mwakilishi wa Mtawala wa Ras Al-Khaimah, Mohamed Ali Musabeh Al Nuaimi, alipofika Ikulu ndogo Migombani jijini Zanzibar jana, kwa mazungumzo. Wa pili kulia ni Balozi wa Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) nchini, Khalifa Abdulrahman Almarzooqi na Mkurugenzi Mtendaji wa RAK Gas, Nishant Dighe. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Wazee Chadema wataka tume huru ya uchaguzi

**Na Enock Charles**

BARAZA la Wazee la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), limesema chama hicho hakina mpango wa kususa kushiriki uchaguzi mkuu wa mwaka huu, lakini linaona kuna haja kuwa na tume huru ya kuuendesha.

Katibu Mkuu wa Baraza hilo, Lodrick Lutembeka, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa, chama hicho kilisusa kushiriki uchaguzi wa serikali wa mitaa mwishoni mwa mwaka jana, ili kutengeneza ushahidi wa kile alichodai kuvurugwa kwa uchaguzi na vyombo vinavyohusika na sasa watajielekeza katika kudai tume huru.

"Suala la kususia uchaguzi awamu hii halipo, sisi tulikuwa tunatengeneza mazingira ya ushahidi na wote mmeona na dunia imeona, sasa kutazamia kwamba tutasusa uchaguzi, hilo halipo na ndiyo maana tunadai kutengenezwa kwa mazingira sawa ya kushiriki uchaguzi," alisema.

Katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 24 jana, Chadema, Chama cha ACT-Wazalendo, Chama cha Wananchi (CUF),

NCCR-Mageuzi, UPDP na NLD vilijitoa katika mchakato wa uchaguzi huo vikilalamikia wagombea wake kuenguliwa kwa sababu walizodai ni za kutunga na zenye lengo la kuwakandamiza kisiasa.

Tangu kuchaguliwa kwa uongozi mpya wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini, Chadema, kumekuwa na hoja ya kudai ya kuundwa kwa chombo huru cha kusimamia uchaguzi mkuu ujao unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Chama hicho kinadai tume iliyopo sasa haina uhalali wa kusimamia uchaguzi huo kwa kuwa si huru.

# Wapewa elimu ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu, KIGOMA**

MAOFISA wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) wametoa elimu ya viwango kwenye mikoa ya Kigoma, Dodoma na Tabora kuhusu faida za kutumia bidhaa bora.

Akizungumza na gazeti hili jana kuhusiana na elimu hiyo, Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema mkoani Kigoma maofisa wa shirika hilo walitoa elimu hiyo katika Wilaya ya Kakonko ambako katika Soko la Omuruganza walifikia wananchi 200, katika Shule ya Sekondari Kakonko wanafunzi 838 na wajasiriamali 20.

Alisema wajasiriamali walipatiwa elimu kuhusiana na namna ya kupata alama ya ubora ya TBS.

Mayugu alitoa wito kwa wajasiriamali kutumia fursa ya huduma ya bure ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao ambayo inatolewa na serikali kwa lengo la kuinua wajasiriamali na hatimaye kuwawezesha kushindana na kuuza bidhaa zao katika masoko ya ndani na nje ya nchi bila vikwazo vya kibiashara.

Alisema kinachotakiwa ni mjasiriamali kupata barua ya utambulisho kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na wakiipeleka TBS mchakato wa kuthibitisha ubora wa bidhaa zao unaanza mara moja.

Pia alisema wajasiriamali hao walielimishwa kuhusiana na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 ambayo yameleta mabadiliko katika Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009.

Kutokana na mabadiliko hayo, majukumu ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula na vipodozi ambayo awali yalikuwa chini ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) sasa yanafanywa na TBS.

Alitaja huduma zinazotolewa na shirika hilo kwa sasa ni pamoja na usajili wa jengo, kusimamia masuala ya usalama na ubora wa chakula na vipodozi na upimaji wa bidhaa za vyakula na vipodozi kwa lengo la kudhibiti ubora.

Majukumu mengine ni utoaji wa leseni au cheti cha TBS kwa bidhaa za chakula na vipodozi na usajili wa bidhaa za vyakula na vipodozi vinavyotoka nje ya nchi.

Wajasiriamali hao waliipongeza TBS kwa kuwafuata kwenye maeneo yao na kuwapatia elimu kuhusiana na kupata alama ya ubora, pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili za kupata alama ya ubora.

Kuhusu majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na TFDA na TBS kwa pamoja na sasa kuhamia kwenye shirika hilo, wajasiriamali hao walipongeza serikali wakisema uamuzi wake umeondoa vikwazo walivyokuwa wakikumbana navyo.

Wajasiriamali hao waliliomba shirika hilo liendelee kuwafikia kwa uharaka, huku wakiishukuru serikali kwa kuondoa urasimu kwenye suala la chakula na vipodozi uliokuwa ukichangiwa na kushughulikiwa na taasisi mbili.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**TANZANIA RESEARCH AND CAREER DEVELOPMENT INSITUTE:** Inatangaza mhula mpya wa masomo Certificate na Diploma za kilimo na maendeleo ya jamii.maelezo zaidi tembelea tovuti yetu www.tracdi.ac.tz Simu:**0714404491/0746995144**

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MKOPO WA HARAKA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITD (EFL).** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumalizia tenda etc. Kwa maelezo zaidi **piga 0758 112 332. Karibu EFL**.

**WAHUDUMU WA HOTELI WANAHITAJIKA** Hoteli ndogo Bagamoyo inatafuta wahudumu, wapishi, usafi, bartender wenye vyeti. Kwa mawasiliano zaidi **Piga 0757 129 546.**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

## KUPOTEA KWA VYETI



115582602

**PAUL MAYALA MLELE.**

Anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne, shule ya Kahama Sekondari chenye Index **No.S.0461-0033** kilichotolewa mwaka 1997.Leaving Certificate ya kidato cha nne chenye **No.E.F.123.** Result slips ya kidato cha nne,shule ya Kahama Sekondari chenye No.174878 mwaka 1997.Cheti chakumaliza chuo cha Ualimu NDALA NZEGA mwaka 2002 chenye **No.072584.**
Yeyote atakaye viona atoe taarifa kituo cha polisi Taarifa ya kituo cha polisi **KAH/RB/TR/5701/2016.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115582702

**KULWA MAHILA NTAMBI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S.1334/0015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MHONGOLO PROGRESSIVE SEKONDARI** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIG/RB/157778/2019.**

## KUPOTEA KWA CHETI



115582702

**VICTOR PETER** anatangaza kupotea kwa cheti cha **DIPLOMA YA UDAKTARI** chenye namba **NS 1141/0139/2007** kilichotolewa na MVUMI TRAINING CENTER mwaka 2017. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/3275/2020.**

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMISTRATION CAUSE NO. 99 OF 2019**

**In the matter of application for letters admistration by EMMANUEL PAUL CHIUTU of P. O. BOX 1249, Dodoma Region .**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding,if they think fit before grand of probation or letters of admistration is made to the above named petitioner.

Objection to grant should be filed on or before the 16 day of January 2020.

Date at Dodoma this 8 day of January 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA REGION

115583102

**IN THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMISTRATION CAUSE NO. 100 OF 2019**

**In the matter of application for letters admistration by SIMON PETRO MSASAMBI of P. O. BOX 1249, Dodoma Region .**

**GENERAL CITATION**

All person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding,if they think fit before grand of probation or letters of admistration is made to the above named petitioner.

Objection to grant should be filed on or before the 16 day of January 2020.

Date at Dodoma this 8 day of January 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA REGION

115583302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WATOTO YA DAR ES SALAAM KISUTU**

**SHAURI LA MAOMBI YA MATUNZO YA MTOTO Na. 291 YA MWAKA 2019**

**THOMAS STEVEN OSASO.........MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**REHEMA SAIDI MOHAMEDI.........MJIBU MAOMBI**

**KWA: REHEMA SAIDI MOHAMEDI**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo ya mwombaji yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo yanaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo inakuhitaji kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 20/01/2020 saa 1:00 asubuhi.

**ANGALIA:** Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, utaweza kusikiliza maombi hayo na kutoa hukumu. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 19 mwezi wa 12/2019.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
KISUTU – DAR ES SALAAM

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WATOTO
KISUTU DAR ES SALAAM.

115582602


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MANE: TUNA NJAA NA TAJI LA EPL

**LIVERPOOL, England**

SADIO Mane amesema mastaa wa timu hiyo watajitoa mhanga kufanya kila kitu kuhakikisha wanamaliza ukame wa miaka 30 wa kushindwa kubeba taji la Ligi Kuu England.

Liverpool waliumizwa msimu uliopita wakati walipopigwa kikumbo na Manchester City kwenye ubingwa dakika za mwisho kabisa.

Lakini, mshambuliaji huyo Msenegali, Mane mwenye umri wa miaka 27, alisema hawawezi kuacha lile lililotokea msimu uliopita lijirudie msimu huu.

Liverpool mambo yao ni safi msimu huu wakiongoza ligi kwa tofauti ya pointi 13, huku wakiwaacha pointi 14 wapinzani wao kwenye mbio za ubingwa msimu uliopita, City.

"Tumejifunza kutokana na makosa ya msimu uliopita. Kile kilikuwa kipindi kigumu sana kwetu. Kwa sasa tunajaribu kufanya akili yetu iwe inafanya kazi muda wote," alisema.

"Unapopoteza ubingwa wa ligi kwa staili ile inaumiza sana akili. Mpango wetu ni uleule, kushinda kitu fulani. Kuna mechi nyingi sana mbele, lakini bado hatujachoka. Hilo halijawahi kuwa tatizo kwetu. Nadhani tupo vizuri msimu huu kuliko ule uliopita.

"Lazima ujitoe muhanga kama ulipatwa na kilichotupata. Na sasa tupo sambamba kwa mapambano hadi mwisho."

# POGBA HAONDOKI UNITED - WAKALA

**LONDON, England**

WAKALA wa Paul Pogba, Mino Raiola amesema mchezaji huyo atabaki Manchester United licha ya kutakiwa na Real Madrid na Juventus.

Kwa muda mrefu Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka United, lakini wakala huyo amesema haondoki Old Trafford.

Real Madrid na Juventus 'Kibibi Kizee' cha Turin zimeingia vitani kuwania saini ya kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Kocha Ole Gunnar Solskjaer amekuwa akisisitiza Pogba hauzwi licha ya kutakiwa na miamba hiyo ya soka Ulaya.

"Paul siku zote amekuwa na mapenzi na Manchester United na Manchester United inampenda Paul. Na mtu pekee wa kuzungumzia suala hili ni Ole kwa sababu aliandika kwa maandishi," alisema Raiola.

Alisema atasimamia kauli ya Solskjaer kwamba hatakubali kumwachia Pogba kuondoka United kwa kuwa ni mchezaji katika kikosi hicho.

Katika hatua nyingine, Raiola alisema hataki kujenga uadui na United baada ya mshambuliaji Erling Haaland kujiunga na Borussia Dortmund.

United ilikaribia kumnasa kinda huyo kabla ya kuzidiwa na Dortmund, lakini wakala huyo alisema ulikuwa ni uamuzi wake binafsi.

"Bado ana umri mdogo, naamini atakuja hapa katika wakati mwafaka. Nataka amani, sitaki uadui na Manchester United," alisema Raiola.



# ARSENAL KUSAJILI BEKI WA UFARANSA

**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal iko mbioni kuwania saini ya beki wa kati wa RB Leipzig, Dayot Upamecano wakati huu wa dirisha dogo la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Kocha Mikel Arteta atalazimika kuvunja benki kutoa pauni milioni 40 ambazo ni thamani ya beki huyo mwenye kiwango bora.

Muda mfupi baada ya kuteuliwa kocha mpya, Arteta alisema anataka kuboresha safu ya ulinzi aliyodai haichezi kwa kiwango bora.

Arsenal ina matumaini ya kupata saini ya mchezaji huyo aliyebakiza



miezi 18 kabla ya mkataba wake kumalizika.

Arteta anataka beki wa kati kuziba pengo la Calum Chambers aliyeumia katika mchezo waliofungwa mabao 2-1 na Chelsea, Jumapili iliyopita.

Beki huyo aliumia kifundo cha mguu na haijawekwa bayana atakuwa nje ya uwanja muda gani, hatua inayompasa kusaka mchezaji wa kuziba pengo hilo.

Arsenal imebakiwa na beki mmoja tegemeo mwenye uzoefu, David Luiz aliyejiunga na Arsenal katika usajili wa majira ya kiangazi msimu uliopita akitokea Chelsea.

Wakati Arteta anataka kuisuka upya Arsenal, nahodha wake Pierre-Emerick Aubameyang amemweka njiapanda kama atabaki Emirates au ataondoka.

## HABARI MICHEZO



# PEP: AGUERO NI MZURI, LAKINI HAKUNA KAMA MESSI

**MANCHESTER, England**

LICHA ya Sergio 'Kun' Aguero kufunga mabao matatu kocha Pep Guardiola amesema Lionel Messi ndiye mshambuliaji namba moja duniani.

Aguero alifunga mabao matatu katika mchezo wa jana usiku ambao Manchester City ilishinda 6-1 dhidi ya Aston Villa.

Guardiola alisema hakuna mchezaji wa kumpiku Messi ingawa Aguero amefanya kazi nzuri dhidi ya Aston Villa.

Kocha huyo alitoa kauli hiyo alipoulizwa nani mchezaji bora ambapo alijibu Messi akimtaja ni mshambuliaji mwenye kipaji.

Pia alipoulizwa kama Messi ni mchezaji bora namba tisa, Guardiola alijibu: "Messi ni namba 9, 10, 11, 7, 6, 5 na 4, lakini Sergio ni miongoni mwao," alisema Guardiola.

Aguero anayetoka Argentina kama Messi, amekuwa mchezaji wa kwanza raia wa kigeni kufunga mabao mengi katika Ligi Kuu England akifunga 175. Awali rekodi hiyo ilikuwa chini ya Thierry Henry aliyefunga 175.

Pia, Aguero amempiku nahodha wa zamani wa England, Alan Shearer kwa kufunga 'hat-trick' mara 12 tangu alipojiunga na City mwaka 2011.

"Nawapongeza wachezaji wote. Kuvunja rekodi ya mchezaji nguli kama Thierry Henry haikuja kwa kipindi kifupi, imechukua miaka," alisema Guardiola.

# ALLEGRI KUTUA UNITED WAKATI WOWOTE

**MANCHESTER, England**

**KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri amekataa kupokea ofa za kwenda kufanya kazi kwenye klabu nyingi akisubiria kiti anachokalia Ole Gunnar Solskjaer kule Manchester United, kwa mujibu wa ESPN.**

**Allegri aliachana na Juventus mwisho wa msimu uliopita baada ya kuiongoza timu hiyo kushinda ubingwa wa Serie A kwa misimu nane mfululizo.**

**Na wakati Mtaliano huyo, Allegri akiwahi kuhusishwa na timu kama Arsenal mwezi uliopita, imeelezwa kwamba bado anafikiria sana juu ya kukubali kazi nyingine kwani sasa anasikilizia hatima ya Solskjaer ndani ya kikosi cha Old Trafford.**

**Arsenal waliripotiwa kumfuata Allegri ili awe kocha wao, lakini Mtaliano huyo kwa sasa matumaini yake ni kwenda kufanya kazi na United, kwa mujibu wa Daily Mail.**

**Gazeti hilo liliripoti kwamba Allegri atakuwa na shughuli pevu kwa sababu Mauricio Pochettino naye anaitaka kazi ya kwenda kuinoa United baada ya kuachana na Tottenham alikofutwa kazi. Allegri kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na United.**

**Solskjaer alikuwa na uhakika wa usalama wa kibarua chake, lakini baada ya kipigo cha kutoka kwa mahasimu wao Manchester City kwenye Kombe la Ligi, kila kitu kinaonekana kuwa na shaka kubwa.**

**Kwenye Ligi Kuu England, kikosi hicho cha Solskjaer kiko katika nafasi ya tano, pointi tano nyuma ya Chelsea waliopo kwenye nafasi ya nne ambayo ni tiketi ya mwisho ya kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kupitia ligi.**

# TAMMY KUBEBA MAJUKUMU YA KANE

**LONDON, England**

TAMMY Abraham amesema yuko tayari kuvaa viatu vya Harry Kane katika fainali za Kombe la Mataifa ya Ulaya, Euro 2020.

Kane anaweza kukosa fainali hizo kwa kuwa amefanyiwa upasuaji wa mguu ambao unaweza kumweka nje ya uwanja hadi Aprili, mwaka huu.

Abraham alisema amejiandaa kuchukua mikoba ya nahodha huyo wa England ikiwa atakosa fainali hizo.

Mshambuliaji huyo wa Chelsea amekuwa katika kiwango bora baada ya kufunga mabao 13 na Jumamosi alichangia ushindi wa magoli 3-0 iliyopata timu hiyo dhidi ya Burnley.

"Namwangalia Harry Kane, ameumia lakini naamini atarejea uwanjani kuzikabili fainali za Ulaya. Itakuwa fursa endapo atashindwa kupona kwa wakati," alisema Abraham mwenye miaka 22.

Hata hivyo, alisema England ina idadi kubwa ya washambuliaji akiwataja Marcus Rashford, Jamie Vardy na Danny Ings ambao ni hodari wa kufunga mabao.

Abraham alisema anapenda kuicheza England na anasubiri fursa kuitwa kuongoza kikosi hicho katika eneo la ushambuliaji ikiwa nyota huyo wa Tottenham Hotspurs atakosa fainali hizo.

***



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL, MAN UNITED ZAJITOSA KWA KABASELE

Ni beki Mbelgiji ambaye ameonyesha kiwango kizuri ndani ya Watford ambayo imeanza...

**LONDON, England**

ARSENAL na Manchester United zimeweka wazi mpango wa kuwania saini ya beki wa Watford, Christian Kabasele, vyombo vya habari mbalimbali vimeandika.

Licha ya Watford kuanza vibaya msimu huu na sasa ikipambana kujiepusha na janga la kushuka daraja, lakini Kabasele ameonyesha kiwango cha juu katika mechi mbalimbali alizocheza za timu hiyo.

Watford inatajwa imeanza kuimarika katika siku za hivi karibuni baada ya Kocha Nigel Pearson kutua klabuni hapo.

Kabasele anatarajia kukubali kusaini mkataba mpya na klabu yake hiyo wakati wowote kuanzia sasa na mkataba huo utamalizika mwaka 2024.

Lakini gazeti la Ufaransa liitwalo Le10 Sport limeandika kuwa klabu hizo kubwa za Ligi Kuu England zinamwania beki huyo na zinataka kumsajili katika dirisha dogo la Januari ambalo linaendelea.

Arsenal na United zimetajwa kumwania beki huyo raia wa Ubelgiji kwa udi na uvumba ili kuimarisha safu zao za ulinzi.

West Ham na Newcastle pia nazo zinatajwa kujipanga kumsajili Kabasele ili kuimarisha vikosi vyao.

Kabasele ambaye amepambana kupata namba tangu alipojiunga na Watford mwaka 2016 kwa dau la pauni milioni 6, ameichezea timu hiyo mechi zinazokaribia 100.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 28 ameichezea Timu ya Taifa ya Ubelgiji mechi mbili.

Arsenal inahitaji beki mpya baada ya kumpoteza beki wake, Calum Chambers ambaye aliumia na atarejea uwanjani baada ya msimu huu kumalizika huku United pia ikiwa imeingia sokoni kuimarisha kikosi chake kwa kumwania nyota huyo.

Kabasele alikosa mechi ambayo Watford ilipata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bournemouth baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu wakati timu yao ikiibuka mshindi dhidi ya Wolves.

## KWA UFUPI

**ERIKSEN KUTUA MILAN**

KIUNGO wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen, ambaye mkataba wake utamalizika majira ya joto amefikia makubaliano ya kusaini mkataba wa miaka minne na nusu na Inter Milan. Spurs inataka kulipwa dau la pauni milioni 17 kumuuza nyota huyo raia wa Denmark katika dirisha hili la Januari. ***(La Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**POCHETTINO ANUKIA BARCA**

BARCELONA imeanza mawasiliano na Mauricio Pochettino kuhusu uwezekano wa kurithi mikoba ya Ernesto Valverde. Kocha huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 47 hajajiunga na timu yoyote tangu Novemba mwaka jana alipofukuzwa na Spurs. ***(Catalan radio station RAC1, via AS)***

**DUNK AKARIBIA CHELSEA**

CHELSEA imeanza mchakato wa kumwania beki wa kati wa Brighton na Timu ya Taifa ya England, Lewis Dunk (28), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 50. ***(Times - subscription required)***

**BELLINGHAM AKARIBIA UNITED**

MANCHESTER United imeungana na klabu nyingine mbili kuwania saini ya kiungo wa Birmingham City na Timu ya Taifa ya vijana ya England (U-17), Jude Bellingham, ambaye ana umri wa miaka 16. ***(Mirror)***

**GREALISH BADO SANA**

STRAIKA wa zamani wa Aston Villa, Gabby Agbonlahor, anafikiria United itatoa dau la pauni milioni 70 ili kumsajili Grealish, lakini akaongeza kuwa kiungo huyo atatua Old Trafford katika kipindi cha majira ya joto kama klabu yake itashuka daraja. ***(Express)***

**SANTO AMWOTA LEMAR**

KOCHA wa Wolves, Nuno Espirito Santo, amemtaja winga wa Atletico Madrid, Thomas Lemar kuwa ndiye mchezaji namba moja anayehitaji kuona anamsajili, huku akifahamu Arsenal, Tottenham na Chelsea pia zinamwinda Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Goal)***

**MUSTAFI ANUKIA UTURUKI**

WAKALA wa beki wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Shkodran Mustafi amesema anaendelea na mazungumzo ya Galatasaray ili kufanikisha mchakato wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 kutua katika klabu hiyo ya Uturuki. ***(Fotomac, via Express)***

**DEMIRAL AMVURUGA SARRI**

BEKI wa Juventus, Merih Demiral, ambaye anahusishwa na tetesi za kutua Arsenal alitolewa kwenye machela wakati timu yake ikishinda mabao 2-1 dhidi ya Roma katika mechi ya Serie A iliyochezwa juzi na Kocha wake, Maurizio Sarri anahofia nyota huyo amepata jeraha kubwa katika enka. ***(Football.London)***

**ETHERRIDGE AINGIA SOKONI**

WEST Ham United imepeleka ofa ya thamani ndogo ya pauni milioni saba kwa Cardiff City ili kumsajili golikipa wa Timu ya Taifa ya Ufilipino, Neil Etheridge, ambaye ana umri wa miaka 29. ***(Football Insider)***

**YOUNG AGEUKA LULU**

CRYSTAL Palace na Lazio ya Italia zimejiunga katika mbio za kuwania saini ya beki wa Manchester United, Ashley Young, ambaye amepewa ofa ya mkataba wa miezi 18 wa kutua Inter Milan. ***(Sun)***

**LEICESTER YAMTOA THOMAS**

MABOSI wa Leicester City wamekubali kumpeleka kwa mkopo mshambuliaji wake kutoka Wales, George Thomas (22), katika klabu ya ADO Den Haag ya Uholanzi ambayo inafundishwa na Kocha wa zamani wa Newcastle United, Alan Pardew. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# HARERIMANA ATANGAZWA RASMI KOCHA MPYA KMC

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Lipuli FC ya Iringa, Haruna Harerimana, ametangazwa rasmi kujiunga na timu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, KMC FC ya jijini Dar es Salaam.

Harerimana ametua KMC kuchukua nafasi ya Mganda Jackson Mayanja ambaye mkataba wake ulisitishwa kutokana na timu hiyo kutokuwa na mwenendo mzuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa waliyoshiriki.

Mwenyekiti wa Bodi ya KMC, Benjamin Sitta, alisema jana jijini kuwa uongozi wa klabu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni umeingia mkataba wa miezi 18 na kocha huyo baada ya kukidhi vigezo walivyoviweka.

Sitta alisema kuwa Harerimana amepitishwa na bodi ya timu ambayo ilipitia maombi kutoka kwa makocha mbalimbali wa ndani na nje ya Tanzania walioomba kuchukua nafasi iliyoachwa na Mayanja.

"Mchakati wa kutafuta kocha haukuwa rahisi kutokana na ujuzi na uzoefu wa makocha waliomba kuchukua nafasi ya Mayanja, ambayo ilishikiliwa kwa muda na Kaimu Kocha Mkuu, Hamadi Ally," alisema Sitta.

Alisema tayari Harerimana ametambulishwa kwa wachezaji na ameanza kazi ya kuinoa KMC kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri katika Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA. "Ni kocha ambaye amekidhi vigezo vyote ambavyo tumeweka na uongozi kuamua kuingia naye mkataba. Kupitia yeye, tunaamini timu itafanya vema na kurejesha ubora wake wa msimu uliopita," alisema Sitta.

Harerimana alisema amekuja kufanya kazi na kama ilivyo makocha wengi duniani, amejipanga kuipa mafanikio.

"Nimekuja kufanya kazi yenye mafanikio, hivyo naomba wachezaji tushirikiane katika kuleta matokeo chanya ya timu na kumaliza ligi katika nafasi nzuri. Nimefurahi kupata uongozi ambao unajali maslahi ya wachezaji na watendaji wa timu," alisema Harerimana.

Wakati huo huo, KMC imefikia makubaliano ya kuachana na wachezaji watano kutokana na sababu mbalimbali.

Wachezaji hao ni pamoja na Aaron Lulambo, George Sangija, Rehani Kibingu, Melly Mongolare na Janvier Besala Bokongu.



Beki wa Timu ya Taifa ya Vijana ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17, Protasia Mbunda (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Burundi, Annonciatte Nshimirimana katika mechi ya kwanza ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Shime afunguka kazi haijamalizika

**Na Shufàa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, Bakari Shime amewataka Watanzania wazidi kuisapoti timu hiyo huku akisema kazi bado haijamalizika.

Tanzania juzi ilianza vema kampeni ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia kwa kuifunga Burundi magoli 5-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime alisema ushindi huo umetokana na wachezaji wake walifuata maelekezo na anaamini wataendelea na kasi hiyo katika mchezo wa marudiano.

Alisema hata hivyo wapinzani wao wameonyesha kiwango kizuri na waliingia katika mchezo huo kwa kutowadharau kutokana na kukumbuka sare ya mabao 3-3, waliyoipata mara ya mwisho walipokutana.

"Wachezaji wangu wamenifurahisha kwa sababu wamefanya niliyokuwa nayataka kuhakikisha wanaipeperusha vema bendera ya Taifa," alisema Shime.

Alisema amewashukuru Watanzania kwa ushirikiano na wataendelea kujiimarisha ili wafanye vema katika mchezo wa marudiano.

"Nawashukuru Watanzania kwa sapoti waliyotuonyesha kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kushuhudia kazi inayofanywa na mashujaa wao," Shime alisema.

Naye beki wa timu hiyo, Protasia Mbunda, alisema wanashukuru Mungu kwa matokeo mazuri waliyoyapata licha ya mchezo huo kuwa mgumu.

Mbunda alisema siri ya mafanikio ni kumsikiliza mwalimu wao kwa makini na kufuata maelekezo anayowapa.

"Tunashukuru kwa matokeo tuliyoyapata, mchezo ulikuwa mgumu, lakini tumejitahidi mpaka tumepata ushindi," alisema nyota huyo ambaye alifunga bao moja.

Mabao mengine katika mechi hiyo yalifungwa na Joyce Meshack na Aisha Masaka ambaye alifunga hat-trick.

Timu hizo zinatarajia kurudiana Januari 25, mwaka huu mjini Bujumbura.

# Tanzanite kuivaa Uganda Jumapili

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), inatarajia kuwakaribisha wenzao kutoka Uganda katika mechi ya kwanza ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Dunia itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Tanzanite, Bakari Shime, alisema kikosi hicho kinaendelea vizuri na mazoezi na anaamini wataanza vema kampeni ya mashindano hayo.

Shime alisema wamejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa Uganda ambayo inaundwa na wachezaji wenye uwezo na uzoefu wa kushiriki mashindano mbalimbali ya kimataifa.

"Timu inaendelea vizuri na mazoezi, idadi kubwa ya wachezaji wa timu hii walikuwa kwenye kambi yetu kabla ya kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji, tunaamini tutafanya mambo mazuri hapa nyumbani," alisema Shime.

Alisema kuwa kikosi chake hakina mchezaji majeruhi na alimtaja Shamimu Ally ambaye aliumia katika mchezo wa juzi dhidi ya Burundi anaendelea vema.

Tanzanite ilitumia ziara ya Algeria kujiimarisha kuelekea mashindano hayo ambapo ikiwa huko ilishinda mechi moja, sare moja na ilifungwa na wenyeji goli 1-0.

Kikosi cha Uganda kinatarajiwa kuwasili nchini kwa ajili ya mchezo huo Ijumaa pamoja na waamuzi wa mechi hiyo ambao wanatoka Kenya.

Michezo
Jumanne Januari 14, 2020
Nipashe



Arsenal, Man United zajitosa kwa Kabasele

HABARI UK 30



Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla (wa pili kushoto), akionyesha nakala ya mkataba wa kazi baada ya Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Luc Eymael (kulia) na Kocha wa Viungo, Riedoh Berdien (kushoto), kusaini jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: YANGA SC**

# YANGA SC, KAGERA TAMBO ZATAWALA

## Ni kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa kesho jijini...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI uongozi wa Yanga jana uliwapa rasmi mikataba makocha wake wapya, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, ametamba timu yake itapata matokeo mazuri katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Makocha wa Yanga waliopewa mkataba wa miezi 18 kila mmoja ni Kocha Mkuu Mbelgiji Luc Eymael na Msaidizi wake, Riedoh Berdien ambaye ni kocha wa mazoezi ya utimamu wa mwili.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli aliliambia gazeti hili jana wamekamilisha mazungumzo na makocha hao na wana imani wataipa mafanikio klabu yao.

"Kile kitu kimekamilika, Luc Eymael na Riedoh Berdien ni mali yetu (Yanga) hadi Juni mwaka 2021, karibuni sana tuijenge Yanga," alisema kwa kifupi Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema kikosi chao kimekamilika na sasa wamejipanga kuendeleza ushindi katika ligi hiyo ambayo ubingwa wake unashikiliwa na watani zao.

"Kwa sasa tuko vizuri kila idara, tulitumia muda wa dirisha dogo kujiimarisha, tunawaomba mashabiki na wanachama wetu wasiwe na wasiwasi, Yanga iko imara na imedhamiria kurejesha heshima," Bumbuli alisema.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, amesema kikosi chake kimejiandaa kuweka rekodi mpya ya kupata pointi tatu dhidi ya Yanga.

Maxime alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri na leo asubuhi wanatarajia kuendelea na mazoezi kwenye Uwanja wa Kawe ili kuhakikisha wanaingia uwanjani wakiwa na ari ya ushindi.

"Wamekuwa wakinisumbua sana, ila msimu huu nimejiandaa kuvunja mwiko, tangu nimekuwa na Kagera Sugar sijawafunga, ila mechi ya keshokutwa (kesho), watashangaa," alisema Maxime.

Aliongeza kuwa kiufundi wachezaji wake wanauwezo wa kupata ushindi na anachohitaji ni kuona wanaongeza utulivu wanapokuwa na mipira.

"Kama tutaamka vema, nina uhakika tutapata pointi tatu, mazoezi ya mwisho tutafanya kesho (leo) asubuhi, nitapata picha ya nani ataanza na nani ataanzia benchi," aliongeza nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Baada ya mechi hiyo ya keshokutwa, Yanga itaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kukutana na Azam FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Simba yaifuata Mbao FC kibabe

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajiwa kuwasili jijini Mwanza leo tayari kuwavaa wenyeji Mbao FC katika mechi ya ligi hiyo itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, imeelezwa.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili jana kikosi hicho kimeamua kwenda mapema jijini humo ili kuwapa nafasi ya kupumzika wachezaji wao ambao wametoka katika fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Rweyemamu alisema hakuna mchezaji ambaye ni majeruhi, benchi la ufundi limedhamiria kuona wachezaji wanapambana katika kila mchezo ulioko mbele yao.

**"Tutaondoka Zanzibar kesho (leo) na tutaunganisha moja kwa moja kuelekea Mwanza kesho (leo) hiyo hiyo, hatutakuwa na kituo Dar es Salaam, ukiiangalia ratiba haionyeshi nafasi ya kupumua, tutapumzikia huko huko," Rweyemamu alisema.**

Simba ambao ni vinara wa Ligi Kuu Bara wakiwa na pointi 35 baada ya kucheza mechi 14, watabakia jijini huko kwa ajili ya mechi nyingine dhidi ya Alliance FC itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

Ndanda FC ya Mtwara yenye pointi tisa na imeshuka dimbani mara 17 ndio inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 20 na ambayo itateremka klabu sita msimu huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >